*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## Kikao cha Tatu – Tarehe 31 Oktoba, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnajua mashine za kuzuia simu zisiweze kufanya kazi ndani hazifanyi kazi vizuri sasa. Kwa mujibu wa Kanuni zetu naomba mzime simu zenu. Katibu tuendelee.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema maswali kwa Waziri Mkuu hayapo Kwa hiyo, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atauliza swali la kwanza. Kwa niaba yake Mheshimiwa Malocha.

Na. 30

**Kasoro Zilizoko Kwenye Sekondari za Kata**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA (K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** aliuliza:-

Wazo la Serikali kujenga Sekondari za Kata nchi nzima ni wazo zuri na limefanikiwa kujenga sekondari hizo lakini zinakabiliwa na kasoro au changamoto mbalimbali kama vile ukosefu wa madawati, maabara, upungufu wa walimu, nyumba za kuishi walimu na hata hosteli za wanafunzi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuondoa kasoro hizo na kuziboresha zaidi hasa kwa Sekondari za Mkoa wa Rukwa Jimbo la Kalambo?

(b) Sheria ya Elimu imemtaka mzazi/mlezi kuhakikisha kuwa mtoto anayepaswa kwenda shule anakwenda shule, lakini sheria haisemi chochote kuhusiana na mwanafunzi wa sekondari. Je, kuna udhati wa kukuza elimu katika hali kama hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU]

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizi kwa kupeleka fedha za ununuzi wa madawati ujenzi wa maabara, nyumba za walimu ukarabati wa shule kongwe na kuajiri walimu wapya. Mwaka wa fedha 2010/2011.

Serikali ilitoa shilingi bilioni 3 kwa ajili ya ujenzi wa maabara, kati ya fedha hizo mkoa wa Rukwa ulipelekewa milioni 160 na shilingi bilioni 2.6 zilitolewa pia kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe na mkoa wa Rukwa ulipewa shilingi milioni 150 kwa ukarabati wa shule za sekondari za Mpanga, Nkasi na Kantalamba. Mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ilitoa shilingi milioni 600 kwa ajili ya maabara hamishika *mobile laboratory,* mkoa wa Rukwa ulipata shilingi milioni 24.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali iliidhinisha shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na ununuzi wa madawati ambapo kati ya hizo mkoa wa Rukwa ulipata shilingi bilioni 130.9.

Aidha, katika mpango wa uboreshaji wa miundombinu ya sekondari, ikiwemo maabara nyumba za walimu na madarasa tayari shilingi bilioni 26.4 zimetolewa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, katika kufanikisha uboreshaji wa shule 264 ambapo mkoa wa Rukwa umepatiwa jumla shilingi milioni 687.4 na katika robo ya mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali imetoa shilingi bilioni 8 ambazo zinatumika katika ujenzi wa nyumba za walimu, na mkoa Rukwa umepata shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kukabiliana na changamoto hizi, mwezi Machi, 2013 Serikali iliajiri walimu wa shule za sekondari, 14,096 wakiwemo 4,176 wa stashahada, 9920 wa Shahada, Rukwa ilipata walimu 276 wakiwemo wa stashahada 180 na shahada 96 kwa mwaka wa 2013/2014 tayari mipango ya kuajiri walimu wapya imekamilika baada

ya kibali cha ajira kutoka walimu wapya watakaopangwa tena nchi nzima ikiwemo mkoa Rukwa na halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na ugatuaji wa shule za sekondari kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, tunahitaji kufanya marekebisho ya sera ya sheria na elimu ili kuweza kukidhi mahitaji ya sasa. Katika marekesho hayo suala la kumlinda mwanafunzi litazingatiwa.

Kwa sasa sera ya Serikali ni kwamba walau asilimia 50 ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi wajiunge na shule za sekondari. Hivyo Serikali inatoa utaratibu unaowalinda wanafunzi hawa ukiwemo waraka namba 6 wa mwaka 2004 ambao unatoa maelekezo kuhusu adhabu inayotakiwa kutolewa kwa wanafunzi kwa wale wanaowapa mimba wanafunzi wasichana.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni ukweli usipingika kwamba jiografia ya Kalambo ukilinganisha na maeneo mengine ya Tanzania yana utofauti mkubwa sana. Je, Serikali kwa kuzingatia uhalisia wa wilaya hii na jiografia yake, itaekeleza mpango mahususi kuhakikisha kwamba tatizo hili mahususi kwa Kalambo linatatuliwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua jiografia ya maeneo yale ya Sumbawanga na ndiyo sababu pia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI iliridhia ombi la wananchi wale kuanzishwa kwa Halmashauri ya Kalambo ili kupata huduma kwa ukaribu zaidi na migao yote ninayoitamka hapa wilaya ya Kalambo inapata *share* yake na kwa hiyo huduma kwa halmashauri ya Kalambo inapata kwa ukaribu zaidi.

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU],

Huo ndiyo utaratibu ambao tumeutumia maeneo yote makubwa yenye mazingira makubwa magumu tumeyapa mamlaka ya kuwa na halmashauri za wilaya ili kuwasogezea huduma zote hizi. Kwa hiyo mikakati ya elimu iliyopo pamoja na mikakati mingine yote ya Serikali ni kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi walioko kwenye maeneo haya.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru pamoja na jitihada hizo za Serikali lipo tatizo kubwa la wanafunzi ambao wanashindwa kuendelea na masomo ngazi za juu na mkoa wa Rukwa hauna chuo kimoja cha ufundi cha *VETA*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha kujenga chuo cha ufundi *VETA* ili kuokoa kundi kubwa la watoto hao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kama tunavyoongea kila siku mpango wa kujenga vyuo vya *VETA* kwa kila mkoa hii mikoa mipya minne na kwa kila wilaya.

Lakini kwa upande wa Rukwa tayari kuna Chuo cha *VETA* Mpanda, mkoa wa Katavi, ambao ni mkoa mpya tayari kuna Chuo cha *VETA* pale Mpanda. Lakini mkoa wa Rukwa zamani tulikuwa tunasema kwamba kuna Chuo cha mkoa wa Rukwa kwa sababu sasa baada ya kugawanywa ndiyo ikaenda kule Mpanda kwa hiyo, tunatambua kwamba hii mikoa minne mipya ikiwemo na mkoa wa Rukwa tutajenga Chuo cha VETA kwa mipango iliyopo.

Mheshimiwa Malocha, ni jana tulikuwa tunazungumza na wewe pamoja na Mheshimiwa Mipata kwamba wakati hawa wakandarasi walikuwa wanajenga barabara ya kutoka Tunduma mpaka Rukwa tayari kuna majengo yameachwa pale na tayari tumeshawaagiza kwamba muandike barua *RCC* waweze kutuandikia barua Wizara ya Elimu ili majengo yale mkitupatia tuweze kutoa mafunzo ya *VETA* kwenye yale majengo.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kati ya Wilaya zilizofanikiwa sana katika ujenzi wa shule za Kata ni pamoja na wilaya ya Rombo, ambapo karibu kila kata ina shule mbili za sekondari. Sasa kumekuwa na ongezeko kubwa sana la vijana waliomaliza elimu ya sekondari lakini hawana nafasi ya kuendelea mbele ili lengo lao la kujitegemea liweze kufikiwa.

Sasa Serikali haioni kwamba ili kuharakisha ujenzi wa hizi shule za kata baadhi ya wilaya kama Rombo ambayo ina shule nyingi baadhi ya shule zikageuzwa na kufanywa vyuo vya ufundi ili kuweza kuwachukua hao vijana ambao sasa baada ya *form four* wanazagaa mtaani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, labda ni kutoa tu elimu juu ya neno Vyuo vya Ufundi, kuna Vyuo vya Ufundi vya aina mbili, kuna Vyuo vya Ufundi ambavyo vinakuwa *credited* na *NACTE,* Baraza la Elimu la Taifa la Ufundi, kuna vyuo vya ufundi ambavyo vinakuwa credited na *VETA.*

Sasa hapa kidogo nina swali baadaye linalochanganua mambo haya na ningeomba Mheshimiwa Mbunge aweze kusubiri na kama swali la nyongeza litakuwa limejumuishwa na hili nitaweza kumjibu ipasavyo.

Na. 31

**Posho na Mishahara kwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji**

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA)** aliuliza:-

Ni sera ya Serikali kuhakikisha kuwa wenyeviti wa vijiji na vitongoji wanalipwa mishahara na posho zao na kwamba Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) alitangaza Bungeni kwamba Halmashauri ambazo hazilipi posho hizo wapeleke majina ya Halmashauri husika.

[MHE. JAMES F. MBATIA]

Je, katika Jimbo la Vunjo ni Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wangapi wamelipwa mishahara na posho hizo tangu 2010/2013?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema kwa kuanza kutoa maelezo mafupi ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wenyeviti wa vijiji na vitongoji hawalipwi mishahara isipokuwa viongozi hao hulipwa posho ya mwezi kutokana na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na ruzuku ya fidia ya vyazo vya mapato vilivyofutwa baada kuonekana kuwa ni kero.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa zinazofanywa na wenyeviti wa vijiji na vitongoji katika kusimamia shughuli zote za maendeleo kwenye maeneo yao. katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali imepeleka fedha ya fidia ya vyanzo vilivyofutwa sawa na shilingi bilioni 63.5 na halmashauri ya Wilaya ya Moshi, imepata shilingi 499,673,000 za fidia.

Halmashauri inatakiwa kupeleka katika Serikali za vijiji asilimia 20 ya fedha kama ilivyo kwa halmashuari zote nchini, matumizi ya fedha hizi ni kwamba asilimia tatu ya hizo zinatakiwa kutumika kwa ajili ya maendeleo na asilimia 17 kwa ajili ya utawala ikiwemo kulipa posho za wenyeviti wa vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2010/2013, halmashauri ya wilaya ya Moshi, imepeleka ruzuku ya fidia kwenye Serikali za vijiji kiasi cha shilingi milioni 207,485,400 ambapo sehemu ya fedha hizo zilikuwa ni kwa ajili ya kulipa posho za viongozi hao. Viwango vya posho vinavyolipwa hutofautiana kati ya halmashauri moja na nyingine kulingana na makusanyo ya mapato ya ndani na fidia inayopelekwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo ni kwamba kwa baadhi ya halmashauri kutopeleka fedha hizi katika Serikali za vijiji. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuzikumbusha tena halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba fedha hizo zinapelekwa katika vijiji na ufuatiliaji ufanyike ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa halmashauri ya Wilaya ya Moshi na hususan jimbo la Vunjo lina vijiji 84 na vitongoji 384 na mpaka sasa hivi jambo fedha hizo zinaonekana zimeenda kwenye halmashauri ya Wilaya ya Moshi, hakuna Mwenyekiti yoyote wa kijiji ameshalipwa posho hizo navyozungumza leo hapa.

Serikali inaonaje ili utekelezaji uwe ni endelevu kwa vijiji vyote nchi nzima watoe circular kwa Wakurugenzi na Wabunge wapate kopi ili ufuatiliaji uweze ukawa ni wakaribu zaidi?

La pili, kwa kuwa wenyeviti hawa wamefanya kazi kwa miaka minne sasa na wanaenda mwaka wa tano, haki zao za huko nyuma ambako hawajalipwa, Serikali inatoa tamko gani kwa halmashauri zote ili haki zao zipatikane, hususan jimbo la Vunjo ambako ndiko anakotoka muuliza swali la msingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nasikitika kusikia kwamba waheshimiwa Wenyeviti wa vijiji na vitongoji kule Moshi hawajalipwa kwa sababu kwa utaratibu ambao ofisi ya Waziri tunaona, na kwa utaratibu ambao tumeelekeza Halmashauri zetu nchi kote kupitia mapato ya ndani kwamba kila kijiji kijidhatiti katika kufanya makusanyo yake na makusanyo zile asilimia nilizozitaja yanaweza kufanyiwa matumizi, lakini lazima uripoti kwa halmashauri.

Lakini kwa vyanzo vyote ambavyo tulivifuta ambavyo sasa ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inapeleka kama ruzuku kwenye halmashauri maana yake fedha ile sasa itumike na imeenda kama ruzuku kwenye halmashauri maana yake fedha ile sasa itumike na imeenda pale kama badala ya fedha ambayo wangekusanya wao na kwa hiyo inatosha kufanya zoezi.

Kwa hiyo, ni wajibu wa kila halmashauri na wakurugenzi nchini kuhakikisha kwamba wenyeviti wote wetu wa vijiji wanalipwa fedha zao kwa wakati. Inaweza pia tunapeleka kwa robo mwaka lakini bado ndani ya miezi mitatu wenyeviti wangeweza kulipwa.

Sasa hili ya kwamba hawajalipwa, tunakuahidi kufanya ufuatiliaji wa kina, hii sasa ikiwemo na ile miaka yote ambayo wenyeviti wa maeneo haya hawajalipwa na kuwaahidi kwamba nitafanya ufuatiliaji tupate sababu kwanini wenyeviti kwa eneo lile hawajalipwa kwa miaka yote minne halafu nitakupa taarifa.

Sasa tutaandaa utaratibu wa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge ili mtusaidie kufanya ufuatiliaji kwenye halmashauri zetu kwa sababu Serikali inapeleka kwenye halmashauri na wakurugenzi nao wanapata zile fedha sasa namna ambavyo wanatumia na kwa kuwa sasa Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe wa mabaraza ya madiwani kwenye maeneo.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


Moja kati ya maswali ambayo mngepaswa kuyauliza na ambayo sasa nashauri myafanyie ufuatiliaji ni pamoja na matumizi ya fedha hizi kwa wenyeviti wa vijiji.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi kwanza mimi nasikia hata kutetemeka kusikia neno alilolisema Mheshimiwa Waziri, tumekuwa tukizunguka majimboni mimi huu mwaka wa tatu, nazunguka kila mahali mimi nadhani sasa Mheshimiwa unataka kugombanisha Wakurugenzi na wenyeviti wa vijiji kwa sababu hakuna mahali popote ambako imeandikwa Serikali inapeleka fedha yoyote katika vijiji? Kwa hiyo, naomba ieleweke vizuri ili kusudi wakurugenzi wasipate matatizo na wenyeviti wa vijiji ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, analosema Mheshimiwa Mbunge anaweza kuwa ni la ukweli kwa baadhi ya halmashauri kama Mkurugenzi hawezi kutekeleza haya ambayo nimeyaeleza. Kwa sababu vyanzo vyote ambavyo tumevizuia kwenye halmashauri kuvikusanya ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI inapeleka fedha zile kama fidia ya fedha ambayo ilitakiwa ikusanywe na halmashauri zake. Ndiyo hiyo hiyo ambayo inatakiwa igawiwe kwa asilimia hizo.

Kwa hiyo, kama ambavyo nimeahidi kwamba jambo hili sasa kama limezungumzwa kwa upana huo sasa ni wajibu wetu sasa kufanya ufuatiliaji na naahidi tutawapa taarifa Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kupata nafasi ili niweze kuuliza swali kwa kuwa wenyeviti hawa ni watu muhimu kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa posho zao aidha haziendi lakini pia kama zinaenda haziendi kwa wakati. Kumekuwepo pia na tatizo la Waheshimiwa hawa Wenyeviti wa Serikali za

Mitaa na vitongoji kutokuwa na sehemu kama ofisi ya kufanyia kazi wamekuwa wengine wanapanga lakini wamekuwa wanaomba omba sana fedha kwa ajili ya pango.

Je, Serikali inaonaje suala hili ili kuweza kuhakikisha kwamba watu hawa wanaweza kupata sehemu za kufanyia kazi ama fedha za kulipia pango ya ofisi wanazokodisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunavyo vijiji vingi nchini na katika kuboresha utendaji ilikuwa inapaswa kila kijiji kiwe na ofisi yake kwa ajili ya kufanya mawasailiano na wananchi wake kwenye maeneo yake.

Lakini tunatambua ziko ofisi ambazo kwa jitihada zake zenyewe zimejenga ofisi, lakini pia, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMi inapeleka ruzuku kwenye Halmashauri ingawa si nyingi kwa ajili ya kutosheleza vijiji vyote; lakini viko vijiji ambavyo sasa vinajenga ofisi zake ni pamoja na ofisi za Kata.

Kwa hiyo, tutaendelea na zoezi hilo la kuboresha ujenzi wa ofisi za vijiji kwenye maeneo yale ambayo yanaelekezwa zile fedha ili kuweza kutoshereza kuwa na maeneo ya kufanyia kazi maeneo haya. Kwa hiyo, wajibu wetu sasa ni kuona uwezekano wa kibajeti zaidi, ili kuongeza eneo hilo tuweze kuwezesha vijiji kuwa na eneo hilo kuwa na ofisi za kufanyia kazi.

**SPIKA:** Ahsante, hili swali la mishahara kwa wenyeviti, Mheshimiwa Waziri mukalifanyie kazi vizuri. Mkalifanyie kazi vizuri, tekinolojia ipo munaweza kupata maelezo kila Halmashauri wanafanya nini na pengine mkaleta taarifa hapa watu wakaridhika. (*Makofi*)

Tunaendelea na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Dkt. Tatus Kamana atauliza swali hilo.

Na. 32

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**MHE. DKT. TITUS MLENGEYA KAMANI** aliuliza:-

Kijiji cha Ngasamo Wilayani Busega kilipatiwa maji ya bomba kupitia mradi wa *TASAF* na Serikali iliahidi kupanua mradi huo kwenda vijiji vya Ngunga, Malili na Nyamikoma:-

(a) Je, ni lini utekelezaji wa upanuzi huo utaanza?

(b) Je, ni lini kwa uhakika wakazi wa vijiji hivyo wataanza kunufaika na huduma ya maji ya uhakika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Vijiji vya Ngasamo, Ngunga na Malili ulianza kutekelezwa mwaka 2003 kwa fedha toka *TASAF 1* kwa gharama ya shilingi 193,894,666. Huu ni mradi mkubwa unaotegemea chanzo cha maji kilichopo katika kijiji cha Ngasamo.

Kazi zilizofanyika ni pamoja na Ujenzi wa Tenki la kusambaza maji kwenye kilima kilichopo karibu na kijiji cha Ngasamo. Kuchimba mtaro na kulaza Mabomba ya maji kutoka kwenye chanzo cha maji hadi kwenye tenki juu ya mlima; ununuzi wa pampu wa pampu ya kusukuma maji na Ujenzi wa nyumba ya pampu.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU]

Mheshimiwa Spika, mradi huu haukuweza kukamilika kwa wakati kutokana na fedha zilizotolewa ma *TASAF 1* kushindwa kukidhi mahitaji yote ya mradi huu mkubwa, hivyo kusababisha mradi kusimama kwa muda wa miaka sita. Wakati wa utekelezaji wa awamu ya pili ya *TASAF,* tathimini ya kitaalamu ya mahitaji ya mradi uliofanyika mwaka 2009 ilionesha kuwa zinahitajika fedha shilingi 168,835,000 kukamilisha shughuli zote za mradi na kuwezesha vijiji vyote vitatu vilivyokuiwa vimelengwa kupata maji.

Hata hivyo, kulingana na taratibu za *TASAF 2* mradi ulipatiwa kiasi cha shilingi 53,531,500 ambapo wananchi walichangia shilingi milioni 7,500,000 pamoja na nguvu kazi kwa ajili ya kukamilisha mradi wa kuwezesha upatikanaji wa maji kwa kijiji cha Ngasamo kwa wakazi wake wapatao 3,100.

Aidha, mradi huu ulijumuisha miradi midogo midogo ndani yake ukiwemo ujenzi wa tanki la maji kijiji cha Ngunga lita 22,000 na umekamilika, ujenzi wa barabara ya Ngasamo hadi kijiji cha Nyangoka Km 2.5 umekamilika. Ufungaji wa mabomba ya kushusha na kusambaza maji kwenye vituo yaani *DP* mita 1,300 umekamilika na ujenzi wa vituo saba vya kusambaza maji *(DPs),* na vitatu vipo kijiji cha Ngasamo, viwili kijiji cha Ngunga na viwili kijiji cha Malili, ila maji bado hayajaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji vya Ngunga na Malili bado hawajanufaika na huduma ya maji ya mradi huu kwa kuwa maji bado hayajaunganishwa kwenye Vituo vya usambazaji maji *(DPs)* vilivyojengwa kwa sababu ya upungufu wa fedha. Kijiji cha Nyangoka hakikulengwa kwa mradi wa maji, ila wananchi wake walinufaika na barabara yenye urefu wa km 2.4 waliyoijenga kwa kushirikiana na *TASAF.*

Mheshimiwa Spika, muda wa utekelezaji wa mradi wa *TASAF* awamu ya pili ulikwisha, Halmashauri zote zilijulishwa na kushauriwa kukamilisha miradi ya wananchi ambayo haikuweza kukamilika kwa sababu mbalimbali kwa kutafuta vyanzo vya fedha, ikiwemo miradi ya maji ya vijiji vya Ngunga na Malili.

**MHE. DKT. TITUS MLENGEYA KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, mradi huu uliwapa matumaini makubwa sana wananchi wa vijiji vya maeneo yanayozunguka. Vilevile maji yaliyoko kwenye kile kisima ni mengi sana kwa sababu ni kisima cha asili, chenye uwezo wa kuhudumia eneo kubwa. Hata hivyo, Wilaya ya Busega ndiyo juzi juzi tu imeanza, haina vyanzo vya mapato. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri anaweza kusemaje?

Serikali haoni kuna haja ya kuuchukua tena huu mradi, kwa sababu Halmashauri hii mpya haina vyanzo vya kutekeleza mradi mkubwa wa namna hii?

Swali la pili ni kwamba, mradi huu mabomba sasa yemepasuka kwa sababu kama nilivyosema maji ni mengi na yana nguvu nyingi. Mabomba yaliyowekwa yamepasuka, lakini Wilaya ya Busega haina mratibu wa *TASAF,* mratibu anatoka Wilaya nyingine ambayo iko Mkoa mwingine tofauti na Busega. Sasa ni lini Serikali italeta mratibu wa *TASAF* katika Wilaya hii ili aweze kufuatilia mradi huu na mambomba yaliyopasuka yaweze kutengenezwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kabisa kwamba mradi huu ni muhimu na unawapa matumaini makubwa wananchi wote wa vijiji vyote vya Ngunga na Malili pamoja kama Ngasamo.

Kama nilivyoelezwa tatizo lililotokea ni la kifedha zaidi kuliko la imuhimu. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutashauriana na Wizara ya Maji, pamoja na Halmashauri ya Wilaya Busega ili kuona ya kwamba Serikali inaendeleza kazi nzuri iliyoanzwa na *TASAF* pale, kuhakikisha kwamba makusudio ya kuwapatia maji wananchi wa vijiji hivi yanafikiwa.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU]

Naujua mradi huu nimewahi kuutembelea, nilishaenda mpaka kwenye chanzo nimetembelea vijiji vyote vinavyozunguka pale mahali. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba tutashirikiana kuhahakikisha kwamba huduma iliyokusudiwa inapatikana badala ya kuuacha kama ilivyo sasa.

**SPIKA**: Mheshimiwa Chiku A. Abwao, nimekuona umesimama?

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, samahani sijakusikia vizuri. Kwa kuwa wananchi wa Isimani wana matatizo makubwa sana ya maji na kwa kuwa kuna visima vingi ambavyo vilichibwa kwa bahati mbaya havitoi maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Isimani, kuhakikisha wanapata maji yaliyo safi na salama?

**SPIKA**: Ninyi munapiga makofi mpaka hatukusikia mwishoni, umemaliziaje? Hebu simama useme tena, hatukukusikia mwishoni.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wa Isimani wanapata Maji yaliyo safi na Salama?

**SPIKA**:Jipya kweli kweli, Mheshimiwa Waziri wa nchi naomba majibu!

**WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyingeza la Mheshimiwa Chiku A. Abwao, kama ifuatavyo:-

Tatizo la maji haliko Isimani peke yake, lipo katika Halamsahauri nyingi nchini na kama tunakumbuka wakati Mbunge hili linajadili tatizo hili, tuliongeza fedha kwa ajili ya kusaidia kuongeza kiwango cha maji na tukatilia mkazo kwamba, maji haya yataenda katika maeneo ya vijijini na kazi ya kutekeleza imeshaanza na miradi mingi inatekelezwa sasa vijijini.

*Contractors* wamekwisha ajiliwa kwa ajili ya kuongeza kiwango cha maji na hiyo itahusu vilevile Wilaya ya Isimani. Hili ni suala la nchi nzima halitakuwa la Isimani peke yake. Lakini kama Isimani kuna tatizo kubwa na Mbunge wa Isimani yuko hapa, tutashirikiana naye kuona namna ya kusaidia kupunguza tatizo hilo.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia)*

**SPIKA**: Mbunge wa Isimani! (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Aaah! Mimi ni Waziri. (*Makofi/ Kicheko*)

**SPIKA**: Mbunge wa Isimani! (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, mimi nazungumza kwa niaba, mimi ni mtu wa Serikali na ndiyo mratibu wa shughuli za Serikali, nina uwezo wa kutoa majibu yoyote humu ndani. Kama hamjui!(*Vicheko*)

Kwa hiyo, kwa niaba ya mheshimiwa Waziri wa nchi, Uratibu na Mawasiliano nataka kutoa jibu la nyongeza kwa swali alilouliza dada yangu Mheshimiwa Chiku Abwao.(*Vicheko*)

Serikali inafahamu tatizo la maji Isimani, Mheshimiwa Rais mwenyewe alipotembelea mara mbili Isimani alijua jambo hilo na hivi sasa kuna mradi mkubwa wa kufufua chanzo cha maji na kurekebisha, ambacho kinatoa maji Mbigiri kwa Professor wenye thamani ya shilingi bilioni tatu.

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU]

Hivi ninavyozungumza Mbunge wa Isimani kwa kutumia vyanzo mbalimbali, ameshachimba visima 25, visima 25 vya maji na hivi sasa tunamalizia visima vingine 10. (*Makofi*)

Nia ni kuwa na kisima cha maji ya akiba katika kila kijiji cha Isimani, badala ya wananchi kuendelea kusubiri mradi ule mkubwa wa bomba, kila kijiji kitachimbiwa kisima kwa jitiada anazofanya Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Serikali. (*Makofi*)

**SPIKA**: Wala huhitaji kusema, maana yake hapa mtu anaruhusa ya kujibu. Kwa hiyo, wewe mwenyewe kama Mbunge peke yake ungeweza kujibu tu, *eeh* kwa sababu wewe ndiyo unayejua jimbo lako.

Tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naona Chiku Abwao analitaka hilo Jimbo *eeh*! (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, tunaendelea, Mheshimiwa Abdallah S. Ameir!

Na. 33

**Shamba la Uvikuta – Chamazi**

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR** aliuliza:-

Katika Wilaya ya Temeke, Jimbo la Kigamboni, Kata ya Chamazi kuna Shamba la UVUKUTA lenye eneo kubwa sana na mpaka sasa ni theluthi moja tu ya shamba hilo linatumika na eneo lililobaki ni pori kubwa linalohifadhi wanayama hatari pamoja na kuwa kimbilio la vibaka wanapofanya uhalifu maeneo mengine:-

(a) Je, Serikali inalijua hilo?

(b) Je, eneo hilo lina ukubwa wa ekari ngapi?

(c) Je, eneo hilo lilitolewa kwa madhumuni gani?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali inatambua uwepo wa Shamba Namba 2820 lenye barua ya toleo yaani *letter of Offer*, *Kumb. Na. LD*/177113/17 ya tarehe 25 Aprili, 2001 lenye ukubwa wa ekari 893 linalomilikiwa na umoja wa Vijana wa Kikristo Uzalishaji Tanzania (UVIKUTA) lililopo eneo la Chamazi katika Manispaa ya Temeke Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, shamba hili lilitolewa kwa matumizi ya makazi, kilimo na ufugaji. Kwa sasa eneo hilo lipo kwenye mchakato wa kuandaliwa matumizi bora ambayo yatajumuisha maeneo ya makazi, miradi ya elimu na mafunzo yaani *Education and Vocational Training* biashara, viwanja vya michezo na huduma za kijamii kama zahanati pamoja na viwanda na kadhalika.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba liko katika mchakato wa shamba hilo kufanyiwa hayo aliyoeleza.

Je, mchakato huo unaanza lini na utamalizika lini?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri atakuwa yuko tayari kufanya vikao na wananchi ambao wanazunguka eneo hilo ili kuelezea azima hiyo kwa ajili ya kuondoa malalamiko? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato kwamba unaanza lini na kumalizika lini, Mchakato umekwishaanza. Kwa kawaida, mmiliki wa eneo, pale ambapo ataona ameshindwa kufikia yale malengo yaliyokuwa yamepangwa awali, au mamlaka ya upangaji ikiona kwamba mmiliki wa ardhi ameshindwa kutimiza masharti yaliyomo kwenye hati au mpango wa matumizi ya ardhi, inayo mamlaka ya kuingilia na kupendekeza ardhi ile ipangiwe matumizi mbadala.

Hivyo, kwa sasa hivi tumekwishapokea maombi ya kubadilisha matumizi kutoka yale ya makazi kilimo na ufugaji pekee na kupima viwanja upya, kupanga matumizi ili kujumuisha yale ambayo nimeyataja katika jibu la swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndiyo nitakuwa tayari kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo linalohusika, pamoja na uongozi wa Mkoa na Wilaya kwenda pale kukutana na wananchi na kuzungumza juu ya mstakabali wa eneo hilo.

**SPIKA**: Nakupongeza kwa majibu mafupi. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Professor Mahamudu Msolla, atauliza swali linalofuata.

Na. 34

**Utafiti wa Madini ya Chokaa Kijiji cha Vitono – Kilolo**

**MHE. PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA** aliuliza:-

Kampuni ya *Kastan Mining Ltd.* ya Dar es salaam ilipewa leseni ya Utafiti wa Madini ya Chokaa (*Prospecting Licence No. PL* 6528/2010) ya terehe 13 Agosti, 2010 kwa kipindi cha

miezi thelathini na sita (36) ya tarehe 13 Agosti, 2010 kwa kipindi cha miezi thelathini na sita (36) katika kijiji cha Vitino, Wilayani Kilolo. Kampuni hiyo imekuwa ikichimba chokaa kwa wingi na kuisafirisha na malori kupeleka mahali kusikojulikana:-

(a) Je, utafiti huo umefikia wapi kwa sasa?

(b) Je, wananchi wa Vitono na Halmasahauri ya Kilolo kwa ujumla wananufaika na uchimbaji huo wa Chokaa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Prof*. Peter Mahamudu Msolla lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Kampuni ya *Kastan Mining Ltd.* ya Dar es salaam, ilipewa leseni ya utafutaji ya madini ya Viwandani yaani, *Prospecting Licence No*. Pl 6528/ 2010 ya tarehe 13 Agosti, 2010 kwa kipindi cha miezi 36. Leseni hiyo, yenye ukubwa wa kilometa za mraba 198.8, ilitolewa katika Wilaya ya Kilolo na uhai wake ulikoma tangu tarehe 12 Agosti, 2013. Utafutaji wa madini ndani ya leseni uliendelea na haukufikia hatua ya kuanzisha mgodi.

Aidha, baada ya uhai wa leseni hiyo, kumalizika tarehe 11 Agosti, 2013 na kwa kuwa mwenye leseni hiyo hajawasilisha maombi ya kuihuisha, eneo hilo kwa sasa liko chini ya Mamlaka ya leseni kwa muda wa miezi minne ambapo baada ya hapo itakuwa wazi kwa waombaji wengine wapya.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia, ilitoa leseni nyingine nne za uchimbaji mdogo katika eneo la Vitono za tarehe 27/

6/2011 kwa Bwana Salim Abdallah Zagar na kuna uchumbaji wa madini ya chokaa unaeoendelea katika leseni hizo. Aidha, kufuatia uchimbaji huo Serikali ilipata jumla ya dola za Marekani 977.63 ikiwa ni mrahaba, ikijumlisha na adhabu ya 25% ya ucheleweshaji wa kulipa mrahaba, ilipouza tani 896 kama mbolea ya chokaa. Kiasi hicho cha fedha kilipwa katika ofisi yetu ya madini Mbeya.

(b) Mheshimiwa Spika, manufaa ya wazi kwa kijiji na kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ni ajira kwa wananchi wa maeneo hayo. Aidha, kampuni hizi zinapaswa kushiriki katika kuchangia shughuli za kijamii katika maeneo hayo, pomoja na kulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Kilolo ambayo ni asilimia 0.3% ya mapato yatokanayo na madini wanayochimba.

**MHE. PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kufuatilia makampuni ambayo yamepewa *prospecting Licence*, kuhakikisha kwamba kweli bado wanendelea kufanya utafiti na kwamba hawachimbi madini. Ninasema hivyo kwa sababu muwekezaji huyu amechimba madini, amekuwa akisomba kwa malori mengi kwa siku, kiasi cha kuharibu hata barabara.

Je, huo bado ni utafiti tu, ama ameanza kuchimba? (*Makofi*)

Pili, manufaa kwa wananchi kwa Vitono, pamoja na Halmsahauri ya Kilolo hayajawahi kupatikana. Hajashughulika kwenye mambo ya *cooperate resiponsibility* yeyote na badala yeke amechimba kwenye mashamba ya wananchi na aliahidi kwamba angelipa fidia na mpaka leo hii hakuna mwananchi yeyote ambaye amelipwa fidia hiyo.

Je, serikali itasaidiaje ili wananchi ambao mashamba yao yamechukuliwa waweze kulipwa fidia stahiki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze kwa kuuliza maswali mazuri ambayo kwa kweli yamekuwa yana mgogoro mkubwa katika sekta hii ya uchimbaji wa Madini katika maeneo mengi na hasa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, utaratibu wa utafiti unaofanywa na Makampuni haya, na kwamba matokeo yake yanapokuwa tayari je, tunajua wakati gani kwamba sasa wanaanza kuchimba au bado wanafanya utafiti.

Uko utafiti wa aina tofauti tofauti, uko utafiti unaoweza ukaishia palepale, lakini uko utafiti ambao unaweza ukapaswa kumaliziwa au kukamilika kwa kutumia nje ya eneo lile kwa sababu ya teknolojia. Hata hivyo, Sheria inataka Wizara ikague maeneo hayo na huwa tunakagua kila baada ya muda fulani, na tunao Maafisa wa Madini katika maeneo haya.

Sasa kama imetoakea basi jambo hili likafanyika kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, basi pengine ni uzembe wa mtaalam wetu ambaye tumemweka kule, lakini naamini kwamba mambo haya yanavyotokea wakati mwingine huwa ni kwa siri au kwa kificho. Tutajitahidi kuweka msisitizo mkubwa katika kuangalia suala hili wakati wote kwa sababu ni kweli Mheshimiwa Mbunge na eneo hili mimi nilipita, yako madhara ambayo yametokea na wao

hawajapata kitu chochote na huyu bwana akafunga leseni yake na kuiachia ili tuweze kutoa kwa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, la pili, manufaa ambayo wananchi wamepata wa Kitono, ni kwamba ni hakuna, ni kweli. Jambo la kwanza kabisa ambalo nataka niliseme hapa, na ninawaomba wachimbaji wa madini wote walielewe na wananchi, kwa maana ya Serikali zote, kwa maana ya Serikali za Mitaa na za Vijiji kuelewa ni kwamba uchimbaji wa madini hauendi kiholela kama ambavyo wachimbaji wanataka.

Ni lazima huyu mchimbaji afike kwenye Halmashari, aripoti, aelekezwe anakokwenda kule kwenye Kijiji, aripoti ili waweze kukubaliana mambo fulani fulani ya msingi na uchimbaji huu hauwezi ukaanza mpaka kwa kibali cha Waziri.

Kwa hiyo, nichukiue nafasi hii kuwaomba sana, kwamba Serikali za Mitaa zinahusika katika uchimbaji wa Madini, na zinatambulika na zinatajwa kisheria kwamba ni lazima zilidhie, na washirikiane ili kuweza kuruhusu huo uchimbaji. Pia suala la fidia, ni suala la msingi sana, leseni ya uchimbaji haiwezi ukatolewa mpaka pale Waziri atakapojiridhisha kwamba fidia zimelipwa, hali ya mazingira imetizamwa, ndipo uchimbaji uweze kuendelea.

Nichukue nafasi hii kuwaomba Viongozi wetu wa Halmashauri wasiwe wanyonge, wanapoona mtu anachimba, wachukue hatua, wamwulize kama ana kibali na ikibidi wawasiliane na Wizara ili kuweza kupata uhakika wa jambo hilo.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, badala ya Wizara ya Nishati na Madini kumpa Mtafiti wa Madini leseni na baadaye aje kwenye Halmashauri, siyo bora kwamba anayeomba leseni hiyo apitie kwenye

Halmashauri ili Ardhi hiyo ijulikane kwamba haina watu katika maeneo hayo?

**SPIKA**: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi ziko haki mbili, iko *mining right* ambayo iko chini ya Ardhi, lakini pia kuna *surface right*. Kwenye Sheria ya Madini yenyewe inazungumzia *mining right* ambayo iko chini ya Ardhi, lakini haimtengi mwenye *surface right*. Halmashauri hizi zinamiliki *surface right,* lakini huweze uka *access mining right* kama hujapata *surface right.*

Hapa ndipo kuna fidia na mambo mengine. Kwa hiyo, ni ukweli kwamba mchimbaji wa Madini, hata kama ana leseni kutoka Wizarani, hataruhusiwa kuendesha uchimbaji, mpaka apate *surface right* ambayo inamilikiwa na Mamlaka zilizoko pale chini.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaomba wachimbaji, wasidharau haki ya *surface*, haki ya hapa juu ya ardhi, hii haki ina watu ambao wameipata kisheria. Ardhi ya Tanzania hakuna iliyo wazi, ardhi inamilikiwa na Mamlaka za Umma, za Vijiji, na Serikali Kuu.

Kwa hiyo, hakuna ardhi iliyo wazi, kwa hiyo, wakipata haki ya kuchimba wasidharau haki za watu wengine wanaomiliki hapa juu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo

la nyongeza. Kwa kuwa kwa sasa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kujenga Barabara nyingi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo katika Jimbo la Peramiho na Makampuni yanayojenga Barabara hizo yamekuwa yakichimba vifusi na kupata maliasili za kutengenezea Barabara hizo kutoka katika Vijiji, lakini wanavijiji wale hawafaidiki na kitu chochote badala yake wanaachiwa mashimo, makorongo makubwa bila kupata faida yoyote ile. (*Makofi*)

Je, Wizara hii haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuhesabu changarawe na kokoto na kila kitu kinachochimbwa katika maeneo ya wananchi pia ni aina mojawapo ya madini na wananchi hao wakapata fidia ama mrahaba kwa namna moja ama nyingine? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza zuri sana la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama ambalo nalo huwa ni chanzo cha migogoro mikubwa inayotokea kwenye Vijiji na Sekta hii ya uchimbaji wa Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria yetu inatambua kwamba, Mchanga, Mawe, ni Madini. Kwa hiyo, isionekane kwamba siyo Madini, na kwamba utengenezaji wa barabara au shughuli zozote zinazo *involve* uchukuaji wa rasilimali hiyo ni lazima watu wa maeneo yale wanufaike, hili liko wazi katika Sheria, lakini maendeleo ni ubia, tunahitaji barabara wenyewe, tunahitaji kupata mambo mengine wenyewe.

Barabara nazo hizi ni msingi, na fedha zinazotengeneza barabara ni fedha za Serikali, tunapoweka hivyo maana yake tunaongeza gharama ya utengenezaji barabara, itakuwa kubwa, na sijui tutapata kipi, lakini niseme ni suala la kukubaliana, tunataka kipi katika hivi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimwulize swali moja dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri unafahamu kwamba wananchi wanaopatikaka katika Wilaya ya Kasulu, kule

katika Kijiji cha Makele hivi karibuni kupitia oparesheni Kimbunga, baadhi yao Migodi yao ya chokaa ililipuliwa na moja ya sababu ambayo imepelekea ni kwa sababu Serikali imekuwa inaona kwamba wale watu ni wachimbaji haramu.

Jambo ambalo siyo kweli kwa sababu Wizara imewapa leseni, lakini wanazungushwa sana na Wizara ya Maliasili na Utalii kwenye kupewa vibali vya kuingia kwenye maeneo yale ambayo Serikali imeiita ni Hifadhi. Ningependa nipate kauli ya Serikali, ni lini *contradiction* hii ya Wizara ya Nishati na Madini ya kutoa leseni, halafu Wizara nyingine wanakuja wanawazuia tena, hii *contradiction* itaisha lini?

Mheshimiwas Spika, ni serikali moja au ni serikali mbili?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Machali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo hili la Makele ni sehemu ya Hifadhi ya Taifa, na kama nilivyosema, haki ya kuchimba Madini, ukishaipata ile haki siyo kwamba haki ya mtu anayemiliki *surface right* inapotea, taratibu zinapaswa zifuatwe, na yako maeneo ya mfano ambayo imetokea hivyo na Wizara hii ya Maliasili na Utalii ikatoa vibali, lakini taratibu lazima zifuatwe.

Siyo tu ukiwa na ile leseni, basi una *access mining* kwa urahisi, hapana, lazima uhakikishe umelipa fidia, lazima utambue haki za watu walioko wanaomiliki hapa juu. Kama kuna watu wa Mashamba, kama kuna watu wana Nyumba, ni lazima kutambua.

Mimi nadhani na nichukue nafasi hii kuwaomba sana na kuwashauri wachimbaji hawa, ambao Mheshimiwa Machali anawatetea leo kwa sababu ni wachimbaji wadogo, lakini naamini ingekuwa ni mchimbaji mkubwa asingefanya hivyo.

[WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

Kwa Kanuni na Sheria iko palepale, kwamba lazima kutambua *surface right,* na haki hii iko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, tujaribu kufuata taratibu tuone namna ya kusaidia, na sisi Wizara yetu iko tayari kusaidia pale ambapo pataonekana msaada wetu unahitajika wa sababu ndiyo tuliotoa leseni ya kuchimba.

**SPIKA**: Swali la mwisho katika hili, Mheshimiwa Telele.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mimi nilitaka kuuliza tu kama aina hii ya leseni wanapewa pia wageni au ni wazalendo tu peke yake.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Telele kama ifuatavyo:-

Ingawa siyo rahisi kujua swali alivyoliuliza, lakini zipo leseni za aina mbalimbali, ziko leseni za wachimbaji wadogo *(Primary Mining License)* ambazo zinatolewa kwa wazalendo tu na ziko zile za kati na kubwa ambazo zinatolewa *either* kwa wageni hata kwa wazalendo. Kwa hiyo, kwa leseni hizi ambazo tumesema hapa ni zile ambazo ni *Primary Mining License* ambazo zinatolewa kwa wazawa tu.

**SPIKA**: Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atauliza swali hilo.

Na. 35.

**Kampuni Zilizomaliza Muda wa Kusamehewa Kodi**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Je, ni Kampuni ngapi zimemaliza ule muda wa kusamehewa kodi na wanadaiwa kiasi gani katika benki walimokopa?

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 inatoa muda wa mpaka miaka mitano kwa ajili ya kuanzisha miradi ya uwekezaji na katika kipindi hicho, miradi hiyo hupata misamaha ya kodi kwenye vifaa vya mitaji (*capital goods)*. Toka mwaka 1997 – 2007 jumla ya makampuni 5,002 ya uwekezaji yalikamilisha ujenzi wa miradi yao na hivyo hayapatiwi misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyo katika hatua ya uanzishwaji na inayopata misamaha ya kodi kwa sasa ni ile iliyosajiliwa mwaka 2008 – 2013. Nafuu ya misamaha ya kodi inayotolewa ni ile ya forodha kwa asilimia 75 na *VAT* asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo, hivi sasa *TIC* kwa kushirkiana na *BOT* na *NBS* inafanya utafiti kwa ajili ya kupata mitaji iliyoingizwa nchini na makampuni ya uwekezaji kutoka nje *(capital inflows)* ili Serikali iweze kubaini kiasi cha mitaji kilichoingizwa kama *"equity"* na mikopo.

Aidha, sambamba na utafiti huu, pia *TIC* kwa kushirikiana na *NBS* na *UNIDO* inafanya utafiti mwingine kwa *sample* ya makampuni 500 ya ndani ili kujua kiasi cha mitaji. Matokeo ya tafiti hizi yatatolewa kwa wadau baada ya kukamilika.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, maswali mawili madogo ya nyongeza. Mwaka 2007 ambapo Waziri anasema walisamehe, misamaha ile ilifutwa, lakini bado kiwango cha misamaha ya kodi ilibaki ile ile asilimia 3.5, ni kwa sababu zipi kama makampuni 5000

yalifutwa misamaha yake, lakini bado kiwango cha misamaha ilibaki pale pale.

Swali la pili, kutokana na *survey* iliyofanywa na *Investors Motivations Survey* ya mwaka 2012 kwa nchi ya Rwanda, Tanzania na Burundi, kati ya wawekezaji 450, ni 139 tu, walisema wao kama hawakupata misamaha hawatawekeza, lakini 413 hawana tatizo bila ya misamaha wangeweza kuwekeza. Kwa nini Serikali inaendelea kutoa misamaha wakati wawekezaji walio wengi kwa kutokana na vivutio vya Tanzania wako tayari kuwekeza bila ya misamaha?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli misamaha inafutwa lakini utaona kwamba *level* imebaki pale pale, ni kwa sababu, wakati miradi mingine inamaliza misamaha ya kodi, kuna miradi mingine inaingia.

Vilevile nayo inapata hizi *exemptions*. Kwa data tu kwamba , kuanzaia mwaka 2011 *inflow, investors* ambao wamekuja na miradi yao inafikia thamani ya dola milioni 1229.4, lakini mwaka 2012 kumeingina dola 1706.9 milioni, mwaka 2003 kumeingia dola 1852.9. Utaona kwamba kwamba kuna kuwa *inflow* nayo inazidi, wakati tunaondoa, lakini wengine nao wanarudi.

Swali lake lingine, ni kweli hiyo ni *survey* iliyofanywa, lakini vilevile sisi kama Wizara ya Fedha tume *commission a study, peer tax exemption study* ambayo ina *study* maeneo ya *excemption*. Katika *study* ile utaona kwamba wawekezaji kweli wasingependa kupata *exemption*, lakini iwapo tuta *improve investment climate.* Kwa sasa *investment climate*

ya Tanzania bado iko chini, na hiyo tuna *compensate with exemption.*

Utaona kwamba wawekezaji wanakuja, wanachopenda kwanza ni *market potential* ambayo sisi kwa Tanzania tunayo, lakini ukienda kwenye mrorongo wanahitaji *roads*. Kwa Tanzania maeneo mengi *roads* zake haziko katika hali nzuri, wanahitaji *competitive labour*, Tanzania bado *labour* yetu iko katika chini *and is not that competitive*.

Kwa hiyo, wakisema kwamba hawahitaji *exemption*, lakini *provided* kwamba, mambo haya yote yamewekwa katika hali nzuri. Si kweli kwamba wanakuja *and they don't need any exemption*, lakini kama tukijaribu ku-*address issues* hizi nyingine, tuki *improve climate investment* yetu hapa Tanzania, basi naamini hata misamaha ya kodi itarudi chini, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali hii ina tatizo kubwa sana la kutoa misamaha ya kodi pasipo utaratibu na ambayo kwa kiasi kikubwa haina tija, na ushahidi wa hilo ni taarifa ya *TRA* ambayo imesema kwamba misamaha ya kodi ambayo imetolewa kwenye uagizaji wa Sukari na Mchele, haikuwa na tija kwa sababu bei ile haikushuka kama ambavyo ilitarajiwa.

Naomba kupata majibu ya Serikali, ilizingatia hoja gani kutoa misamaha ya kodi kwenye uagizaji wa Mchele na Sukari na wakati *TRA* inasisitiza kwamba hakuna tija kwa sababu *impact* yake kwenye bei haionekani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Kafulila kama ifuatavyo:-

Siwezi kukubaliana naye kwamba *TRA* wamezungumza kwamba hiyo misamaha haina tija, kwa sababu wakati misamaha ya Mchele na Sukari ilipokuwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



ikitolewa, Tanzania tulikuwa tume-*face high food inflation rates,* kulikuwa tu hiyo ndiyo sababu ambayo imeingia kwa ajili ya kutoa hizo *exceptions*. Inawezekana sehemu nyingine hakukuwa na ile *impact* kwa ajili ya *inflow*, Dar es Salaam tumeona na sasa hivi tunajua kwamba *food inflation* iko chini kwa sababu bei za Sukari pamoja na Mchele zimeendelea kuwa *stable,* lakini kwa sehemu nyingine kwa sababu tu ya ubovu wa *infrastructure* kweli ule msamaha wa Sukari na Chakula ulipoingia haujaweza kufika sehemu nyingine kutokana na ubovu tu wa *infrastructures* zilizopo.

Hiyo misamaha ya Mchele na Sukari ilipotolewa kulikuwa kuna sababu muhimu na maalum kwa wananchi wa Taifa hili.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, kwamba Serikali imekili kwamba inatoa *incentives* kwa makampuni ya nje kuja kuwekeza hapa. Kwa kuwa Serikali inapoteza kwa kutoa zile *incentives* ambao wao wange-*claim* kama ni *taxes*.

Je, Serikali inaweka kama hii ni uwekezaji kwa hawa wawekezaji wanaokuja kama sehemu ya uwekezaji wao Serikali ni kutoa zile *incentives* na *exemptions* kwa kampuni ambazo zinakuja kuwekeza. Kwa nini sasa ibakie kuwa ni sehemu ya uwekezaji peke yake wakati Serikali imeshatoa sehemu yake ya kodi kwenye kuwekeza huko?

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Uwekezaji na Uwezeshaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru na kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri na kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea, misamaha kwa ajili ya mitaji au uwekezaji, hakuna kodi ambayo tayari imeshalipwa, ila tunatoa *incentives* kwa wale waje.

Pili, mitaji inashindaniwa nchi zote siyo Tanzania tu. Kwa hivyo, wale wenye mitaji, wanapotaka kuwekeza wanaona ni wapi ambapo mazingira ni bora zaidi, ikiwemo na hii misamaha ya kodi, lakini tusingependelea sana kutoa misamaha wakati ambapo si lazima.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Watanzania waone kwamba bila ya uwekezaji hakuna maendeleo. (*Makofi*)

Misamaha haitolewi kwa makampuni ya nje tu, inatolewa kwa makampuni ya ndani vilevile, na kama tunakubali hivyo, naomba niwaonyeshe kwamba uzoefu umeonyesha, kila tunapofuta misamaha hiyo ya kuvutia, siyo ya kuondoa kodi ambayo ipo, ya kuvutia, uwekezaji unatelemka na takwimu zipo, na tutawapeni.

Ninaomba Watanzania wapende wawekezaji kwa sababu ya kuendeleza maendeleo ya nchi yetu na ukuaji wa uchumi.

Na. 36

**Matumizi ya Fedha za Kigeni Nchini**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Kumekuwepo na matumizi makubwa ya fehda za kigeni hususan Dola za Marekani katika kununua bidhaa na huduma mbalimbali katika masoko hapa nchini.

(a) Je, kwa kufanya hivyo kuna athari gani katika uchumi wa nchi yetu?

(b) Kama kuna athari. Je, Serikali imechukua hatua gani katika kurekebisha tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ni ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, lenye vipengele viwili kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, endapo matumizi ya fedha za kigeni yatakithiri yanaweza kusababisha athari mbalimbali zikiwemo kupungu ufanisi wa sera za fedha, kupunguza uwezo wa Benki Kuu kutimiza wajibu wake kama mkopeshaji wa mwisho katika uchumi, yaani *lender of last resolt,* na kuwa kero endapo watu watalazimika kufanya malipo kwa njia za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha matumizi ya Dola katika uchumi wetu bado hatujafikia mahala pa kuweza kuwa na madhara ambayo tumeyataja. Uwiano kati ya amana za fedha za kigeni na ujazo wa fedha, ambapo uliwahi kupanda hadi kufukia asilimia 34 mwaka 2003 kwa sasa umeshuka hadi kufikia asilimia 27.2 mwezi Juni 2013.

Aidha kiwango cha amana za fedha za kigeni ambacho kinazidi rasilimali za fedha za kigeni za Mabenki kilikuwa asilimia 23 tu ya hazina ya fedha za kigeni inayotunzwa na Benki Kuu, hivyo tatizo la Benki Kuu kushindwa kutekeleza wajibu wake wa mkopeshaji wa Mwisho bado halijaweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi agosti 2007 Serikali ilitoa tamko rasmi kuhusu matumizi ya fedha za kigeni katika kulipia bidhaa na huduma katika soko la ndani. Katika tamko hilo Serikali iliagiza kuwa mkazi yeyote wa Tanzania asilazimishwe kulipia bidhaa au huduma yeyote hapa nchini kwa fedha za kigeni isipokuwa tu mtu akiamua kwa hiari yake mwenyewe kulipia kwa kutumie fedha ya kigeni. Aidha

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA]
Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 sehemu ya 3 kipengele cha 26 nayo imeweka wazi kuwa Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa malipo ya bidhaa na huduma nchini.

Mheshimiwa Spika, sheria ya usimamizi wa fedha za kigeni ya mwaka 1992 na kanuni zake za mwaka 1998 zinatamka wazi kwamba Watanzania wanaruhusiwa kupokea, kumiliki na kutumia fedha za kigeni kwa shughuli zao za kiuchumi hapa nchini.

Aidha baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii, akiba ya fedha za kigeni inayotunzwa na Benki kuu iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 228.3 mwaka 1993 sawa na asilimia 6 ya pato la taifa hadi kufikia Dola za Kimarekani Milioni 4,069 ambayo ni sawa na asilimia 14 ya pato la Taifa kwa mwaka 2012.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 imeweka wazi kuwa Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halili kwa malipo ya bidhaa na huduma hapa nchini, na kwa kuwa Serikali ilitoa tamko mwaka 2007 kwamba Mtanzania asilazimishwe kulipa huduma hizo kwa fedha za kigeni, na kwa tamko hilo Serikali imetoa mwanya unaokinzana na sheria.

Je Serikali kwa kuweka matamko laini kiasi hicho kutaifanya *exchange rate* ya Dola kuwa kubwa dhidi ya Shilingi na ukizingatia *demand motive* ya fedha hizo mbili yaani Shilingi na Dola?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imeacha hali iwe ilivyo, na baadhi ya bidhaa na huduma kupatikana kwa *rate* ya Dola jambo ambalo linafanya gharama ya bidhaa na huduma kuwa kubwa, nini kauli ya Serikali?

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA]

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Pareso kama ifuatavyo.

Wakati tunatoa tamko hilo tuliweka wazi kwamba kweli mwananchi asilazimishwe, asilazimiswe kutumia pesa ya kigeni hususan Dola katika kupata huduma na bidhaa. *At the same time* tunamtaka mwananchi huyo huyo anaweza kutumia fedha hiyo ya kigeni kwa shughuli zake za kiuchumi. Kwa hiyo hayo ni maeneo mawili tofauti. Ikiwa mtu labda hana shughuli zake za kiuchumi, anataka kununua bidhaa kama ni *capita* kwa ajili ya shughuli zake za uchumi na bidhaa hiyo haipatikani labda isipokuwa kwa fedha nyingine ya kigeni basi hapo anaruhusiwa. Lengo ni kuweza tu kumrahisishia mwananchi kuweza ku-*invest* na kuweza vile vile kutoa *investment* kwa kutumia fedha ya kigeni. Kwa hivyo, wakati tuna-*control* matumizi haya kiholela *at the same time* tunampa mwananchi fursa ya kuweza kujishajiisha kiuchumi kwa kupata bidhaa kwa njia hiyo hiyo ya kigeni. Kwa hivyo kumekuwa hakuna *contradictory.*

Swala la pili kwamba kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kumekuwa hakuna athari mpaka sasa hivi. Ili athari ya kiuchumi itokee basi, *level* ya fedha ya ndani, fedha yako ya *local currency* pamoja na fedha ya kigeni iwe asilimia 50 hapo ndipo uchumi utaweza kuwa *distorted*.

Lakini sasa hivi kwa sababu ya *control measures* ambazo Benki Kuu ya Tanzania imeweza kuzichukua kwa Kuruhusu, lakini *at the same time* kwa ku-*control* matumizi haya tumeweze ku-*stabilize* na sasa tumeshuka asilimia 27 tu ya fedha za kigeni katika mzunguko huu wa kiuchumi. Kwa hivyo naomba tu mkumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi hiyo athari haijaweza kuathiri sana mzunguko wetu wa fedha hapa nchini.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matumizi makubwa ya Dola, hali ya pesa ya Tanzania imeimarika dhidi ya Dola. Je, ni sababu zipi mahsusi ambazo zimesababisha kuimarika kwa Shilingi hii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa fedha naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kadege kama ifuatavyo.

Sababu ziko nyingi, kwanza tukiangalia sera za fedha ambazo tunazi-*implement* hapa nchini zimesababisha fedha yetu iweze ku-*stabilize*. Lakini kuna *measures* za kiuchumi ambazo zimechukuliwa, kwamba sasa hivi tunajitahidi *at least* kuweza kuzalisha.

Sasa kwa sababu bidhaa nyingi zinapatikana ndani kwa hivyo ile *motion* ya kununua Dola, *demand* ya kununua Dola imekuwa imeshuka kwa sababu bidhaa nyingi wanaweza kuzipata humu ndani.

Kwa hivyo, sababu nyingi Mheshimiwa Spika tunaweza tukachukua muda mrefu sana kuanza kuzielezea, lakini kiufupi tu kwamba sera zetu za fedha pamoja na sera za matumizi pamoja na sera za kiuchumi ambazo tumeweza kuzi-*implement* zimesababisha kwa njia moja ama nyingine kuweza ku-*stabilize* Shilingi yetu *against* Doa. Ahsante sana.

No. 37

**Utaratibu wa Kuwawezesha Vijana wenye Ulemavu Kujiunga na VETA**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Serikali imedhamiria kujenga Vyuo vya Ufundi *(VETA)* kwenye kila Wilaya nchini ili kuwawezesha vijana kupata mafunzo ya fani mbali mbali ya kuwawezesha kujiajiri.

Je, kuna utaratibu gani mahususi umewekwa ili kuwawezesha vijana wenye ulemavu kujiunga?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, katika kipengele cha tatu kinazungumzia utoaji wa elimu na upatikanaji wa nafasi kwa makundi maalum kama vile walemavu, yatima na watoto wa mitaani. Hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa kila mtoto kuwa na haki ya kupata elimu bila ya ubaguzi wowote. Kwa msingi huo huo vijana wenye ulemavu wanaoomba nafasi za kujiunga na vyuo vya ufunsi stadi huchaguliwa bila ubaguzi.

Matangazo ya kuomba nafasi za kujiunga na vyuo vya ufundi stadi hutolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja na mbao za matangazo. Hivyo, vijana wanaoomba nafasi za kujiunga na vyuo vya ufundi stadi hujaza *form* hizo ambazo zina kipengele cha kuainisha aina ya ulemavu ili kuweza kupata huduma kutokana na aina ya ulemavu walio nao.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Januari 2009 hadi Desemba, 2012 vijana wapatao 578 wakiwemo wavulana 345 na wasichana 233, wenye aina mbalimbali za ulemavu walihitimu mafunzo ya ufundi stadi katika fani mbalimbali hapa nchini.

Aidha, kwa kutambua mahitaji maalum ya walemavu, vyuo vya ufundi stadi vimeweka miundombinu rafiki kwa walemavu a wa aina zote ili kuwawezesha kujifunza kwa urahisi. Hivyo, natoa rai kwa wazazi na walezi wote wenye vijana wenye ulemavu kuomba nafasi za kujiunga na vyuo vya ufundi stadi pale matangazo ya kuomba nafasi hizo yanapotolewa.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Serikali, nikiamini kwamba kweli hivi vitu ni kweli kwa baadhi ya vyuo lakini vyuo vingine bado hawajarekebisha masuala hayo, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa wazazi walio wengi wenye vijana hao wenye ulemavu, wao kiuchumi hali zao zinakuwa hali dhoofu, masikini kutokana na kuwa na shughuli ya hawa watoto kuwaangalia. Serikali inasemaje kuona uwezekano wa kuwalipia gharama za mafunzo haya vijana hawa ambao wanaomba wenye ulemavu kwenye hivyo vyuo vya *VETA?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa ELimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Margareth Mkanga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, anachosema hapa Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba kama nilivyosema kwamba kuna yatima, kuna walemavu na wengine wasiojiweza.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda kwenye vyuo vya *VETA* nchini pote, ada ya kulipa mavunzo hayo ni Shilingi laki moja na ishirini (120,000/=) tu. Hapa sisi tulikuwa tumeweka sera hii kwa sababu ya kuhakikisha kwamba vijana wengi wanaokosa elimu ya sekondari na hata wale wanaopata elimu ya sekondari wakitaka kwenda kujifunza ufundi waende wakasome mafunzo hayo; kwa sababu gharama za kuwalipia waalimu na hata mchakato wa kupata karakana

na mashine zile zinazoendesha vyuo ni ghali sana, lakini ada hii ni ndogo sana.

Lakini wazo la Mheshimiwa Mbunge bado ni wazo zuri sana tutalifanyia kazi namna ya kupunguza ada kwa vijana hawa walemavu. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa suala la walemavu ni pana sana, naona Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu kwa walemavu sijui wa aina gani; lakini kuna walemavu ambao ni viziwi, mabubu, wengine wana mtindio kama wa ubongo lakini wanaweza kwenda shule. Kwa kuchukulia kwa mfano Wilaya ya Kilombero kuna walemavu wasiopungua 400, hawa ambao wako mitaani, na hakuna chuo chochote katika mkoa wa Morogoro ama Wilaya ya Kilombero, ambacho kinasaidia hawa walemavu kwa ajili ya kupata ufundi ili wajitegemee maisha yao.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuweka Kitengo cha wanafunzi wenye ulemavu katika chuo cha Maendeleo ya Wilaya ya Kilombero ili watoto hao wapate elimu ya Ufundi na Kujitegemea kimaisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Kiwanga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, aina za walemavu, labda siku-*mention* kwenye swali langu la msingi, lakini ni aina ya walemavu wote ambao wanapenda kwenda kusoma vyuo vya ufundi.

Ndiyo maana nimesema kuna *form* ambazo huwa zinatoka kila mwaka mwezi wa nane, kuomba kwenda kusoma mafunzo haya ya ufundi. Siyo suala tu la kuweka chuo

pale Kilombero lakini vyuo vya *VETA* kama nilivyosema vipo kila Mkoa; hata pale Morogoro fani hizi zinatolewa.

Kwa hiyo nilikuwa naomba wale vijana wa Kilombero waombe tu, na wakienda pale chuo cha *VETA* Morogoro, ama Dakawa pale watakuta kuna form kabisa, na hapa nimekuja nayo form maalum, na mheshimiwa tunaweza tukawasiliana hata nikakuchapia, bado ukapeleka kule Kilombero ukawapa vijana wanaotaka kwenda kujifunza haya mafunzo ya *VETA.*

Suala hili ni kwa nchi nzima wala hakuna upendeleo. Wapo walemavu wa ngozi , albino wanachukua *form* na wanasoma, wapo blind, wale wasioona kabisa na wapo wale *deaf* wasiosikia, lakini vile vile kuna wale mchanganyiko ambao tunawaita *blind-deaf* yaani wasioona na kusikia, na wale vile vile walemavu wa viongo. Wote hawa ni walemavu ambao nimesema wako 578, tayari kwa *trend* ya miaka mitatu wamemaliza vyuo vya ualimu.

Kwa hiyo, hakuna upendeleo wowote. Kama nilivyosema hata kwa Waheshimiwa Wabunge wengine, kama wapo majimboni basi tuwasiliane na mimi niweze kuwapa *form* waweze kujaza. Pale kwenye *form* wamesema kwamba chagua chuo unachotaka kwenda. Kwa hiyo siyo lazima wawe wanasoma Kilombero, anaweza akatoka Kilombero anaenda Dar es Salaam, akatoka Kilombero akaenda Mbeya.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa ni kilio cha Wana Longido wanalia kwa muda mrefu wanalia kwamba wanahitaji Chuo cha *VETA,* Waziri akatuambia tutenge eneo na tumekwishatenga eneo kwa muda mrefu sana.

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo Cha *VETA* katika Wilaya ya Longido ili vijana wa aina zote wanaotaka kujiunga na

*VETA* waende kusoma huko kuliko kuzunguka kulinda nyumba za watu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama tunavyoendelea kuahidi kuanzia mwaka 2011, 2012 hata mwaka huu majibu ni yale yale kwamba katika ilani ya Chama cha Mapinduzi tumedhamiria kwamba tutajenga vyuo vya *VETA* kila Wilaya.

Mpango huo ndivyo unavyoendelea na kama ninavyosema kila siku kwamba tumeshsaanza, Chuo cha Makete kimeshamalizika na Wanafunzi wameshaanza kusoma pale, na Mheshimiwa Rais wiki iliyopita alikuwa kule na amekizindua Chuo cha Makete na mambo yanaenda vizuri. Baada ya hapo tunahami kwenye vile vyuo vingine vitano vya wilaya; Ludewa, Kilindi, Ukerewe, Chunya na Namtumbo. Baada ya hapo tutafuata Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kuona kwamba mlolongo wa kila mwaka vyuo vinne vinne ama vitano ni mlolongo mrefu sana, na tunaweza tukafika mpaka mwaka 2020 hapa tusimalize Wilaya zote, tuliamua kwamba popote pale penye Chuo cha Maendeleo ya Jamii *(FDCs)*tuanze kutoa mafunzo ya *VETA.*

Kwa hiyo kwa mwaka wa jana tumebadilisha ama tumeweka mafunzo ya vyuo vya ufundi vya *VETA* kwenye vyuo 25, ambavyo kwa sababu sikujua ungeuliza ningeweza kuja kusoma hapa, kwa hiyo tumebakiza vyuo 30 ambapo

ndiyo *trend* kwa mwaka huu kwamba tutavibadilisha tuanze kuingiza mafunzo ya *VETA.*

Kwa upande wa Longido kule hakuna chuo chochote kwa *FDCs* wala *VETA.* Kwa hiyo Longido iko kwenye kati ya Wilaya 28 ambazo baada ya kupata fedha tumeshaandika maandiko mbalimbali, tukishapata fedha tu tayari Wilaya ya Longido iko kwenye mpango wa kujengewa Chuo cha *VETA.*

No. 38

**Vyuo vya VETA Kutoa Mafunzo kwa Madereva wa Matrekta**

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER** aliuliza:-

Pamoja na Serikali kujenga Vyuo vingi vya *VETA* nchini lakini bado kuna uhaba mkubwa wa Madereva wa matrekta.

(a) Je, kwa nini Vyuo vya *VETA* visitumike kutoa taaluma ya Udereva wa Matrekta na jinsi ya kutumia vyombo hivyo?

(b) Je, kwa nini Vyuo hivyo pia visitoe elimu ya jinsi ya kuvifanyia matengenezo vyombo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulsalaam S. Amer, Mbunge wa Mikumi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sera ya Kilimo, Serikali imekipa kilimo umuhimu wa pekee kwa kutenga Vyuo vitano (5) nchini vya Ufundi Stadi, chini wa usimamizi wa *VETA*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kwa lengo la kutoa mafunzo ya udereva wa Matrekta na Stadi za kilimo kwa wanaohitaji.

Vyuo vinavyotoa mafunzo hayo ni Chuo cha *VETA,* Kihonda na Dakawa kwa pamoja viko mkoa wa Morogoro, Chuo cha *VETA* Mpanda mkoani Katavi, Chuo cha *VETA* Oljoro mkoani Arusha na Chuo cha *VETA* Manyara kilichopo mkoa wa Manyara. Mafunzo yanayotolewa yanahusisha udereva wa matrekta na jinsi ya kutumia matrekta hayo, lakini vile vile na jinsi ya kuvifanyia matengenezo vifaa hivyo.

Jumla ya vijana waliohitimu mafunzo hayo kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka wa jana 2012, kwa kozi ya udereva wa matrekta kwa muda mrefu ni vijana 252 na kozi ya udereva wa matrekta muda mfupi ni 85.

Aidha, jumla ya wanachuo wanaoendelea na mafunzo kwa mwaka huu kwa kozi ndefu ya udereva wa matrekta ni vijana 158 na mafunzo ya kozi ya muda mfupi ni vijana 14.

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama kubwa ya kuendesha mafunzo hayo, Serikali ilitenga vyuo vitano tu ili kuweza kutoa mafunzo kwa ufanisi zaidi. Serikali itaendelea kuviimarisha vyuo hivyo kwa ununuzi wa matrekta na kuongeza wataalam. Hivyo, natoa rai kwa wananjamii wenye kuhitaji kupata taaluma hiyo na ujuzi katika vyuo hivyo wapeleke maombi yao katika vyuo vinavyotajwa kwani hata nafasi za mafunzo bado ni nyingi kuliko wanaoomba.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya kuongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, sasa hivi mahitaji ya Matrekta yameongezeka nchini. Kama Waziri alivyosema ameruhusu

Vyuo vitano (5) kutoa mafunzo hayo, ninaona haiwezi kutekeleza kauli mbiu ya kilimo kwanza. Mahitaji ya Matrekta na Madereva wa hayo na Matrekta ni mengi.

Je, kwa nini, Serikali isione huu ni wakati muafaka wa kuruhusu vyuo vyote kutoa mafunzo hayo ya Udereva wa Trekta nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukitaka kuongeza ajira kwa vijana wetu vijijini, na kupunguza ongezeko la vijana kwa ajili ya kutafuta kazi za ajira.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kuruhusu kupunguza gharama ya mafunzo ya Trekta au kutoa kabisa ada kwa ajili ya kuwapa mafunzo ya Udereva wa Matrekta vijana wetu waliopo vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Ameir, Mbunge wa Mikumi, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kuhusu idadi ya vijana wanaoomba kujiunga na *VETA* kwa kuja kuchukua fani hii ya Udereva wa Matrekta. Ninachoweza kusema hapa labda sisi Wabunge tukahamasishe huko kwenye Majimbo yetu ili vijana hawa wajitokeze.

Lakini ukweli ni kwamba baada ya kuona kwamba kwanza gharama ya kuendesha yale Matrekta na kununua, maana yake ili kuendeshe hii kozi, ya *Agro Mechanics,* upate Matrekta pamoja na vile vyombo vyake na vifaa vyake.

Ni gharama ya shilingi milioni 193. Kwa hiyo tuliamua kama Serikali kutenga vyuo hivi vitano kwa ajili ya kuendeshea mafunzo hayo. Lakini mpaka hivi ninavyosema vijana wanaojiunga ni wachache kuliko vyuo. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kama mtahamasisha vijana waje

wasome kozi hii bado tunaweza tukaongeza na kupanua kwenye vyuo vingine.

Swali la pili, kuhusu kupunguza gharama za mafunzo. Kama nilivyosema hata kwenye jibu la swali la Mheshimiwa Magareth Agnes Mkanga. Mafunzo ya vyuo vya *VETA* yanatolewa kwa ada ndogo sana. Tena hata ukimchukua mtoto wa Sekondari anayesoma miaka minne, na ukimchukua na kijana wa *VETA* anayekwenda kujifunza ili ajiajiri, unakuta hapa kwa mwaka kijana analipa shilingi 120,000/= tu. Lakini chakula anapata pale na ada ya masomo.

Kwa hiyo, ni ada ndogo sana Mheshimiwa Mbunge. Nilikuwa ninaomba kwa hili tukubaliane na hali halisi kwamba shilingi 120,000/= kwa mwaka mtoto anapata chakula pale, maji, umeme na kulipa mishahara na gharama nyingine za Mafunzo, na kama nilivyosema vyombo hivi bado gharama hii ni ndogo sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, Ufundi bila ya vitendo ni kazi bure, yaani *practicals.* Kumekuwa kuna malalamiko makubwa sana kwamba Wanafunzi wanaosoma katika vyuo hivi vya ufundi, hawapati fedha kwa ajili ya kufanya *practicals.* Matokeo yake wanamaliza bila kuwa na ufundi stahili na hii inatokana na kwamba tengeo, au ruzuku inayopelekwa katika Vyuo vya *VETA,* ni ndogo sana, ukilinganisha na ile asilimia inayotakiwa kwenda.

Je, nilitaka kujua kutoka Wizarani. Ni lini wataongeza fedha katika vyuo hivi ili wanafunzi waweze kumaliza wakiwa na ufundi wa uhakika na waweze kuajiriwa sehemu zozote zile wanazokwenda?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UNFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Susan A. Lyimo, ni Waziri Kivuli wa Wizara yetu.

Kwa hiyo, nisingelipenda swali hili nimjibu kinamna ambavyo sintakuwa na ufahamu nalo sana. Lakini ni swali zuri. Mimi nilikuwa ninaomba kwa sababu sijawahi kupata malalamiko yoyote kutoka kwa vijana wakilalamika kwamba hatupati fedha kwa ajili ya *practical* kwenye vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa ninaomba aliweke liwe swali la msingi ili niweze kulijibu kwa ufasaha zaidi.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga Chuo chenye hadhi sana cha *VETA* katika Jiji la Arusha. Lakini miundombinu kufika kwenye Chuo hicho, hasa barabara wakati wa masika, imekuwa inaleta shida sana hata walimu kutokufika kwa wakati,, ama wakati mwingine kutokufika chuoni kabisa. Lakini vile vile kuna tatizo kubwa la maji katika chuo kile na wamechimba visima mara mbili, ninafikiri bila kupata maji ya kutosha.

Je, Serikali ina mpango gani kwenye chuo hicho kizuri sana, ili kiweze kuwa na hadhi ya wanafunzi kusoma bila ya matatizo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Arusha Mjini Ndugu yetu Lema kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, swali hili liko *very specific,* kwamba linagusa miundombinu ya chuo husika cha pale Arusha Mjini. Mimi ninaomba nifanye mawasiliano na Mamlaka husika ili nipate majibu kamili ya swali hili na tuweze kujua kwamba miundombinu na mambo mengine kama alivyosema ya maji, halafu tuweze kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge nitampatia majibu yaliyokamilika.

[SPIKA]

**SPIKA:** Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa Maswali umekwisha. Mmeona tume *relax* katika maswali ya Nyongeza kwa sababu tulikuwa hatuna Maswali ya Waziri Mkuu, lakini siyo kwamba hiyo ndiyo kawaida. Kawaida uliza maswali mafupi ili tuweze kupata nafasi kwa wachangiaji wengi. Ninashukuru Mawaziri wanaendelea kujibu maswali yao kwa kifupi na hiyo inatusaidia kuongeza muda wa kujadili. Kwa hiyo, ninawaomba muendelee na utaratibu huo.

Waheshimiwa Wabunge ninapenda kuchukua fursa hii kuwatambua Wageni waliopo. Bahati mbaya waliokaa kwenye *Speakers Gallery* sijapata majina yao. *I am sure* ni wageni wetu, *but I did not have the name, so I will do it in the afternoon.*

Tunao Wanafunzi 40 na Walimu wanne (4) kutoka Shule ya Sekondari ya Kiwanja cha Ndege Dodoma. Wanafunzi wa Shule ya Sekodnari wako wapi ninawaomba wasimame.

Ahsanteni sana. Karibuni sana. Tunao Wanamichezo 24 kutoka Halmashauri ya Mji Mpanda Mkoa wa Katavi. Wakiongozwa na Ndugu Bahati Mwaikafu. Ninawaomba msimame hapo mlipo.

Wanamichezo ahsanteni. Tunao viongozi 14 wa Timu ya Mchezo wa *Pull Table* Tanzania ambao ni washindi wa tatu (3) barani Afrika, wakiongozwa na Fred Mushi. Ninawaomba hao wanamichezo wasimame hapo walipo.

Wanamichezo hao kama mlivyowaona, wameambata na na viongozi wao yupo, Mheshimiwa Fred Mushi – Makamu Mwenyekiti. Wengine mkae ili viongozi waliosimama tuweze kuwaona. Yuko Ndugu Patrick Nyagusi, mshindi wa Afrika. Hongera sana. Ndugu Patrick kama mlivyoomuona ndiye mshindi wa Afrika katika mchezo ya *Pull Table.* Hongera sana Bwana Patrick. Tunao wageni watatu

ambao ni Wanafunzi kutoka katika Chuo Kikuu cha *St. John's.* Wako wapi hao wanafunzi wa *St. John's.* karibuni sana. *(Makofi)*

Ninao wageni niliokuwa ninasema sijapata majina ya. Nimeyapata, yuko Balozi wa Norway hapa nchini Mheshimiwa Ingunn Klepsvick. Karibu Mheshimiwa Balozi, *welcome to* Tanzania, yuko na msaidizi wake Bi. Elizabeth Schwabe-Hansen, *welcome. I am sure I going to see you in the afternoon. Thank you very much.* Tunao wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Ahsanteni sana na wageni wengine ambao hatukuwataja pia wanakaribishwa.

Waheshimwia Wabunge, Mwenyekiti, wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii saa tano (5.00) kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Lakini wanaomba kabla ya Saa Saba. Wanatakiwa wamuarifu Spika, kwa nini wanaomba kukutana muda huo na wapewe ruhusa. Mikutano yote inatakiwa ifanyike saa saba. Kama unabadilisha muda unatakiwa mumuarifu Spika. Kwa hiyo ninaagiza Kamati hii nayo ikutane saa saba.

Halafu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshmiwa Deo Filikunjombe anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kuwa leo mchana saa saba na robo (07.15) watakuwa na kikao katika ukumbi nambari 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kunako majira ya saa saba mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa C. Mheshimiwa Pindi H. Chana – Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, ameniomba

niwatangazie wajumbe wa Kamati yake ya kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Msekwa D.

Halafu Mkurugenzi wa Mambo ya Bunge ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, nafikiri Spika, mwenyewe kuwa tutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi leo baada ya kipindi hiki cha maswali. Yaani Kamati ya Uongozi ile ya Bunge tutakuwa na kikao sasa hivi baada ya kumaliza kipindi cha Maswali.

Waheshimiwa Wabunge kama tulivyoahidi jana, kulikuwa kuna hoja mbili za Waheshimiwa Wabunge. Hoja ya Mheshimiwa Said J. Nkumba na Mheshimiwa Lugola, kwa hiyo ndiyo maana ninaomba Kamati ya Uongozi twende tukutane kule tukaweza kuona namna nzuri ya kuendesha shughuli nzima.

Kwa hiyo, kwa sababu hiyo nitamwomba Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Zungu, aweze kuendelea na shughuli inayofuata baada ya kuingia kwenye kipindi kingine. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Kwa Mwaka 2014/2015

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ninaomba muwe *brief.* Kwa sababu kama mnavyoona muda umetutupa mkono.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 39 (i), ambayo ninaomba niisome. “Waziri anaweza kuulizwa

Maswali kuhusu masuala yoyote ya Umma, au jambo lingine lolote, ambalo linasimamiwa na ofisi yake.

Vile vile Mbunge yeyote anaweza kuulizwa Mawali kuhusu mambo yoyote anayohusika nayo, kutokana na kuteuliwa na Bunge kushughulikia mambo hayo."

Mheshimiwa Spika, mapema wakati wa kipindi cha Maswali, wakati majibu yanatolewa kwa Swali Nambari 32, Swali hili lilielekezwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Stephen Wasira akatoa majibu ya swali hili. Lakini baada ya kutoa majibu. Mheshimiwa Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge akasimama, kuongeza majibu ya Serikali na ilikuwa ni haki kusimama kwa sehemu ya kwanza ya Kanuni, kwamba Waziri mwingine awaweza kutoa nyongeza ya majibu.

Lakini wakati akitoa majibu hayo akawa anatoa majibu akizungumzia kama Mbunge, akisema Mbunge, Mbunge, Mbunge, akirudia, katika jambo ambalo swali la mwuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Chiku Abwao, lilihusu Jimbo ambalo ni la Waziri mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, alifanya hivyo, na alipokuwa akiendelea na alipomaliza ikaonekana kama vile ni sahihi kujibu kama Mbunge, lakini Kanuni ya Wabunge wengine kujibu maswali inahusu (i) Wabunge walioulizwa, yeye kama Mbunge hakuulizwa swali kuhusu lile swali lililokuwa likiulizwa. Lakini pili, inahusu Wabunge walioteuliwa na Bunge kwa ajili ya kazi maalum, yeye hakuteuliwa na Bunge kwa ajili ya kazi aliyokuwa akiifanya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile kilichotokea leo ni ushahidi wa namna ambavyo mchanganyiko wa vyeo kati ya Uwaziri na Ubunge unathari katika usimamizi wa Serikali. Ninaomba mwongozo wako ili jambo hili lisijitokeze tena. Waziri atakiwa kuepuka kutumia nafasi yake ya Uwaziri kujibu masuala ya Jimboni kwake kama ambavyo alivyofanya.

[MHE. JOHN J. MNYIKA]

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mpaka mtakapobadilisha Katiba. Kilichotokea ni sahihi.

*(Hapa Mheshimiwa John J. Mnyika Alisimama)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ninakuomba tafadhali ukae. Mheshimiwa John J. Mnyika ninakuomba ukae. Kwa nini unakuwa mbishi? Kanuni umeishika mwenye unatakiwa kunisikiliza na mimi pia.

Alichokisema Waziri, Mbunge yeyote anayo haki ya kujibu kitu kinachomhusu. Soma Kanuni nyingine. Anayo kanuni.

Tusibishane Kanuni zetu ziko wazi, hata wewe ungeliguswa kwenye eneo lako kama unahusika, utasimama na mimi nitakuruhusu, *power of replying* ni wajibu wako. *Power of replying* ni haki ya Mbunge yeyote hapa atakayeguswa.

**MBUNGE FULANI:** Hata kama ni Waziri?

**SPIKA:** Waziri ni Mbunge, hiyo ya kwanza. Tuendelee na Mheshimiwa Mbunge mwingine. Mheshimiwa David Kafulila, uwe *brief.*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(vii) kufuatia tukio ambalo limejitokeza wakati Maswali yakijibwa. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, aliuliza kuhusiana na tatizo la misamaha ya kodi.

Ukanipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza ambapo nilitaka majibu ya Serikali kufuatia taarifa ya *TRA,* inayoonyesha kwamba misamaha inayotolewa kwenye sukari na mchele haina tija kwa walaji, ambao kimsingi ndiyo makusudio ya Serikali. Nikataka maelezo ya Serikali. Majibu

[MHE. DAVID Z. KAFULILA]
niliyojibiwa, Wizara ya Fedha ikaonyesha kwamba taarifa hiyo siyo kweli. Lakini pia ikaonyesha kwamba jambo hilo au uamuzi huo wa misamaha ya kodi kwenye mchele na sukari ina tija.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara. *TRA* wanatoa taarifa zao kwenye Kamati yetu. Taarifa ninayo hapa, labda kwa maslahi ya Bunge lako Tukufu niseme kwamba.

**SPIKA:** Ninakuomba Mheshimiwa Mbunge, jinsi unavyoelekeza hoja zako utaratibu siyo huo. Kwa sababu kama ni suala la *issue* ya swali, hatuwezi kuanza ku-*debate* swali lililojibiwa. Kama una hoja yoyote andika maelezo sisi tupate majibu. Kwa sababu hatuwezi kubishania maswali. Wabunge ninaomba msikilize hizi ni Kanuni, siyo kwamba mnaenda kama tunaendesha *Club* ya pombe.

Ninachomuagiza Mheshimiwa Kafulila, aende akaandike, kusudi lije kwa utaratibu wake, hatuwezi kubishana maswali yote hapa. Kaandike leta ije kwa utaratibu unaohusika. Mheshimiwa Mbunge yule aliyesimama alikuwa ni nani?

*(Hapa Mheshimiwa David Z. Kafulila Alisimama Tena)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila nimeishakuagiza tayari ukafanye nilichokuagiza. Waheshimiwa wengine ni nani aliyesimama?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 64(i)(a). Ambayo inasema kwamba: "Bila kuathiri masharti ya Ibara 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge. Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Mheshimiwa Spika, wakati nimeuliza swali la nyongeza kutokana na swali ambalo liliulizwa na Mbunge Mheshimiwa Profesa Peter M. Msola, swali nambari 34.

[MHE. MOSES J. MACHALI]
Naibu Waziri katika majibu yake, kuna *statement* ambazo amezitoa kidogo zinaashiri kama kwamba yeye ni Nabii, anajua ambacho mimi ningelieweza kufanya jambo ambalo halina ukweli. Alizungumza. "*Suppose* ingelikuwa ni Makampuni makubwa ya uchumbaji wa Madini, mimi Mbunge nisingeliweza kuwatetea. Lakini kwa sababu ni wachimbaji wadogo wadogo ambao wanaopatikana kule Makere, wachimbaji wa chokaa, ninawatetea."

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kunithibitishia, amepata wapi ithibati au ushahidi kwa kusema kwamba nisingeliweza kuwatetea wachimbaji wakubwa wakubwa. Watu baadhi ya Mawaziri wamekuwa wanajibu kiainaaina, hovyo hovyo tu wanavyofikiria majibu ya kubeza Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba kwa sababu alichokizungumza hayupo akilini mwangu, na wala hayupo ndani ya utashi wangu, na mimi ni Mbunge wa wote. Wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo.

Ninaomba mwongozo wako ni kwa nini, Mheshimiwa Waziri asiweze kuniomba radhi. Ndiyo aniombe radhi, kwa sababu alichokizungumza sikuwa katika *perspective* hiyo kabisa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako juu ya hili. Kwa sababu baadhi wamekuwa wanajibu maswali kiaina aina tu ambavyo wanavyojisikia na Bunge limeonekana ni mahali pa kuweza kuzungumza vyovyote vile.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba mkae chini wote. Ninaomba mkae chini wote. Waheshimiwa ndiyo maana nimemwambia Mheshimiwa David Kafulila. Utaratibu wa kama hujaridhika kuhusiana na jinsi maswali yaliyvyojibiwa. Hatuwezi kuanza kubishana hapa. Kila

[SPIKA]
Mbunge aliyeuliza hapa, akitaka kubishana swali lake atabishana hapa, ndiyo maana nikasema tuna Kifungu kinachosema utatoa maelezo binafsi. Katika maelezo binafsi tunafanya kabla ya kuahirisha kikao jioni, yeyote yule ambaye anafikiria hakupendezwa na jambo fulani, anao muda wa kuandika na kusoma, tutampa dakika zake zote za kusoma. Halafu pale utaratibu wetu unachukua nafasi yake. Vinginevyo kila mtu tukimruhusu katika pindi cha maswali asimame na kusema mimi sikuridhika. Itakuwa siyo Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ninawaagiza Mheshimiwa David Kafulila, kafanye hivyo. Mheshimiwa Moses Machali, kafanye hivyo. Mimi nitawapeni muda wakati muafaka muweze kueleza hayo mnayotaka kujieleza. Vinginevyo haiwezikani kama hivyo mnavyotaka. Wengine wanaona uvivu kufanya hivyo. Huu ni utaratibu, andikeni mkaeleze mtapewa muda fuateni Kanuni ya 28 na Kanuni zinginezo zile.

**MBUNGE FULANI:** Hakusikika

**SPIKA:** Kitu gani?

**MBUNGE FULANI:** Hakusikika.

**SPIKA:** Nani Mbunge gani?

Mheshimiwa unajua tatizo la Wabunge mnachanganya kila kitu. *Power of replying* hata wewe kama umekuta mtu amekusemea eneo lako unayo, una haki ya kujibu, Mbunge yeyote anayo haki ya kujibu. Mbunge alijibu kama Waziri wakati wa maswali alisimama.

*(Hapa Waziri fulani alisimama)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ninakuomba na wewe pia ukae na unyamaze. Mheshimiwa Waziri *communication* mnayoifanya mnaleta fujo katika Bunge.

*[SPIKA]*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe na *order*, tatizo lenu ninyi mnafikiri kwamba humu tunaweza kuongoza tunavyotaka, hapana, kila kitu kina Kanuni zake na naomba mjifunze hivyo, siyo suala la kuzomea au kufanya nini, sio *point*, someni Kanuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu nilizoeleza, tunasimama kwa ajili ya Kamati ya Mipango.

**KAMATI YA MIPANGO**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na uchangiaji kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2014/2015. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, ajiandae Mheshimiwa Stephen Ngonyani na Mheshimiwa Mbatia. Mheshimiwa Mgimwa!

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye Mpango, kwanza nataka nizungumzie habari ya bajeti ya mwaka 2013/2014. Makusanyo ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ya robo ya mwaka ni 85.7% kwa makusanyo ya ndani na 34.2% kwa makusanyo ya nje. Makusanyo hayo yanatoa dira kwamba uwezo wa Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo ni tatizo kwa sababu mpaka sasa tumepata 32.4% tu kutoka kwenye misaada ya nje, kuna pengo la 68%, hili ni tatizo. Kwa hiyo, Serikali inatakiwa ijiangalie upya ili kusudi tuweze kujiimarisha katika makusanyo ya ndani ili tuweze kushughulikia miradi ya maendeleo hapa nchini. Kwa mfano, tulikuwa tunataka tujielekeze kwenye Wizara ya Maji kwa kipindi cha robo mwaka kwa shilingi bilioni 157 lakini mpaka sasa hivi imetolewa shilingi bilioni 43. Kwa maana hiyo ni

*[MHE. M.H. MGIMWA]*

kwamba miradi mingi ya maji vijijini haijatekelezwa. Kwa hiyo, Serikali tunatakiwa tujiangalie upya katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012/2013, Serikali ilipanga matumizi ya bajeti ya shilingi trilioni 15 na mwaka 2013/2014, Serikali ilipanga matumizi ya bajeti ya shilingi trilioni 18 na mwaka 2014/2015, Serikali imepanga matumizi ya bajeti ya shilingi trilioni 20, kila siku Serikali inaonyesha kwamba kuna ongezeko la matumizi lakini ukiangalia hali halisi Serikali huwa haina uwezo wa kufikia, kwa mfano mwaka 2012/2013, Serikali haikuweza kuwa na uwezo wa kukusanya shilingi trilioni 15 na mwaka 2014, nina uhakika kabisa Serikali itakuwa haina uwezo wa kukusanya shilingi trilioni 18. Kwa hiyo, ni vema Serikali inapotuletea Mpango huu wa Maendeleo ikatuonyesha na *source,* wapi tutapata pesa hizo hasa tukijiekeleza katika maeneo ya ndani kuliko kutuwekea mipango mikubwa ya matumizi wakati uwezo wa kukusanya pesa hizo kwa ajili ya matumizi hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kuhusu Tume ya Mipango, lakini kabla sijazungumzia Tume ya Mipango, naomba nisome kidogo mapendekezo ya Kamati ya Bajeti. Kamati ya Bajeti inasema kwamba Tume ya Mipango ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya kitaifa nchi nzima. Nchi yetu ni kubwa na miradi mingi hutekelezwa kwa wakati mmoja. Kamati inasita kuamini kwamba Tume ya Mipango katika hali yake ya sasa inaweza kutekeleza majukumu haya. Mimi sikubaliani na hoja hii ya Kamati. Tume ya Mipango ni *thinking tank* ya Serikali kwa hiyo kazi yake kama *thinking tank* ni kuelekeza tu na siyo kusimamia miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea ku-*quote*, Kamati inasema kwamba; aidha Maafisa Mipango wa Wizara na Halmashauri hutakiwa kuandaa maandiko ya miradi na kuwasilisha Tume ya Mipango kabla ya kuidhinishwa na kutolewa idhini ya fedha. Hata hivyo, Kamati imearifiwa kuwa wengi wa Maafisa wana uwezo mdogo wa kuandaa maandiko ya miradi. Sasa kama *thinking tank* inakuwa haina

*[MHE. M.H. MGIMWA]*

watu wenye uwezo basi hilo ni tatizo. Naomba tuliangalie eneo hili, kwa hiyo, Tume ya Mipango inatakiwa iwe na watu wenye uwezo wa kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango imekuwa na tatizo, kuna baadhi ya maeneo imetuletea matatizo. Wabunge tunaamua katika bajeti na Wizara ya Fedha inaamua, ikifika wakati wa uidhinishaji wa fedha lazima Tume ya Mipango ipitie, kwa hiyo, inakuja kutucheki mara ya pili sisi Wabunge tumefanya nini. Hili jambo siyo zuri na matokeo yake miradi mingi ya maendeleo inachelewa na kuchelewa kwa miradi ya maendeleo kunasababisha *cost* ya ile miradi kuwa mikubwa zaidi. Kwenye jambo hili mimi sikubaliani na hilo jambo, baada ya sisi Wabunge kupitisha bajeti kama fedha zipo zipitishwe na ziende kwenye miradi inayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni Sheria ya Manunuzi. Sheria ya Manunuzi imepitwa na wakati. Sheria ya Manunuzi inasababisha gharama nyingi, imekuwa na mianya mingi ya rushwa na pia kumekuwa na udanganyifu mkubwa. Kwa hiyo, Bunge lako Tukufu na Serikali zinatakiwa ziangalie utaratibu mpya wa kurekebisha sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mtovu wa fadhila nisiposema kwamba Serikali kuna baadhi ya maeneo imefanya vizuri na hakuna eneo kubwa ambalo Serikali imefanya vizuri kama katika eneo la barabara. Miundombinu ya barabara hapa nchini ni mizuri, ni ukweli usiopingika lakini bado kama Serikali tunatakiwa tuendelee kufanya vizuri katika kurekebisha uchumi wetu, tunatakiwa tujiwekee mikakati katika eneo la reli. Kama kweli tutajiimarisha kwenye reli *automatically cost of production* zitashuka hapa nchini na kusababisha hali ya uchumi kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni ukusanyaji wa pato la taifa. Wenzetu Serikali wanatuambia pato la taifa kwa mwaka uliopita lilikuwa ni 6.9% na safari hii ni 7.0. Ni kweli katika nusu mwaka hali ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



mapato imebadilika, lakini hali ya mapato imebadilika mbona haiendi sambamba na kuondoa hali ya umaskini? Pato la Tanzania limebadilika lakini hali ya umaskini iko palepale. Kwa hiyo, ukituambia pato la Taifa limekua hapa si kweli na mimi sikubaliani na hoja hii. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba kama tunataka tuzungumzie hali ya mapato ni lazima iende sambamba na ukuaji wa uchumi wa mtu mmojammoja kwa ujumla. Matabaka kati ya watu maskini na matajiri limezidi kuwa kubwa zaidi kuliko hapo awali, kwa hiyo, tunatakiwa tujiangalie kwenye eneo hili. Tukitaka kujua kama uchumi umekuwa lazima *gap* lipungue la waliokuwanacho na wasiokuwanacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni mfumuko wa bei. Ni kweli mfumuko wa bei umeshuka lakini mfumuko wa bei ungeshuka zaidi kama tungeangalia eneo la umeme, kama umeme ungepungua bei zaidi, nina hakika kabisa mfumuko wa bei ungeshuka. La pili, ni eneo la reli, kama usafiri wa reli ungekuwa wa uhakika nina uhakika kabisa *cost of production* ingeshuka na mfumukowa bei ungeendelea kushuka. La mwisho, hivi ni sababu zipi zinazotufanya sisi Watanzania tuendelee kuagiza mchele nchi za nje wakati mchele upo mwingi kwenye ma-*godown*? Hii ni aibu na tunaendelea kuongeza *cost* ambazo hazina thamani yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri mhusika na Serikali, inieleze mikakati iliyoiweka ya kuwalipa wazabuni wa ndani. Tumekuwa tunawatesa wazabuni wa ndani, wananchi wa Tanzania wanazidi kujitahidi kutaka kujiimarisha kiuchumi lakini Serikali ndiyo inakuwa inawaangusha watu wake wenyewe. Tunataka mikakati ya uhakika, Serikali imejipanga kiasi gani kuwalipa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mgimwa, muda wako umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Stephen Ngonyani, ajiandae Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa

Mwaiposa pia ajiandae. Naona Mheshimiwa Stephen Ngonyani hayupo na sasa namwita Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hii ya mapendekezo ya mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Spika alitoa agizo kwa Serikali kwamba Mpango huu ni wa Serikali nzima lakini sasa hivi kuna *full Ministers* wapo wanne tu. Sasa sijui tunafanya kitu gani hapa jamani! *Full Ministers* wapo wanne tu kati ya Mawaziri 29 yaani sijui tumechoka, kuna mchokomchoko fulani hivi katika jamii ambao unasikitisha sana, sijui tunakwenda wapi? Wa tano ndiyo anaingia sasa hivi Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu kubwa, ni umakini wa mipango tunayopanga hapa. Mapendekezo ya mpango huu yana kurasa 62, zaidi ya kurasa 47 ni kama *copy and paste* za mwaka jana na kurasa 13 au 14 ndiyo mpango wenyewe tunaotegemea wa mwaka ujao wa fedha. Kurasa 62 kwa Wabunge na makabrasha mengine kusoma inakuwa ni kujirudiarudia sana. Naomba tu kusema kwamba, dunia ya leo kuna kitu kinachoitwa *KISS (Keep It Short and Simple)*, waweke kwenye majedwali ambayo yanarahisisha Waheshimiwa Wabunge kuweza kufuatilia kwa umakini na urahisi kuliko hii vuta nikuvute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumechambua kwa makini na niseme kabisa mawazo yetu ya Kamati ya Bajeti nayaunga mkono na tuangalie vipaumbele ambavyo ni muhim. Nizungumzie vipambaumbele viwili yaani bandari pamoja na reli kwa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ambaye ameingia hapa sasa hivi. Kama tunataka uchumi wetu uweze kuingia kwenye karne ya 21, ukaingia kwenye kipato cha kati, hatuna budi kuwekeza kwa kiwango kikubwa kwenye bandari na reli. Bandari zetu zote zinahitaji kama dola bilioni tatu. Bandari ya

Dar es Salaam dola bilioni 1.5 na reli inahitaji kama dola bilioni 7. Jumla tukitafuta dola bilioni 10 tutaondokana na huu wasiwasi tunalionao, tutafungua lango kuu la reli ya kati au lango kuu la uchumi na usafiri ambao ni rahisi kuliko wote duniani kwanza ni wa maji, pili ni wa reli. Ujenzi wa barabara ambao tunausifia sana, usafirishaji wa zaidi ya kilomita 600 huwa ni hasara. Angalia haya malori makubwa yanavyozidi kuharibu barabara zetu kwa hiyo tunarudia kwenye umaskini uleule yaani tunajenga barabara ya kuja Dodoma, ya kwenda Kaskazini hata ya kwenda Kusini. Kwa hiyo, bila kura na reli ambayo itasafirisha mizigo na kwa urahisi ambao ni *cheap,* tutakuwa hapa tunajidanganya tu kwamba barabara zimejengwa lakini tunazunguka kwenye umaskini uleule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa Serikali, wanasema deni ni himilivu lakini kwa mapana zaidi, timu iwe ni ya maabara au ni ya wapi, fedha zipatikane, *generation* hii iwekeze kwenye bandari, *geographically* tupo vizuri, tuwekeze kwenye reli vizuri ili tuondokane na hizo ngonjera za vuta nikuvute za kukopa dola 100,000, 200,000 au 1,000,000 lakini tukope *heavily* na tuwekeze, mikopo hii duniani ipo na siyo lazima tufuate masharti ya *IMF* na *World Bank* tu, sisi ni Taifa ambalo tukiamua tunaweza. Sisi nchi yetu hii ambayo imekuwa ni kiongozi katika Bara la Afrika, mbona tunakuwa na majibu mepesimepesi kwa maswali ambayo ni magumu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tarehe 9/4/2013 tulivyokwenda kumwapisha Uhuru Kenyatta nilikuwepo na Waziri Sitta alikuwepo na Mheshimiwa Lowassa na wengine. Wimbo wa Afrika uliopigwa, beti ya kwanza ni wimbo wa Tanzania, ni wimbo wa Afrika leo kwamba Mungu ibariki Afrika, ndiyo wimbo wa Afrika. Sasa kama tumepewa heshima hiyo na Bara la Afrika, sisi Tanzania tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia ngonjera zilizotokea jana hapa kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, hakuna kosa kuwa na ushirikiano kati ya Kenya na Tanzania wala Kenya na Uganda, ukiangalia nchi zote za Afrika Kenya

ni ya kwanza kwa uwekezaji wa Tanzania *FDI* yaani *Foreign Direct Investment*, kwa dunia ni ya pili, lakini majibu hapa nani kampa talaka huyu, nani kamuoa huyu, *economic diplomacy* ipo wapi? *Let us be sincere*! Kauli hizi zinaleta maafa makubwa kwa Taifa hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uongozi wetu wa Taifa la Tanzania sawa, tuna kilomita za mraba zaidi ya 945,000, Kenya 581,000, Uganda 236,000, Burundi 27,000 na Rwanda ni 26,000, sawa sisi tumewazidi kwa zaidi ya kilomita za mraba 73,000 lakini tumewazidi hivyo, tunaitumiaje fursa tuliyonayo katika kuonyesha kweli tunaongoza katika ukanda huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie kwenye sekta ya utalii, Tanzania ni ya pili kwa vivutio vya utalii duniani baada ya Brazil lakini ukiangalia tupo nafasi ya ngapi kwenye vivutio hivi katika kuleta mapato kwenye Taifa hili katika ushindani? Sisi ni wa pili duniani lakini tunashika nafasi ya 110 kati ya nchi 133. Mauritius ni ya 131 kwa vivutio vya utalii duniani kati ya 133 lakini ni ya 53 katika sekta ya utalii. Sasa ukiangalia hii sekta ya utalii leo hii, wenzetu wa Kenya ni wa 28 kwa vivutio vya utalii lakini *in terms* ya uingizaji wake wa pato la Taifa ni 103 imeishinda Tanzania, sisi ni wa pili duniani. Sasa sekta hii ya utalii mbona kigugumizi? Mwaka jana hapa kwenye bajeti na tusingependa itokee tena kwenye bajeti inayokuja kwamba tunaanza tena kukamua watalii hawa wakati tunajaribu kuikuza sekta hii ya utalii, tunajaribu tuangalie sekta ya anga itakuwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia leo hii *KLM* kutoka Amsterdam kuja Kilimanjaro, kuja Dar es Salaam ni aghali kuliko kutoka Amsterdam kwenda Nairobi. Sasa kwenye utalii humu tunawekezaje? C*ostal line* yenye kilomita 1,424, mahoteli ya kitalii yapo wapi? Wazawa watalii wanaowekeza humu ndani, mzawa anapewa nafasi ya kujenga hoteli lakini hapewi eneo la kujenga hoteli, inakuwa ni urasimu tu. Wizara ya Ardhi na Wizara ya Utalii wanatenga maeneo, wanakubaliana mwekezaji amekuja *immediately* anapewa

eneo ili kuondokana na huu urasimu, urasimu, urasimu, urasimu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwa kweli, tujitahidi tuone ni namna gani badala ya kusikiliza upande mmoja tu kuhusu hili sokomoko lililotokea tarehe 24 na 25 mwezi wa Juni kule Kampala na 28 Agosti, 2013, Jumatano, kule Mombasa kuhusu Rwanda, Uganda na Kenya. Tumesikiliza upande mmoja wa Serikali lakini ukiangalia Wakenya walivyowekeza hapa waweza kutuacha hivihivi, hapana! Tuone hii ni changamoto chanya na sisi tuamke tuwekeze *seriously* kwenye bandari yetu, tuwekeze *seriously* kwenye reli yetu na kutoka Dar es Salaam kwenda Bunjumbura na kwenda Congo ni karibu zaidi na ni punguzo la zaidi ya kilomita 1000 kwa hiyo *economically* mfanyabiashara yeyote atakuja kwenye bandari ya Dar es Salaam. Sasa tusilalamikelalamike tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nguzo kuu sita za umaskini wa fikra. Nguzo ya kwanza ni majungu, ya pili ni fitina, ya tatu ni umbeya, ya nne ni kusema uwngo, ya tano ukishasema uwngo unajenga chuki katika jamii na ya sita ni uvivu wa kufikiri. *Let us be sincere,* tujiulize tunaongea nini na nani, mahali gani, wakati halafu athari yake itakuwa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe Taifa linaloongoza Bara la Afrika. Uwezo huo tunao, tusiangalie wazo limetoka kwa nani, angalia *quality* ya wazo lenyewe, angalia fikra zenyewe, tushirikiane wote. Naamini pamoja tukiamua Taifa la Tanzania tunaweza, uwezo tunao ilimradi tuachane na hizi tofauti ndogondogo za kiitikadi kwenye mpango wa kitaifa tunawekeza fikra zetu zote kwa pamoja kwa kuwa Taifa hili ni letu sote kwa maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia muda huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kutunza muda. Sasa namwita Mheshimiwa Mwaiposa, ajiandae Mheshimiwa Jenista Mhagama na atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nashukuru kupata nafasi ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu kuhusiana na Mpango ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze waandaaji, lakini la pili nitake kusema kwamba ni mara yangu ya pili kusimama hapa Bungeni kuongelea suala la vipaumbele. Nakumbuka mwaka jana wakati ninachangia, niliishauri Serikali ijaribu kuja na vipaumbele vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mpango huu, umekuja na vipaumbele Sita. Hata hivyo, mbali na vipaumbele hivyo umekuja tena na sehemu nyingine kumi na mbili ambazo pia zitapewa vipaumbele. Tukiangalia maana ya hilo neno vipaumbele, maana yake ni mpango ambao unatakiwa utoe fursa kwa maeneo machache lakini maeneo mengine yakiwa yameachwa. Hata hivyo, ukiangalia kwenye mpango huu kiuchumi hakuna hata eneo moja ambalo limeachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata wasiwasi sana kwa sababu tukienda kwa jinsi tunavyokwenda na vipaumbele sita na maeneo mengine kumi na mbili, tutamaliza mwaka kama ilivyo kawaida, tutashindwa kufuatilia, tutashindwa kufanya *monitoring*, tutashindwa ku- *evaluate* na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano, naona Serikali ya awamu hii imejitahidi sana kuelekeza nguvu nyingi kwenye barabara na hilo limeonekana. Laiti tungeweza kuchukua vipaumbele vichache kwa mwaka mmoja tu, hata tukachukua tu hiyo miundombinu, tukaweza kuhakikisha kwamba mambo ya umeme yamekaa vizuri, mambo ya

kilimo yamekaa vizuri, mambo ya viwanda yamekaa vizuri, nadhani hii ingeweza ikasaidia sana nchi kuona kwamba ni wapi inakwenda vizuri au ni wapi imekwenda vibaya. Kwa mpango huu, nadhani tunaweza tukafikisha mwaka kama ilivyo kawaida tukashindwa ku- *evaluate* kwamba tumefanya vizuri namna gani katika sekta hii lakini pia ni wapi tulikwama tusifanye vizuri katika sekta hii. Kwa hiyo, bado naiomba Serikali, hebu iangalie ni namna gani inaweza ikaja na vipaumbele vichache ili tuweze sasa kuhakikisha tuna-*concentrate* kwenye zile raslimali chache za kifedha tulizonazo na *impact* iweze kuonekana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mengine ambayo napenda sana kuyazungumzia kwa mfano, elimu. Tukienda kwa mwenendo huu wa vipaumbele vingi lakini pia tukikumbuka ule mradi wa Matokeo Makubwa Sasa na haya matokeo makubwa yakajikita kwenye vipaumbele vyote hivi, nina wasiwasi kabisa kwamba tunaweza tusifanye vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu nimepata nafasi ya kuzungumza na Walimu katika shule zao za *primary* katika Kata sita kati ya nane nilizonazo katika Jimbo la Ukonga. Lengo lilikuwa ni kuangalia zile changamoto walizonazo, lakini pia ni namna gani wamejipanga kupokea mpango huu wa Matokeo Makubwa Sasa. Changamoto ziko nyingi mno, lakini kama tutakwenda kwa mtindo huu tunaokwenda nao, hata katika elimu hatutaweza kufika mahali kwa sababu ziko changamoto za uchakavu wa madarasa, madarasa hayatoshi, madawati hakuna, Walimu hawatoshi na kadhalika. Pia nilipata tena nafasi ya kuongea na Maafisa Elimu katika Kata husika. Wale wenyewe wanasema kwamba wanausikia huo mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, lakini wana changamoto lukuki ambazo zitawafanya wao washindwe kusaidia mpango huu ili uweze kufanikiwa hasa katika nyanja ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana labda na jiografia ya maeneo mbalimbali ya Tanzania yalivyo, hususani ya Jimbo la Ukonga, unajikuta kwamba Afisa Elimu ambaye ni msimamizi mkuu wa shughuli za elimu katika Kata nzima,

*[MHE. E.E. MWAIPOSA]*

kutokana na jiografia anashindwa kufikia shule mbili kwa siku. Hiyo ni changamoto. Ssasa wao wanasema mpango umekuja, lakini sisi vitendea kazi bado havijafika. Huo ni mfano tu ambao nimesema niutoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kama imekuja na vipaumbele vingi kiasi hiki basi hebu iangalie sasa Mpango huu wa Matokeo Makubwa tusije tukauelekeza kwenye vipaumbele vyote na maeneo yote ya kiuchumi ya Tanzania. Tungechagua maeneo machache, hata matatu au manne tu, tukaweza kuelekeza huko huu mpango ili kwanza tuweze kuusimamia vizuri, lakini pia tuweze kuja ku-*evaluate* ni namna gani katika hizi sekta ambazo tumejielekeza kwa sababu ya kuwa na rasilimali chache za kifedha tumefanikiwa na pia namna gani hatukufanikiwa na kwa sababu gani. Hayo ndiyo mawazo yangu katika kuishauri Serikali kwenye jambo zima la kuchagua vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la reli. Nakumbuka hata mwaka jana eneo hili lilizungumziwa sana. Hili ni eneo ambalo kama likitumika vizuri linaweza likasaidia sana kunyanyua uchumi wa nchi hii na lingeweza pia likasaidia kuhakikisha kwamba bei za bidhaa nyingi zinapungua. Hata hivyo, cha kusikitisha nimesoma mpango huu nikakuta kwamba mwaka jana, kati ya mambo ambayo yalikuwa yafanyike kwenye reli, ni upembuzi yakinifu. Hiyo ilikuwa ni mwaka 2012/2013 ndivyo ilivyoandikwa kwenye mpango, mwaka 2013/2014 hiyo haijazungumzwa lakini mwaka 2014/2015 ndiyo sasa inakuja na kitu gani kitafanyika kwenye eneo hili la reli. Naona pia wamerudia kwamba wataendelea kumalizia upembuzi yakinifu pamoja na kutafuta wakandarasi watakaofanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kama tunavyokwenda, ni wazi tutachelewa kufika, kwamba kwa miaka mitatu tunafanya upembuzi yakinifu. Hii itafanya maendeleo yachelewe sana. Naomba eneo hili la reli lipewe kipaumbele ili ujenzi wa reli uweze kuanza hasa zile zinazochukua mizigo kwa sababu kwanza malori mengi yanaharibu sana barabara. Kama ambavyo Waheshimiwa

Wabunge wameona, hasa wale waliotokea Dar es Salaam, barabara nyingi zimeharibika kwa sababu ya kubeba mizigo ambayo ni mikubwa zaidi kwenye malori. Kwa hiyo naomba pamoja na maeneo hayo, basi kwenye eneo hili la reli Mheshimiwa Waziri aangalie ni namna gani anaweza kuharakisha na kuhakikisha mizigo mikubwa yote inaelekezwa kwenye usafiri wa reli ili iwezeshe reli kujiendesha yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo eneo la viwanda. Mpango ni mzuri, umezungumzia viwanda lakini nisikitike kusema kwamba sijaona kama tulivyoongea mwaka jana, tuliomba Serikali ianze kufuatilia viwanda vile vya zamani ambavyo walipewa wawekezaji ili waviendeleze kwa mujibu wa utaratibu ambao ulikuwa umewekwa. Vipo viwanda vya katani, viwanda vya kutengeneza magunia, viwanda vya ngozi ambavyo vimekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza kuanzisha viwanda vipya wakati vipo viwanda vya zamani ambavyo vilikuwa vinatakiwa vifufuliwe kwanza ili viweze ku-*accommodate* vijana wetu na watu wengine ambao hawana kazi, tutapoteza rasilimali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwaiposa, kengele yako ya pili.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Assumpter Mshama, wajiandae Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Zainabu Vullu.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo napenda niliongelee ni kwamba, labda tungeondoa neno kipaumbele katika mpango huu kwa sababu unaposema kipaumbele, ndani ya kipaumbele hakuna kipaumbele. Kwa hiyo, kusema kuna vipaumbele lingeweza kuondoka tukatumia neno mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Mpango wa Maendeleo wa mwaka huu, mpango huu wa mwaka 2014/2015 hauna tofauti na mpango wa mwaka 2012/2013. Kwa maana nyingine kama kungekuwepo na kipaumbele, ina maana vipaumbele vilivyokuwa vimekuja, vilikuja vitano, kitu walichokifanya leo wamechukua kile kipaumbele cha mwisho wakakitenga vikawa viwili, mwaka huu vikawa sita. Pale ambapo anasema huduma za utalii na fedha, mwaka jana vilikuwa vimeunganika lakini mwaka huu imekuwa ni kipengele cha tano, huduma za fedha na kipengele cha sita ni utalii. Kwa hiyo, ni kwamba hakuna kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika tatizo ninaloliona linalosababisha Mpango wetu wa Maendeleo wa Tanzania usifanyike. Kama mtu angekuwa na mpango, nakumbuka tena hata nilipochangia mara ya mwisho nilisema kabisa kwamba, mpango mzuri upo lakini watekelezaji ni akina nani? Mfano kama unataka kusema una mipango sita, tungesema ni ya miaka mitano, tungekuja na mipango kama ninavyofikiri, labda mwaka 2011 ukaweka miundombinu na kilimo, mwaka 2012/2013 maendeleo ya rasilimali watu na huduma za fedha, mwaka 2014/2015 ukaenda viwanda na huduma za utalii. Mwaka unaofuata ungechomoa kimoja kwamba hiki sasa kimekuwa tayari, tunaingiza kipaumbele kingine. Kwa hiyo, ndiyo maana ninasema hakuna kipaumbele, kuna mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye niliyoyachunguza na kuyaona yanayosababisha mipango yetu isitekelezeke. Jambo la kwanza ni kuwa na vipaumbele au mipango mingi kwa wakati mmoja bila kuwa na fedha za kutosha kufanyia kazi hizo. Ukiwa unatumia *cash budget*, yaani wewe unaandaa, kwa mfano hiyo staili inayotumika hata harusi ina nafuu. Mtu anapoandaa harusi anakuwa anaandika vitu na analeta bajeti kwamba tunategemea kupata wageni mia nne (400) na tunategemea kuwa na kitu hiki na hiki, lakini kwenye Serikali huwezi ukandaa bajeti wakati huna hata senti tano mfukoni, unategemea watu au Mipango au makusanyo yatakayotokea. Kwa hiyo, huwezi kufikia malengo hata siku moja. Kwa mfano, unategemea bia, watu wakiokoka wakaacha kunywa bia huwezi kupata fedha. Ulikuwa unategemea kupata kodi, bila kutumia *capital budget* hatuwezi kutimiza mipango yetu hata siku moja. Kwa hiyo, suala la kwanza lazima tu-*deal* na *cash budget*, tusipange mambo kama kwenye harusi. Hata wale wanaoandaa mpango hawafahamu fedha watazitoa wapi. Wanaandaa mpango, wanauleta kwetu, ukiwauliza hizi fedha utapata wapi hawana majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kufanya kazi kwa mazoea. Mpango huu tunasema tumekuja na staili mpya ya Matokeo Makubwa Sasa, lakini kwa watu wapi? Watanzania hawa ambao wamezoea kufanya vitu kama wanavyotaka, siyo rahisi kutimiza utaratibu huo. Kukosa wasimamizi walio makini, walio na mzigo wa kulisaidia Taifa hili, bila hivyo hiyo *Big Results Now* haiwezi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulindana kazini. Mtu anakosea, anaendelea kuwepo kazini, unategemea kupata matokeo makubwa kwa sasa, siyo rahisi! Halafu chuki, fitina na ugomvi, watu wengine hawamwambii Rais ukweli. Kuna mtu tulimwita katika Kamati yetu, wakati anajieleza, alitueleza labda fulani awepo. Alipokuja huyo mtu akasema, aah mbona mnatugombanisha? Aah, wewe si ulisema akiwepo huyu na sisi tukiwepo tutaweza kufanya mambo sawasawa? Tukamwambia wewe ndiye unatakiwa sasa hivi kumshauri

Rais, utamshauri nini wakati amekuja mtu mmoja umebabaika na umesema vitu tofauti? Kwa hiyo, hata fitina, kutomwambia Rais ukweli, watu hawamwambii Rais ukweli na matokeo yake mambo hayaendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutotathmini kazi iliyofanyika. Kuna miradi, kwa mfano ukiangalia kwenye mpango wa mwaka jana miradi ile imebeba mambo muhimu 18. Hivi leo amekuja Bwana Mpango na mpango uleule wa mwaka jana, unawezaje kutathmini? Huwezi kupata *impact*. Kwa hiyo, kinachokosekana ni watu kutojua kwamba hivi vyote tunapeleka vitaweza kufanyika kwa wakati huu kulingana na uwezo wetu wa kifedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawaogopi mtu awaye yeyote. Mtu anaweza kufanya kitu chochote, kwa wakati wowote na asiulizwe chochote, na hata akiulizwa hakuna kitu kitakachofanyika. Huwezi kupata matunda au majibu ya kusema *'Big Results Now'* kwa sababu watu hawaogopi kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzembe wa hali ya juu kazini. Kwa mfano, mtu ametengeneza barabara ameiharibu bado anapewa muda tu irudie, irudie, irudie, uzembe wa hali ya juu! Kwa nini mtu huyu asifilisiwe tukaweka mtu mwingine akatengeneza barabara ikawa tayari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi zaidi ya mapato. Hivi kweli Wabunge tunafika mahali hatujapata mshahara, tunapata tarehe 30 kama tunafanya kazi kwa Mhindi, maana Mhindi ndiye ana mpaka tarehe 34 au kwa mtu binafsi! Kusema kweli ni matumizi mabaya, matumizi yanayozidi mapato. Ukipiga matumizi yetu, eti unategemea mtu kutoka China ndiyo atusaidie katika matumizi, kwa nini tusikusanye? Tungefanya kama wanavyofanya watu wengine, anakusanya fedha za miezi mitatu, kama hujakusanya unakopa zinakuwepo, kwa hiyo, unapanga mambo kulingana na kilicho kwenye kikapu, lakini watu wanaandaa vitu wakati kwenye kapu hakuna kitu. (*Makofi*)

*[MHE. A.N. MSHAMA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya kazi bila malengo. Mtu yuko kazini ameajiriwa, hajawekewa malengo kwamba ifikapo tarehe 30 tunataka utuletee moja, mbili, tatu. Anafanya kazi, anaweza kwenda Kariakoo, akazurura mjini, tarehe 30 lazima alipwe. Kwa nini watu wasiwekewe malengo ya kutimiza ili mtu alipwe kulingana na kile alichokifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni maneno mengi kuliko matendo. Sisi tulipoletewa huu mpango kuuangalia kama bajeti, tuliuliza kitu, hivi tumebadili *budget cycle*, imetuletea mabadiliko gani katika nchi hii? Mimi naona ndiyo imekuwa *worse*, yaani tumekuja na mpango, tumekuja na bajeti hapa tukasema kuanzia tarehe 1 Julai, mambo yatakuwa sawa, lakini mpaka leo katika Wilaya yangu ya Misenyi fedha ya maendeleo, hakuna! Sasa tulikuwa na sababu gani ya kubadili *budget cycle?* Mimi naona kwamba watu maneno ni mengi kuliko matendo, tukiweka nguvu kwenye matendo lazima tutapata *Big Results Now.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mipya kabla ya zamani kuisha. Una mradi huu haujaisha umeanzisha mwingine, matokeo yake unajikuta una miradi chungu mbovu ambayo haitimiliki. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie, hayo ndiyo niliyoona yanayosababisha mpango kutotekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya mapato ya ndani. Mheshimiwa Waziri ameeleza katika maelezo yake kwamba wanakwenda kuangalia vyanzo vipya. Naomba atakapohitimisha atueleze ni vyanzo vipya vipi ambavyo tunaweza tukaongeza mapato. Uko ushauri mwingi Wabunge wanautoa, lakini kila siku tunarudishiwa maji, soda, sigara na bia. Tunaomba tuone ni namna gani wamegundua vyanzo vipya na tunataka kuviona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kazi na ajira. Tuna vijana wako mitaani, watu wengi hawana kazi. Hiyo yote ni kwa sababu hata wanapokwenda shuleni wanasoma wanajua wakimaliza shule ni kuajiriwa. Kwa nini kwenye

mitaala tusiweke mtu kujua kwamba unapomaliza shule ukiajiriwa ni sawa lakini bado kuna kujitegemea. Pili, Serikali ikaandaa utaratibu mzuri wa vijana wanapomaliza shule wanakuwa wanaweza kwenda kujiajiri, lakini mazingira mazuri ya kujiajiri yaweze kufanyika na hivyo tunaweza tukawasaidia. Vijana wengi wana vyeti vyao, wanahitaji *collateral* katika benki, kwa nini tusiwe na benki ya vijana ya kuwasaidia? Wao wakijulikana na matatizo yao na kwa maana hiyo misingi ya kukopa itakuwa tofauti na misingi mingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mshama na sasa ninamwita Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Vullu, Mheshimiwa Ntukamazina na Mheshimiwa Selasini wajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu hiki, ukurasa wa 48 unasema kuwa, inapendekezwa kwamba maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015 yazingatie yafuatayo:-

(i) Kudumisha amani na utawala bora kwa kuwa ni misingi muhimu na kuwezesha uzalishaji mali, uwekezaji, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niguse kwenye eneo muhimu sana la utawala bora. Katika siku za hivi karibuni imekuwa ni lugha ya viongozi kusisitiza kuwa wanaomba Amani na Utulivu kila mahali kila kiongozi akisimama anasema amani na utulivu. Naomba nikumbushe tu kuwa amani ni tunda la haki. Haki inapokuwa imewekwa mahali pake hatuhitaji kugombana, hakutatokea fujo. Amani ya nchi hii

haitalindwa na vifaru vingi, haitalindwa kwa kuongeza Wanajeshi wengi, amani ya nchi hii itatokana na pale wananchi wanapopata haki zao, wananchi wanapotendewa haki, wananchi wanapopata huduma zile ambazo wanastahili kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, kwa muda mrefu tumekuwa na mfumo wa chama kimoja, pamoja na kuwa kwenye vitabu tumebadilisha, tunasema tuna mfumo wa vingi, kuna watu kwenye fikra zao hawaamini kuwa tuko kwenye mfumo wa vyama vingi kwa hiyo wanaona watu wengine ambao hawana imani kama ya kwao ni watu wanaoleta vurugu. Nataka niwakumbushe walioko madarakani kwamba *we are here to stay* na tuko hapa kwa mujibu wa Katiba, sisi siyo *intruders,* ni Watanzania, watawala mnatakiwa ku-*accommodate* mawazo tunayoyaleta hapa kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu. Aidha, *let us perish together as fools* au tuishi pamoja kama Watanzania na kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua watu wengine Kagame hawampendi lakini kuna nukuu yake moja ninaomba niisome. Anasema, *Africa is lagging behind and there is no good reason for that. We have everything to enable us to move from where we are, to where we want to go. It should be leadership commitment and transform the lives of our people across the continent".* Aliyasema haya kwenye *Summit* mwaka huu kwamba Afrika tuna kila kitu hakuna sababu yoyote kwamba tuwe nyuma katika maendeleo isipokuwa ni tatizo la uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbatia amezungumza hapa kuwa tunazungumza Mpango wa Maendeleo na Serikali ndiyo wanaosimamia mpango huo, angalia Mawaziri wako wapi? Spika jana amezungumza hapa, hawapo, ambao mnatakiwa mchukue mawazo yetu ili mkaya-*accommodate* kwenye mpango huu lakini hampo! Hatuelewi mko wapi, mko wawili, watatu, hamtoshi, hata mkijielezea hampo. Hii inaonyesha kuwa hampo *serious* na

ndiyo maana Serikali hii leo Waziri Magufuli anasema wenye malori wasimamishwe barabarani analeta hasara kwenye Taifa karibu shilingi bilioni ishirini, anakuja Waziri Mkuu anasimamisha, *the same government.* Waziri wa Maliasili anasema sijui watu wa Loliondo waondoke, anakuja Waziri Mkuu anasimamisha, *the same government.* Utawala wenu umefitinika. Hatuwezi tukawa na mipango mizuri wakati nyumba yenu hamjaiweka vizuri. Ndiyo maana nimesema *we are here to stay, either* mtu-*accommodate or let us perish together as fools* kwa sababu mnahitaji mawazo yetu tuko huku, hamwezi mkatupuuza. Mawaziri Vivuli na Mawaziri husika ambao mna dhamana wengi wanawaona Mawaziri Vivuli kama ni maadui.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Hamuwezi kukaa pamoja, tukashirikiana tukapanga mipango pamoja...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kaa chini, endelea Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hatuwezi tukakaa pamoja tukajadiliana kwamba hili ni Taifa la pamoja, tunaweka mipango ambayo haitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali hii ambayo imepewa dhamana kama nilivyosema, mlianza mwanzoni na Kauli Mbiu nyingi, mkasema Ari Mpya, Nguvu Mpya na kama vile haitoshi mkasema Kasi Zaidi. Ngoja niwaambie kitu kimoja, Kasi, *if you are heading the wrong direction is useless* kuongeza kasi. Mtu kama anapotea hum-*motivate* kuongeza kasi unampa *education* akae kwenye *drawing board* namna gani aende kwenye mwelekeo sahihi. Kwa hiyo, Kasi Zaidi mliyosema ni kasi ambayo imefanya uchumi wa nchi yetu ushuke chini badala ya kuendelea mbele. *(Makofi)*

*[MHE. MCH. P. S. MSIGWA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliyepita amesema tumebadilisha utaratibu wa *budget cycle* lakini matunda yake hayapo. Tunatoka kwenye Majimbo yetu huko mpaka leo hata nusu ya ile hela tuliyojadili mwaka jana haipo, leo tunakuja na mpango mpya, hii ni *business as usual.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika ukurasa wa thelathini, kwa mfano katika kipengele cha maliasili, Wizara ya Maliasili ni ya pili baada ya Wizara ya Nishati na Madini kuleta fedha za kigeni lakini hapa imewekwa utadhani Chuo cha Mkwawa, imeelezwa kidogo tu. Mipango ambayo haionyeshi mazingira ya kuiwekea Wizara ya Maliasili kuongeza utalii katika nchi hii, mazingira ambayo Serikali hii iliwawekea wawekezaji wale wa madini ambao kimsingi madini yanayochimbwa Tanzania mikono yake imejaa damu, kwa sababu kuna watu wamekufa na baada ya hapo wanaondoka wanatuachia mashimo. Wizara hii ya Maliasili, mazingira ambayo Serikali ilitengeneza kwenye Nishati na Madini, sioni mkakati mkubwa ambao mnaitengenezea Wizara hii ambayo uchumi wake ni *sustainable* ambapo wananchi watapata ajira, tutalinda wanyama wetu lakini mazingira hayo hayajatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwa mfano kwenye viwanja vya ndege, mmesema mnaweka mpango ambao ni *strategic*. Mmesema mtatengeneza kiwanja cha ndege cha Songwe, naunga mkono, pale ni pazuri. Mnasema kiwanja cha ndege Mwanza nakubaliana. Kuna kiwanja cha ndege Bukoba, kuna kiwanja cha ndege Kigoma, kuna kiwanja cha ndege Mafia, kuna kiwanja cha ndege cha Julius Nyerere, ninakubaliana na kiwanja cha ndege Tabora. Hata hivyo, mnawezaje kwenye mpango huu, Mkoa wa Iringa hapa katikati tuna mbuga kubwa ya wanyama na tunataka tukuze uchumi katika masuala haya ya utalii, tuna mbuga ya wanyama ya *Ruaha National Park,* kubwa na ni kivutio kikubwa, uwanja wa ndege wa Nduli mmeutenga. Hii ni mipango gani ambayo unaweza kuacha hapa katikati hakuna uwanja wa ndege na Mji wa Iringa ni moja ya vivutio,

ni Mji Mkongwe pamoja na historia ya Mkwawa, mnawezaje kuuacha katika Mpango huu wa Maendeleo kwa ajili ya kukuza uchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Wizara hii ya Maliasili ni ya pili baada ya Nishati na Madini. Haya ni mambo ambayo tulitegemea wataalamu mkikaa ni lazima tuwe na *strategic,* tuangalie ni *centers* zipi ambazo zitaongeza uchumi, una-*deal* kwanza na *primary contradiction* ndiyo unaenda kwenye *secondary* ambayo itajishughulikia yenyewe baada ya kumaliza hapa chini. Ya kwanza, niliyozungumza ni utawala bora. Utawala bora kama haupo, haya mambo yote hata tupange hayatakuwepo. Mtaongeza mabomu ya machozi, mtaongeza Maaskari, mtaongeza bunduki lakini kama wananchi hawatapata haki yao, watapiga kelele tu. Mtafanya mikutano mingi, Mheshimiwa Rais amewaambia kabisa kuwa mjiandae kisaikolojia, mtasema wembe ni uleule lakini utawachana wenyewe kwa sababu hampangi mipango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kwa ajili ya kutetea Taifa letu kwa pamoja. Nachotaka kusema hata kule Afrika ya Kusini waliandika kwenye makabrasha kuwa ubaguzi wa rangi umeisha lakini mioyoni mwa watu ubaguzi wa rangi ulibaki, *and this is what happening here.* Tunaimba utawala bora, tunaimba amani na utulivu lakini ndani ya watu wengine wana chuki, wakiona mpinzani wanamchukia, wanaona kama hastahili kuwepo mahali hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Msigwa. Namwita Mheshimiwa Vullu na Mheshimiwa Ntukamazina na Mheshimiwa Rita Mlaki wajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kwa kuwa nilijua nitachangia, nilimpigia simu Mwenyekiti wa *Council* ya Ngara nikimuuliza kama wameshapata fedha za maendeleo kwa mwaka 2013/2014? Akasema wamepata kidogo lakini akaniambia kuwa kwa miaka mingi hawajawahi kupata fedha za maendeleo, wamekuwa wakipata fedha za maendeleo chini ya 40%. Sasa hiyo inaonyesha kuwa tuna mipango mizuri lakini utekelezaji bado ni mbaya. Tatizo letu *we talk miles and act centimetres. We do not work the talks. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni nini? Kwa kuwa sasa tumeweka vipaumbele vizuri, Serikali ijitahidi kubuni na kutafuta vyanzo vipya vya mapato. Siku zote nimekuwa nikizungumzia kuwa sekta isiyo rasmi au *the informal sector is a sleeping giant* ambayo bado hatujai-*tap*. Najua kuwa mpango wa MKURABITA ulianzishwa ili kurasimisha mali na biashara za wanyonge ili waweze kutozwa kodi. Kwa hiyo, nashauri kuwa tuiangalie *informal sector* na Serikali isaidie MKURABITA ili iweze kufanya kazi yake ya kurasimisha mali na biashara za wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni makusanyo, tuimarishe makusanyo. Nimekuwa nikizungumza na *Commissioner General* wa *TRA*, Bwana Kitilya, namuuliza vipi makusanyo? Anasema wao wanavuka viwango ambavyo wanapewa na *Treasury* lakini inawezekana *Treasury* wanawapa viwango vidogo. Katika bajeti iliyopita, nilisema kuwa *the Treasury must put its house in order.* Nikaawambia wataalamu wa Benki Kuu na watalaamu wa TRA, ni watalaamu zaidi kule wale *Treasury* kwa sababu mambo ya *monetary policy* ambayo yanahusu *interest rates* pamoja na *Inflation* watalaamu wako Benki Kuu. Mambo ya *fiscal policy* ambayo inahusu mambo ya *Taxation* na mambo ya *Government spending* wataalamu wako *TRA*, pale *Treasury* wanatakiwawawepo wataalamu wa *fiscal policy* na

*monetary policy* ili waweze ku-*control* hata matumizi ya Serikali. Kwa hiyo, tuyaangalie makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni *Big Results Now*, hata bajeti iliyopita nilisema ili tufanikiwe na hii mbinu ya *Big Results Now* lazima tu-*address* zile *prerequisites. Prerequisites* maana yake ni nini? Ni kwamba watendaji wa Serikali bado mtizamo wao siyo mzuri, *we need change of mind set,* wawe na mtizamo chanya kusudi waweze kuwa watendaji wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuwezesha Tume ya Mipango. Mimi nina imani na Waziri Wasira, bahati nzuri *we went to the same very good school, American University,* ni mtalaamu sana. Aidha, nina imani na Tume. Tume ina watalaamu wa *fiscal policy na monetary policy* lakini nchi hii ni kubwa sana, kama tunawapa kazi ya utekelezaji pamoja na kuwa *think tanks,* ni lazima tujenge *capacity* yao, tuwawezeshe kwa kuwapa watalaamu wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma, ni jambo zuri sana na tunaweka mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji lakini *we must at the same time* kuhakikisha kwamba hii sekta binafsi inatozwa kodi ipasavyo kusudi tuweze ku-*finance* mradi wetu. Jambo muhimu ambalo nataka kulisisitiza, wakati tunazungumzia *private sector* kuwa mhimuli wa uchumi bado sekta ya umma iwe ni kiongozi wa uchumi, *micro-economic management* ni kazi ya Serikali. Kwa hiyo, *the Government must regulate the private sector* bila kuikaba roho. Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana tunapozungumzia *partnership* lakini Serikali ni lazima iwe ni kiongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo nimekuwa nikilizungumzia ni *procrastination,* kigugumizi cha kufanya maamuzi muhimu. Nilizungumza wakati wa bajeti iliyopita kuwa tulichelewa sana kujenga reli ya Isaka- Keza- Msongati- Burundi, Keza- Kigali Rwanda. Sijui katika hali hii ya mahusiano yetu na Rwanda kama hiyo reli tutaijenga kwa

*[MHE. D. A. NTUKAMAZINA]*

sababu hiyo reli ilikuwa ijengwe na nchi tatu ya Burundi, Rwanda na Tanzania. Ninachozungumzia hapa ni kwamba tuachane na *procrastination,* kigugumizi cha maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *equitable distribution of resources.* Nimelizungumzia wakati wa bajeti iliyopita kuwa tunao mpango mzuri lakini hizi fedha ndogo tulizonazo tuzigawe na kuangalia nchi nzima. Ngara iko pembezoni tusije tukaisahau kwa sababu iko pembezoni, *equitable distribution of resources.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wa wazawa, nilizungumzia sana katika bajeti iliyopita na pia nilizungumza na Katibu Mtendaji na Mheshimiwa Wasira kuwa katika mpango, msiwe mnasahau kuweka sera ya upendeleo kwa ajili ya wazawa. Wakati wa bajeti nilitoa mfano sera ya uzawa ya Malaysia. Juzi nimekwenda Zimbambwe, wana sera ya *indigenization* na *they are very serious about* sera yao ya *indigenization*. *South Africa they are very serious about black empowerment.* Hapa kwetu mimi sijaona the *exact equivalent* ya sera ya aina hiyo. *With all due respect* kwa Mheshimiwa Nagu, lile Baraza la Uwezeshaji lakini haitoi sera ya upendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kituo cha wagonjwa wa moyo. Hapa nimefurahi sana na ninaipongeza sana Serikali kwa kuanzisha kituo kizuri cha magonjwa ya moyo pamoja na figo. Serikali inatumia fedha nyingi sana kuwapeleka wagonjwa nje ikiwa ni pamoja na mimi nimekuwa nikienda India. Naomba tuimarishe hiki kitengo cha magonjwa ya moyo pamoja na figo ili tuokoe fedha za Serikali kwa ajili ya kupeleka watu nje ya nchi. Pia tuwape motisha Madaktari wetu ili wasitoroke kwenda Afika Kusini kutafuta *green pasture* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni nidhamu katika matumizi. Serikali ijitahidi, tuwe na nidhamu zaidi katika matumizi ili tuokoe

fedha za matumizi ya kawaida ziende kwenye matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni usafiri wa anga. Mimi nina imani sana na Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwamba ataifufua bandari na reli lakini naomba sana afufue *Air Tanzania*. Ni aibu kwa vinchi vidogo kama Rwanda inakuwa na ndege saba, *three Boeings* na mimi hizo huwa ninazitumia kwa sababu ni karibu na kwangu, Burundi wana ndege ndogo, Swaziland kanchi kadogo wana ndege. Sasa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, hii ni changamoto yako, tafadhali naomba tuwe na ndege yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nimemaliza, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Deogratias. Sasa namwita Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala wajiandae.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeusoma sana mpango huu kwa makini na ni mpango mzuri kusema ukweli lakini bado ninaona kuna tatizo kubwa katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini. Naona nipendekeze mwanzo kabla ya kusema hoja zangu ili nisikose nafasi ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali ianzishe kitu kinaitwa *Economic Intelligence Unit*. Nchi nyingi zilizoendelea zina hiki kitengo. Naomba Serikali waende hata Uingereza kwanza watizame jinsi wanavyofanya kazi, kuanzia mwanzo wa kupanga mpango wanakuwa na hawa watu. Hawa watu wanakuwa na *composition* ya Wachumi, Wahandisi, Ma-*geologist*, watu wa kilimo, Wahasibu na wataalamu mbalimbali ambao wataisaidia Serikali katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



mpango kuwa *realistic* na ule mpango. Wanafanya *feasibility study* kabla na unapouweka hapo, unajua kabisa huu mpango unatekelezeka. Baada ya hapo, hiki kitengo kinasimamia utekelezaji. Sisi tutajuaje kama walitekeleza, tutarudia tena mwaka mwingine na mwingine ambapo siyo kitu ambacho kinatusaidia na wanafanya tathimini kwamba mpango huu ulifika wapi. Naheshimu sana Tume ya Mipango pamoja na ngazi zote waliotengeneza mpango huu lakini tunaomba tuboreshe kwa kuwasaidia sana katika kuandaa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kusaidia sana katika mambo ya *growth rate* ya uchumi wa nchi yetu. Pato la Taifa limekua kwa 7%, ninatoa pongezi sana na vilevile *inflation* kushuka kutoka 10.6% mpaka kufikia 6.1% katika kipindi cha miezi tisa, ni kazi kubwa na nzuri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwa haraka kabisa mpango huu napendekeza uweje. Napendekeza mfumo au mpangilio wa huu mpango ubadilike kidogo. Nikianza na kipaumbele ambacho tulipewa, labda nichukue mpango wa 2012/2013 halafu niulinganishe na 2013/2014. Nikitizama mpango huo, kipaumbele cha kwanza kama viwanda, kule iliongelea kuwa tutajitahidi sana kushughulika na mambo ya Mchuchuma, tukaongelea mambo ya kuchoronga mashimo kule Engaruka kwa ajili ya magadi na kadhalika. Mwaka huu ikarudia lakini angalau ikatusaidia kidogo, ikaongelea kuwa tutahakikisha viwanda vilivyopo vinavyotumia rasilimali inayopatikana nchini angalau tunaweza kusindika mazao na kuongeza thamani ya hayo mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ufafanue zaidi, badala ya kusema tu kuwa tutasimamia usindikaji hebu tubadilishe sasa tuandike kuwa tutasimamia kwa mfano zao la ngozi, tamkeni tu mtasimamia kiwanda hata kimoja kama kile cha Mwanza ambacho kimekaa *idle* na kuna ng'ombe nyingi katika Kanda ya Ziwa na nchi yetu ikiwa ya pili au ya tatu kwa ng'ombe hapa Afrika. Tukitaje halafu tukifuatilie na

*[MHE. R. L. MLAKI]*

Serikali ihakikishe inafanya kila mbinu kuhakikisha kwamba kweli hiki kiwanda kinajengwa. Hali kadhalika na kusindika mazao ya kilimo. Tunaweza tukachagua mazao mawili, tukasema korosho labda na maharagwe, hebu twendeni kwa mpango unaotekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana nikumbushe kwamba tumepitisha Sheria hapa ya *PPP (Private Sector Partnership)*. Sheria hii itatusaidia, kama Serikali imesema inajitoa kufanya biashara, basi tutumie sheria hii, tujaribu kuhamasisha ili tuweze kuanzisha hivi viwanda. Ni muhimu sana nchi yetu ikawa na viwanda. Kwenye mpango huu sikuona kabisa wapi imezingatia uanzishwaji wa viwanda. Tumegusagusa tu, kweli tunaongelea kuchoronga mashimo, mpango huu na mpango unaofuata? Naomba tuliangalie suala hili kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kuongelea sana kuhusu reli kama wenzangu walivyofanya. Mpango uliopita umeongelea reli ya Dar es Salaam – Isaka - Kigali na upembuzi yakinifu umekamilika. Mwaka huu tumeongelea reli ya kati na tutajitahidi kujenga reli mpya. Mafanikio yalikuwa kwamba tumeweza kufanya upembuzi yakinifu wa gati namba 1 - 7 na vilevile tukasema kwamba tutajenga mpya. Naomba katika mpango wa sasa, tuweze kufafanua. Sasa hivi katika upande wa bandari ambao nimerukia, hii tuliyosema kwamba tutajenga zile gati ambazo tayari upembuzi yakinifu umefanyika, je, ndizo ambazo tutazirekebisha mwaka huu katika mpango wa sasa? Je, huo mpango wa bandari mpya itakayojengwa ni ile ya Bagamoyo ambayo tuliongelea mpango uliopita? Tufafanue zaidi, ndicho ninachotaka kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee sasa kuhusu utalii. Mpango mzima wa utalii ambao unasaidia uchumi wa nchi yetu, kweli niseme bila kusita kwamba haukuingia kwa kina. Mwaka jana tunaongelea jinsi ambavyo tutaingiza tozo ile inaitwa *bed night levy,* tunaongelea tutakavyonunua *furniture* za chuo, tunaongelea tutakavyopandisha *star hotel,* iwe *two star, three star* na

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kuendelea katika mpango? Angalau mwaka huu umeboreka kidogo unaongelea kuboresha vituo vya utalii lakini tuwe bado *specific,* tuseme tunataka kuongeza hoteli tano hata mbili basi kama tano ni nyingi na tusimamie zijengwe, angalau tutakuwa na uhakika tumesogea hatua moja kuliko twende katika hivi vitu ambavyo ni *supporting* badala ya kuwa *phyical* na kuhakikisha kwamba tumeweza kupata katika sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hizi *terminology* za kuzingatia, kuhamasisha, kuboresha hazipimiki. Kwa hiyo, tungejitahidi sana tuweke vitu *concrete* katika huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea kuhusu sekta ya madini. Utekelezaji wa mpango uliopita, umeelezea kukamilika ukarabati wa ofisi za madini. Mpango unasema jinsi utakavyofanya ukaguzi, mambo ya afya kwa wale wachimbaji wadogo wadogo, usalama wao, mara utajenga mtaro! Mpango wa mwaka huu angalau unaongelea kuimarisha rasilimali watu, kuendeleza shughuli za kuongeza thamani za madini na kadhalika. Hata hivyo, Watanzania wanachotaka kusikia, ni jinsi ambavyo mpango utamwezesha Mtanzania kushiriki katika biashara ya madini. Tusiwafanye Watanzania ni wachimbaji wadogowadogo, twende nao wachimbe kwenye migodi mikubwa. Madini pamoja na gesi, tuwatengeneze wafanyabiashara wetu wenyewe, inahitaji mitaji mikubwa lakini Serikali iweke mikakati katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kuona katika mpango jinsi ambavyo Serikali itaimarisha *STAMICO* ili iweze kuingia katika uchimbaji huu. Vilevile tungependa kuona jinsi ambavyo Serikali itavyoimarisha *TPDC* lakini kwenye mpango mzima mimi naona kama imeachwa na haionekani jinsi ambavyo itakavyotusaidia. Hii ni rasilimali ya nchi yetu na tunaitaka isaidie nchi yetu sana hasa kwa sisi wenyewe kubakia na *resource* kubwa ya hivi vitu. *(Makofi)*

*[MHE. R. L. MLAKI]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maeneo machache nimegusia katika mapendekezo na nachosisitiza ni mpango uwe *specific* zaidi na kuoainisha vitu vitakavyofanyika kwa uwazi zaidi. Aidha, mpango uweke vitu vichache kutokana na uwezo wa nchi na sio mambo mengi ambayo yatashindwa kutekelezeka kutokana na kutokuwa na fedha. Mwisho, mpango uwezekane kupimika. Kama kweli tumeweza kuutekeleza, tuepuke na hiyo misemo ya kuhamasisha na nini. Watu wa *Economic Unit* ambayo itakuwa *formed,* ndio waweze kupima na kutusaidia katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napendekeza mpango uwe na *continuation.* Kwa mfano, tukisema mwaka huu tuna kitu fulani, tuhakikishe mwaka ujao tunafuatilia sio tunaanza kingine kabisa na kile ambacho tulisema tutakifanya hatujakimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Selasini ajiandae Mheshimiwa Dokta Kigwangalla, Mheshimiwa Mabumba na Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mawazo yangu katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu, mpango ulio mbele yetu ni sehemu ya mpango ule wa miaka 25 ambao tuliupitisha hapa Bungeni. Huu tulionao sasa, ni awamu ya nne ya utekelezaji wa ule mpango wa awali. Mimi nilitegemea kwamba Serikali ingetuletea jedwali la utekelezaji kwamba ile awamu ya kwanza tulipanga mambo kadhaa haya na tumeyatekeleza kiasi fulani. Vilevile nilitegemea kwamba haya yaliyoletwa, yangekuwa na muda maalumu wa utekelezaji kwamba tunasema tutashughulikia reli, lini tunategemea tutakamilisha lengo hili. Yanapoletwa jumlajumla tu namna hii, wazo ambalo linaloingia ni siasa.

Wabunge wengi wanachokisema ni kwamba huu mpango una mambo mengi sana ambayo kulingana na uwezo wetu wa kifedha ni kazi sana, haiwezekani kutekeleza yote. Kwa hiyo, tutabaki tunadonoadonoa tu mwishoni tubaki hapahapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu la kwanza, mimi ningeshauri tuangalie katika huu mpango, yale mambo muhimu ambayo yanaweza kusaidia kupeleka uchumi wetu kwa haraka zaidi na tuyatekeleze hayo. Tumezungumza kwa mfano reli na hili litarudiwarudiwa sana na wachangiaji wengi kwa sababu reli ikitengenezwa itafungua bandari yetu. Reli ikitengenezwa barabara zetu zitalindwa, reli ikitengenezwa ajira zitaongezeka. Kwa hiyo, tuangalie ni namna gani kwa mfano, tunaweza kuchukua jambo hilo moja, tukalipa msisitizo na tukaweka muda maalumu wa kulitekeleza baada ya huo muda ni rahisi hata Bunge kuangalia kwamba mliahidi jambo hili kwa mwaka moja litashughulikiwa sasa tumefikia mahali hapa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha wazo hilo ambalo ni la ujumla. Mimi napenda sana kuzungumzia habari ya utawala bora. Tunaweza tukawa na mipango mizuri sana lakini utekelezaji wake ukawa mgumu kwa sababu ya hili suala la utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati tulilamikiwa kuhusu urasimu ndani ya Serikali kwamba wako wawekezaji au wapo wananchi ambao wana tamaa ya kuwekeza, lakini miradi yao inachukua muda mrefu sana kuidhinishwa. Imefikia hatua kwamba hata barua, kwa baadhi ya Taasisi za Serikali hazijibiwi. Sasa uzembe huu, unatukimbizia wawekezaji, wanakata tamaa wanakwenda kuwekeza nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hilo, kuna uzembe tu wa kutofanyia mambo kazi. Watu wanataka kuwekeza lakini inaingia hisia ndani ya watendaji labda mradi una rushwa kitu kama hiki, kwa hiyo, watu wanazungushwa tu ofisi hii, ofisi hii, ofisi ile matokeo yake watu wanakata tama,

*[MHE. J. R. SELASINI]*

wanakwenda kuwekeza nchi za wenzetu na mafanikio yanaonekana makubwa tu. Kwa hiyo, ningeshauri Serikali, kama kweli tunataka kwenda, mambo ya urasimu tuyaache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja alikuwa anatuambia kuna *supermarket* moja ilikuwa ijengwe hapa, lakini watu wakazungushana hapa wakaenda Uganda, Rais akaita wale wote wanaohusika wakakaa kikao, siku moja kila kitu kikamalliza. Sisi jambo moja litazungushwa kwenye maofisi mwaka mmoja, miaka miwili, hakuna uamuzi, hakuna anayezungumza, sasa hata hao wawekezaji tunaotaka waje hawatakuja, wanakwenda kwingine. Kwa hiyo, tuache urasimu na tufanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo pia la kutokuwa na *procurement plan* katika Wizara, Idara za Serikali na kadhalika. Watu walishajua kwamba kuna mpango wa utendaji lakini hakuna kitu chochote kinachoandaliwa. Kwa hiyo, wanasubiri mpaka fedha zinapopatikana ndio wanakurupuka kuanza kufanya kazi. Sasa mimi nashauri kwamba kuwe na huo mpango wa manunuzi kwa sababu *process* yenyewe ya manunuzi inachukua muda mrefu. Ni vizuri Wizara za Serikali, Taasisi za Serikali na kadhalika zikawa na *plan* za manunuzi mapema kabisa wakati tunasubiri upatikanaji wa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu utawala bora, viongozi na sisi wenyewe Watanzania hatufanyi kazi. Tunaenda kwenye nchi za wenzetu, tunaona wenzetu wanavyofanya kazi. Sasa haiwezekani, hatuwezi tukaendelea bila kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya ofisi za Serikali, ukiingia hukuti watu na unaowakuta hakuna majibu, hakuna uamuzi. Sasa ukija huku mtaani, mimi nashangaa hata fedha tunapata wapi. Nchi yetu ni kama imegeuzwa kuwa nchi ya walevi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mbunge Dar-Es – Salaam, hebu nenda Sinza unyoooshe mpaka Bunju ni baa

tu, watu wanakunywa kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa nane usiku, watu wanakunywa tu. Hawataki kufanya kazi wakati tunataka maendeleo, hili halitawezekana. Ni lazima ifikie mahali tubadilishe *mindset.* Serikali itengeneze utaratibu madhubuti wa kupima utendaji wa watumishi wake na ihakikishe kwamba sheria zilizopo zinafanya kazi sawasawa. Vipi watu wanakaa kutwa nzima wanakunywa hawafanyi kazi, halafu wanaachwa tu hivi? Watu hawa wanapaswa kufanya kazi ili nchi iendelee, kodi ipatikane na mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuzungumza ni kuhusu utalii. Nchi yetu ni ya pili kwa vivutio vya utali duniani baada ya Brazil. Hata hivyo, pato tunalolipata kwenye utalii sio sawasawa na vivutio tulivyonavyo. Nafikiri hatuweki mkazo na wa kutosha katika kutangaza vivutio vyetu na kulinda baadhi ya vivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu Mlima Kilimanjaro. Mimi naupigia kelele sana hapa Bungeni. Sasa hivi ukienda pale Kilimanjaro, hususani katika Jimbo langu la Rombo, watu wote wanakimbizana na wananchi waliopanda miti yao zamani na sasa wanataka kuivuna kwa ajili ya kujenga nyumba zao na shughuli mbalimbali wanakatazwa, wengine wanapigwa, wengine wananyang'anywa mbao zao. Nimeshasema kama ilivyo kwenye pembe za ndovu, pale mlimani, msitu ule wa asili, miti ile inavunwa usiku, malori yanashusha mbao katika ule msitu, hayana taa na mengine yanalindwa. Sasa hili linawaudhi wananchi! Unakwenda kumzuia namna gani mtu kukata mti aliopanda mwenyewe kwa miaka labda 20 na anautunza? Leo anataka kuezeka nyumba yake unamkatalia lakini msitu ule unavunwa, watu wanaona tu, watu wanaangalia tu. Sasa itafika mahali theluji pale mlimani itakwisha. Watalii hawaji kuangalia ule mlima kwa sababu ya urefu wake, wanakuja kuangalia theluji katika nchi za *tropical.* Sasa hili nimelisema sana, nisikilizeni jamani. Kama hii operesheni ya meno ya tembo inaendelea, pelekeni operesheni pale mlimani kuzuia miti kuvunwa na sio kukimbizana na mwananchi mmoja mmoja ambao kwa kweli

wanavuna kilicho chao. Watu wa Rombo hawafundishwi kupanda miti, ni desturi yao. Watu wa Rombo wanajua ukikata mti mmoja unapanda kumi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, pale Moshi pana kiwanja cha ndege ambacho kilikuwa kinaleta utalii pale kiurahisi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Selasini, ni kengele ya pili.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Msemaji anayefuata ni Mheshimiwa Dokta Hamisi Kigwangalla, hayupo. Mheshimiwa Mabumba atafuatiwa na Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi na Mheshimiwa Kombo.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano, kwa mapendekezo ya mpango ambao amewasilisha katika Bunge lake Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojadili mapendekezo haya, matarajio yangu yalikuwa kuonyesha ni kiwango gani utekelezaji wa bajeti tuliyoipitisha, Serikali imeweza kuitekeleza kwa kutoa rasilimali fedha, ili kutekeleza kazi ambazo Bunge hili zilipitisha hapa. Kwa bahati mbaya, mambo haya sijaona katika mapendekezo ya mpango huu. Waziri ameelezea baadhi ya sekta ambazo kwa maoni ya Serikali tumefanya vizuri. Ni kweli tumefanya vizuri kwa kudokoa sehemu ndogondogo sana kwa sababu mambo ni mengi, wakati wenyewe hautoshi. Maoni yangu, naona Taifa letu halijawa na vipaumbele ambavyo tunavijua kwamba tukivitekeleza hivi, uchumi wetu utakuwa lakini vilevile

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



wananchi wetu tutawaondolea umaskini na pia tutaweza kuongeza ajira kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano sekta moja hii ya kilimo ambapo Serikali ilikuwa na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Mimi nilitarajia kuona hapa tunaambiwa kwenye utekelezaji wa sera ya Kilimo Kwanza, nchi yetu imepiga hatua kiasi gani kuondokana na shida ya kuwa na uhakika wa chakula. Kuna maeneo tunapozungumza hapa yametajwa kwamba yana shida ya chakula. Sasa nilitarajia tuambiwe hapa, sera ya Kilimo kwanza katika Mikoa mbalimbali, Serikali imefanikiwa mambo gani? Mfano kwenye eneo moja la kuhakikisha kwamba tuna kilimo cha umwagiliaji, ni mabwawa mangapi yamechimbwa ili watu wetu wasitegemee tena kilimo cha mvua ambacho hakina uhakika? Naelewa Mikoa ile ya Shinyanga, Simiyu, Tabora, kilimo chao ni cha kutegemea mvua. Wanatumia nguvu nyingi sana lakini mavuno ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeambiwa kwenye sekta ya barabara kwamba tumefanikiwa sana. Mimi nadhani Serikali ingeweka nguvu zake kutatua kero katika Miji mikubwa hii ambayo leo *traffic jam* inasumbua hata uzalishaji wenyewe unashuka. Tunaambiwa barabara za kupita juu, *fly overs* Dar-es-Salaam, utekelezaji wake ukoje? Leo Dar-es-Salaam imekuwa ni karaha sana, eneo la kwenda kwa saa moja unakwenda kwa saa tatu au nne, uzalishaji uko wapi? Wafanyakazi wanaishi katika hali ya mateso kwa sababu analazimika afike asubuhi saa moja na nusu, kwa hiyo, aamke saa kumi na moja au saa kumi na anapaswa kuondoka saa tisa na nusu anafika kwake saa tano usiku. Nilitarajia kuona ni namna gani kwenye mpango huu, kero hii kwenye eneo la barabara, kwenye Miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Tanga, Serikali inatuambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye eneo la reli, taarifa ambayo imetolewa hapa, mimi sijaifurahia sana. Kama kweli tunataka kujenga uchumi imara na endelevu na wa kasi, ni lazima Serikali iangalie reli. Mfano sasa hivi wakati

*[MHE. S.M. MABUMBA]*

wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanapoitenga Tanzania basi kumbe ni wakati muafaka Tanzania kuimarisha reli mpaka Kigoma wananchi wa nchi ya Burundi na DRC ambao kwa kweli kama sisi tutaweka miundombinu mzuri, watatumia na hata hawa ambao wanajaribu kuunda ushirika mwingine, wao watakuwa wamepotea sana kwa sababu haiwezekani uzunguke kama tulivyoambiwa kilomita mia tisa za ziada. Mtu wa Burundi hatatumia hiyo *alternative* nyingine, mtu wa DRC hatatumia hiyo *alternative* hiyo nyingine, hawa ambao wanataka kwenda kule ni kwa ushabiki lakini uhalisia haupo, kibiashara hailipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yangu iimarishe reli. Hata hizi barabara ambazo tunajenga kwa gharama kubwa sana, tutaweza kuzilinda. Waziri wa Ujenzi alisema hapa, uzito wa malori yanayopita kwenye barabara zetu wakati mwingine ni mkubwa sana, kwa hiyo, usalama wa barabara haupo. Kwa hiyo, kwenye eneo hili, naomba Serikali yetu ijenge sasa reli kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunanufaika na fursa ambazo zipo DRC na Burundi lakini pia wananchi wa maeneo yale ya Kigoma na Tabora.

Mheshimwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Mpango wa Maendeleo, vilevile ni lazima tuzungumzie habari ya ulinzi na usalama wa nchi yetu. Sijaona kwenye kitabu hiki wapi wanaelezea habari ya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kwamba hata huu uchumi tunaotaka kuujenga, tuweze kuufanikisha. Kwa mfano, usipowekeza kwenye ulinzi na usalama, ambapo sekta ya utalii kutokana na upana wake inaweza kuchochea sana ukuaji wa uchumi wetu kwa sababu sekta hii inatoa ajira na unaleta fedha za kigeni. Naomba sana kwenye mpango huu, suala hili la ulinzi na usalama wa nchi yetu na hata haya matukio ambayo yametokea leo, watu wengine ndani ya Jamhuri ya Muungano tunatembea hatuna uhakika na maisha yetu. Upande wa pili wa Zanzibar kule ambako kila siku watu wanamwagiwa tindikali, watu wanadhalilika, mpango wetu huu kwa sababu naamini ni moja katika *mandate* ya Muungano kuhakikisha kwamba amani inapatikana katika mipaka yote. Sisi kule tunamwagiwa tindikali, maisha yetu

yapo hatarini, tuna hofu, hatuna amani. Sitaki kusema sana kwa sababu wote mmeona Padri yule mtu mzima miaka sitini alivyodhalilika, leo tunaambiwa hata kuona haoni, jicho lake limekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni lazima iwekeze kwenye amani, kwenye usalama, kwenye ulinzi, vinginevyo unapowavamia watu wenye ushawishi katika jamii, mfano sisi hapa tunaitwa Waheshimiwa, Ubunge wetu ni miaka mitano, baada ya miaka mitano wananchi wanaweza wakapoteza ladha ya kukuchagua tena, ukawa mwananchi wa kawaida, lakini viongozi wa dini wanakufa na uongozi wao. Kwa hiyo, wana ushawishi mkubwa katika jamii, ni lazima tuwalinde ili tuhakikishe kwamba wanasaidia pia kushawishi watu wanaowaongoza kuunga mkono sera zetu. Tunapowaachia wakawa wanadhalilika, haitusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo moja ambalo Waziri amezungumzia kuhusu viwanja vya ndege. Nipongeze kazi imefanyika pale Kigoma lakini kama nilivyosema, uwanja wa ndege wa Kigoma tuupanue uweze kuhudumia DRC na Burundi. DRC na Burundi wawe washirika wakubwa na Tanzania na wengine wata-*regret* katika maamuzi yao na wakiendelea, fursa ya DRC inatosha sana kuachana na wengine ambao wanaibeza Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana kengele ya pili.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Ya kwanza!

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa nitamwita Mheshimiwa Modestus Kilufi na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo ajiandae.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupewa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzungumzia uhai wa Taifa kama Taifa halina uchumi mzuri. Mipango yote hii inategemea uchumi mzuri. Nimefurahishwa sana na mipango mingi ambayo imeoneshwa humu na mimi niseme kwamba tu watu wazuri sana katika kupanga lakini napata taabu sana tunapokuja kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo rasilimali nyingi sana wala si za kusema tubuni, tunavyo vyanzo vingi sana vya kiuchumi ambavyo vinaweza kusababisha uchumi wetu ukapanda. Tatizo tulilonalo ni namna gani tunasimamia vyanzo hivi, ni namna gani tunajipanga vizuri kucheza vizuri na wawekezaji ambao tunasema sasa hivi tuelekeze nguvu zetu kwenye sekta binafsi ili iweze kusaidia kwenye utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo au kuchangia kwenye miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kwamba leo Wabunge tupo hapa tunachangia lakini napata taabu kuona kwamba sijui ni nani anayeratibu haya tunayoyasema kwa sababu ukiangalia idadi ya Mawaziri waliopo, kwa kweli hairidhishi. Sijaelewa hapa tunapozungumza, anayeratibu ni nani kwa sababu leo hapa Serikali imetuletea mpango tunatakiwa tuujadili lakini wale waliotuletea mpango ili tujadili waratibu na wakafanye vizuri zaidi, hawapo, sasa inakuwaje? Nadhani hapa kuna utani kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi wameyasema wenzangu, lakini siku zote nimekuwa nikizungumza humu Bungeni kwamba nchi hii haina miiko ya kulinda uchumi wa nchi, hatuwezi kwenda hata kidogo, haiwezekani! Tunajifunza kwa wenzetu ambao wameendelea wana miiko. Nchi gani ambayo watu wanafanyakazi bila woga. Haiwezekani kabisa Waziri anajua tunajadili hapa mambo ya msingi ambayo anatakiwa arekebishe hayupo. Kwani kama ni safari kwa nini zisipangwe wakati ambao siyo wa kipindi cha Bunge?

*[MHE. M. D. KILUFI]*

Unapangaje safari wakati Wabunge wanaendelea kuchangia hoja na wewe tunakutegemea utusaidie kurekebisha, wapo wachache tunawashukuru mliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo mengi ambayo yanatokana na uwajibikaji. Nchi hii haiwezi kwenda kama Serikali haitasimamia watendaji mbalimbali ambao wanatakiwa watekeleze miradi hii na mipango hii mizuri ambayo imewekwa mezani kwetu. Nina mifano mizuri tu ya kuonesha ni namna gani hatupo *serious* katika kusimamia uwajibaki na utekelezaji na usimamizi wa mipango mbalimbali ya nchi yetu. Kwa mfano, hivi Halmashauri nyingi ambazo zimesababisha upotevu wa pesa nyingi na tukategemea hatua zitachukuliwa kwa watu waliosababisha upotevu huo lakini mpaka leo wanasuasua, hawachukuliwi hatua, tunategemea nini tupeleke fedha zetu huku kwa ajili ya mipango ya maendeleo. Mfano mzuri ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbarari, imepata hati chafu na nchi nzima tunasemwa. Mimi nimekuwa nikisema kila siku juu ya ubadhirifu uliopo pale lakini leo waliochukuliwa hatua ni kichekesho, ni watu wawili, watatu tu, wengine wapo wapi waliopoteza mabilioni ya fedha za maendeleo ya wananchi wa Mbarali? Kitendo hiki cha kutokuchukua hatua kwa watu wanaofanya vibaya nchi hii haiwezi kuendelea hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, China tunasema sasa hivi inaenda vizuri, lakini ina mipango mizuri ya kudhibiti wale wote wanaofanya vibaya. Wabunge kama tungekubaliana, ilitakiwa tuwe na sheria kali ya kusimamia uchumi wa nchi hii ikiwa ni pamoja na kuwapima Mawaziri utendajikazi wao, kwa sababu Waziri angeendelea kuwa Waziri kutokana na kuendelea na ku-*perform* kwa Wizara yake. Sasa wewe unaongoza Wizara, Wizara inaenda vibaya unaendelea kuwa Waziri, unafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, ni siku mbili, tatu hizi tumeshuhudia wafugaji wakipata shida na kuhangaika katika nchi hii, lakini Wizara ipo na Waziri yupo! Hivi hawa wafugaji wanawezaje kuhangaika hivi? Hivi tuseme Serikali imeshindwa

kubuni ni namna gani mifugo inaweza ikawa ni chanzo cha uchumi katika nchi hii? Kwa nini tuache wafugaji wanahangaika tu, wanapata shida, wanakuja hapa wanalialia. Haya tunaambiwa kuna ng'ombe zao zimeshikwa zipo mahali fulani lakini mwenye kutoa kauli kwamba wapigwe faini, waachiwe tutengeneze utaratibu mzuri hayupo, ng'ombe zinauzwa. Wafugaji wapo hapa na Serikali ipo hapa inaona. Ushauri wangu kwa Serikali yangu ni kwamba operesheni ni nzuri na nia yake ni nzuri, lakini kitendo kinachofanyika na kuona watu hawa wanahangaika, si jambo jema hata kidogo. Tunajivunia nini kama mifugo ambayo tayari wafugaji wetu wanaitunza tumeacha inaachwa hovyo ovyo, tunawafilisi watu badala ya kuweka utaratibu mzuri ambao utawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vyanzo ambavyo mimi nilitegemea kama Serikali itaweka mipango yake vizuri, mifugo ni chanzo kizuri cha uchumi wa nchi hii. Badala ya hizi ranchi za Taifa kugawiwa kwa wawekezaji, tungeweza tukawapa wafugaji hawa na wakapewa masharti yaleyale wakaweza kumudu kutimiza ili kusudi nchi hii kama tunategemea ranchi kama sehemu ya uchumi basi tutapata kutoka kwa wafugaji wetu. Tunashindwa nini leo kutenga maeneo ya wafugaji hata wakayalipia kuliko ilivyo sasa wanahangaika. Tukaboresha miundombinu ya maji na kadhalika ili wafugaji hawa nao wakawa ni sehemu ya pato la Taifa. Hata hivyo, tumewaacha wanahangaika ni chanzo kizuri cha mapato, ni afadhali hata kama tungesema wawe wanalipia ile mifugo lakini tuwatengee maeneo mazuri kuliko kuwaacha wanavyohangaika hivi sasa. Hicho ni chanzo ambacho naona hatujakiwekea mikakati mizuri ambayo ingeweza kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuimarisha viwanda ili kuzalisha ajira nyingi kwa Watanzania wengi ambao hawana ajira. Tunahitaji kuimarisha kilimo ili kusudi vijana wengi na wananchi wengi wa Tanzania ambao wamejiajiri kwenye kilimo waweze kulima kwa tija. Tunazungumza Kilimo Kwanza sijaona mkakati kama ambavyo wenzangu wamesema labda ni kitu gani

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kinafanyika au tunatarajia kifanyike ili tuweze kutengeneza *scheme* nyingi za umwagiliaji na vijana waweze kujiajiri huko. Sijaona mpango huo ambao unaonesha haya, nimeona tu kwamba kuna maeneo fulani yataendelezwa kwa kilimo, lakini ni mikakati gani tutaitumia hii nguvukazi kubwa ambayo imekaa tu Mjini, vijana wanazurura ili waweze kwenda kujiunga kwenye miradi hiyo muhimu, viwanda havipo, mimi siwalaumu, wafanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hatujaweka mipango mizuri ya kuweza kujiajiri kwa hawa wananchi wanaozurura mjini. Nguvukazi kubwa hii ambayo inakaa haina kazi kubwa, mtu anauza tu vifulana, anatembea siku nzima unategemea alete uchumi kwenye Taifa lake, atatoa wapi, kama hatujampa mipango mizuri? Hawa vijana hawapendi kuzurura, lakini tungewekeza kwenye kilimo na mimi nasema kwenye kilimo kuwaachia wawekezaji peke yake bila sisi kuweka nguvu yetu na kuonesha mipango yetu bado hii sekta haitaweza kutukomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tumeweka wawekezaji lakini hatujaonesha ni namna gani wawekezaji watashirikiana na wananchi wa maeneo yale ili wananchi wale nao waweze kunufaika na uwekezaji huo. Tunategemea wawekezaji kuwepo mahali pale wananchi wa maeneo yale nao wanufaike na uchumi wao upande, lakini hatujaweka miiko wala taratibu zozote. Mwekezaji anaambiwa unawekeza hapa endelea, matokeo yake ni ugomvi na wananchi wa maeneo yale, ni taabu, ni kero, wale wananchi wanaona kama wamepelekwa jehanamu katika eneo lao ambalo walikuwa wanaishi kwa raha na mustarehe. Je, huu ni uwekezaji kweli? Je, asilimia wanazochangia Serikalini ni kiasi gani? Tumefanya utafiti kiasi gani kuona mafanikio ya uwekezaji katika nchi hii? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana, ni kengele ya pili. Sasa namwita Mheshimiwa Kombo.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Mpango wa Maendeleo ya Taifa, ni chombo ambacho kinazihusu Wizara zote za Serikali. Mimi nilitegemea na kutazamia kwamba kwa sababu tunajadili masuala ya mpango, basi Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu wao pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara wangekuwepo katika kujadili suala hili. Hata hivyo, kwa sababu tuna utamaduni wa kusema na kusoma bila ya kutenda, ndiyo leo ukaona kwamba Mawaziri na Manaibu waliopo ni wachache na si hivyo tu hata Makatibu Wakuu wa Wizara husika hawapo, pamoja na agizo la Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niseme kwamba tuna sera inayosema kwamba Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi. Kama Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi, tujiulize ni kwa kiasi gani tunaitumia ardhi yetu katika masuala ya kilimo? Tumepeleka kipaumbele gani katika masuala ya kukuza kilimo? Tuna hekta ngapi za kilimo? Mimi nasema kwamba bado tamko la Tanzania kwamba ni nchi ya wakulima na wafanyakazi litaendelea kuwa ni tamko ndani ya vinywa vyetu na ndani ya maandishi lakini hatujaweza kutekeleza sera ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika masuala ya ufugaji ambayo wengi wameyaongelea, nakubali kwamba Tanzania tuna utajiri mkubwa wa mifugo. Hata hivyo, mpango huu haujaeleza ni kwa kiasi gani Tanzania tuna bahari, mito na maziwa ambayo yana samaki wengi, tuna wavuvi wengi tu, lakini suala hili halijaguswa. Niseme kwamba hii ni kinyume na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa sababu sekta ya uvuvi ipo kwa asilimia kubwa ndani ya nchi yetu. Tuna maeneo makubwa ya bahari, tuna samaki wengi, tuna maziwa mengi yenye samaki wengi, tuna mito mingi yenye samaki wengi, je, tunazitumia vipi rasilimali hizi kwa uchumi wa Taifa? Kama si maneno ya usanii yaliyomo kwenye vitabu, rasilimali hizi tunazitumia vipi? *(Makofi)*

[MHE. K. K. KOMBO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wameendelea katika masuala ya ufugaji wa samaki. Ni mara nyingi sana kumsikia Mheshimiwa Kitandula akizungumzia masuala ya ufugaji wa samaki, lakini yanazungumziwa humu yanawekwa kwenye madroo ya meza, hayafanyiwi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wataalam wengi wa uvuvi. Je, hawa wamepewa nyenzo gani za kuweza kufanyia kazi. Wamepewa uwezo gani wa kuweza kuwaelimisha wenzao ili tuondokane na umaskini. Wamepewa uwezo gani wa kuwaelimisha wenzao ili waweze kufanya kazi kwa kujiajiri katika Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanaachwa na hayashughulikiwi. Sasa Mpango huu ni mzuri na nawashukuru Kamati ya Bajeti na pia Kambi ya Upinzani kwa namna ambavyo waliweza kuwasilisha hoja zao. Hoja zao zilikuwa na msingi. Kamati ya Bajeti hoja zao zilikuwa za msingi na itabidi Wizara izifanyie kazi, isiwe wameshatoa kazi, lakini ikachukuliwa kama kinanda kinachopigwa kwenye taarabu. Ikimalizika taarabu na kazi imekwisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mpango ulipaswa kuangalia mabadiliko ya tabianchi kwa uchumi wa Taifa la Tanzania. Je, Mpango wa mwaka 2014/2015, umeangalia angalia vipi athari za mabadiliko ya tabianchi kwa uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuna suala zima la viwanda. Niseme kwamba, viwanda ni sehemu ya ajira kwa vijana, lakini tujiulize hivi kweli viwanda vipo? Viwanda ambavyo vilikufa vimefufuliwa? Vinafanya kazi? Vimeajiri vijana wangapi? Kwa sababu viwanda vitakapokuwa hai na vikawa vinafanya kazi, vitaweza kuajiri vijana wetu wengi na kwa hivyo lile suala tulilosema la vijana kukaa vijiweni litaweza kuondoka kwa kiasi kikubwa na vile vile tutaweza kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ni suala la barabara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kombo. Sasa namwita Mheshimiwa Rage.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Rage, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kikwembe na Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza, napenda kupongeza mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2014/2015 na vile vile…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rage, hebu hamia kwenye *microphone* nyingine.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya kuunga mkono napenda vile vile kuipongeza Serikali yangu ya CCM kwa kazi nzuri iliyofanya katika kuhakikisha kuna mabadiliko katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika maeneo makubwa manne; maji, reli, kilimo na umeme. Napenda kuanza na reli kwa sababu tumekuwa tunaongea kwa muda mrefu sana katika Bunge letu hili. Tunapenda kuwakumbusha tu Serikali yetu kwamba, sasa wabadili na kuongeza *speed* ili waweze kwenda mwendo wa kasi. Bahati nzuri Waziri mwenye dhamana ya masuala ya reli Mwenyezi Mungu amekuja na hekima mpya na nguvu mpya, lakini nadhani

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*


tusipomwezesha kifedha, nguvu zake na hekima yake itapotea bila sababu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kwa zaidi ya miaka 25, tulikuwa hatujawahi kuthubutu kununua mabehewa. Mheshimiwa Waziri huyu kwenye hotuba yake ya bajeti ametuhakikishia tutapata mabehewa 15 ya vichwa vya treni na tutapa mabehewa 276 kwa ajili ya kubeba mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma hii kama itatekelezwa, kwa bahati mbaya ilikuwa kwenye Mipango wa Mwaka 2012/2013, lakini haikutekelezwa. Mimi nipo kwenye Kamati ya *PAC*, taarifa tuliyokuwa nayo ni kwamba, malipo ya awali yamelipwa wiki chache tu zilizopita, kwa maana hiyo mabehewa haya hayatafika nchini mpaka mwakani tena, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuhakikishia, Mwenyezi Mungu akijalia mabehewa haya tukayapata, uchumi wetu utabadilika kwa sababu mizigo mingi itaweza kubebwa kwenye reli na malalamiko ambayo kama uliyasikia jana kwa Waziri wa Ujenzi barabara zetu zimeanza kuharibika ni kwa sababu tunatumia sana barabara kuliko reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Benki Kuu zinaonesha kwamba, zao la tumbaku ndilo linaingiza fedha za kigeni kuliko zao lolote, lakini mkulima hafaidiki kwa sababu analipa gharama za kusafirisha kwa njia ya barabara tumbaku kwenda Morogoro, mbolea kutoka Dar es Salaam kuja Tabora au katika mikoa mingine, yote inakwenda kwa barabara. Kwa hiyo, gharama hii itakuwa kubwa. Lakini endapo mabehewa Dkt. Harrison Mwakyembe tukiyapata, gharama ya usafirishaji itapungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea suala la maji. Vita ya tatu ilishakwisha. Watabiri wanatabiri kwamba kama itatokea vita ya nne basi itatokea kwa ajili ya maji. Sijui kwa nini Serikali yetu katika Sekta hii bado inazembea.

*[MHE. I. A. RAGE]*

Nina ushahidi wa kutosha kabisa na nitatoa mfano wa mradi wa *KASHIWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu unanikera sana, una uwezo wa kuzalisha maji milioni 1.2 *litres* kwa siku moja, lakini maji yanayotumika sasa ni lita milioni 17 tu asilimia 9.2. Asilimia 91 ya yale maji yamekaa *idle* pale Ihelela, kwa nini? Kwa kipindi cha miaka mitano sasa Serikali imepitisha pesa zaidi ya bilioni 4.7 kwa ajili ya kulipa gharama za umeme na kuendesha mradi wa *KASHIWASA*. Kinachohitajika maji yamefika Kahama wapelekewe wananchi wa Maswa, Bariadi, Nzega, Igunga, Tabora, Urambo na Sikonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *KASHIWASA* watapata kuuza maji lita milioni 57 kwa siku moja. Maana yake nini? Sasa hivi *KASHIWASA* wanauza *cubic meter* moja ya maji shilingi 505. Lakini ukiweza kupeleka maji haya yakafika mpaka Tabora maji yatakuwa shilingi 249. Je, uchumi haujabadilika hapo? Utakuwa umempa mwananchi nafuu na Serikali itapata nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme; Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Wizara hii tangu imefanyiwa mabadiliko, Mawaziri wale watatu wanastahili sifa kubwa sana. Ni aghalabu sasa hivi kupata umeme wa masaa machache, umeme uko *throughout now. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tupate uhuru miaka 52 mpaka mwaka 2005 wananchi waliokuwa wanapata umeme ilikuwa ni asilimia tisa tu, lakini sasa wananchi ambao wanapata umeme wa uhakika inafikia takribani asilimia 26 mpaka 28. Kwa maana hiyo, kuna uwezekano kabisa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kabla ya 2015, asilimia 45 mpaka 50 ya wananchi kupata umeme itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ninazo taarifa za uhakika kwamba, sasa hivi *pipes* zimeanza kuwekwa kutoka kule inakotoka gesi kwenda Dar es Salaam. Kwa uchunguzi niliofanya, nimegundua kwamba, bei ya

umeme itashuka kutoka senti 45 za Marekani mpaka kati ya senti sita mpaka 10 za Marekani. Hii maana yake nini? Maana yake uchumi wa nchi utabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa rai kwa Waziri mwenye dhamana, atuletee mabadiliko ya Sheria ya *Road Toll.* Reli wananunua mafuta mengi sana. Sasa wao wanatakiwa tuwasamehe zile pesa wanazolipa kwa ajili ya *Road Toll* zingerudi kwenye reli ili tuimarishe reli ya Kati na reli zingine. Kinyume chake habari ya mipango au kuendeleza uchumi wa nchi hii, tutakwama tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kushauri kwamba, Wizara ya Fedha sasa ibadilike katika kutoa maamuzi yake inapokuwa Bunge hili linaidhinisha Bajeti na watoe pesa katika miradi ambayo tumeshapitisha ili tuweze kutekeleza kwa wakati unaotakikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa Kampuni moja inaitwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rage.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mpango huu mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Namwita Mheshimiwa Dkt. Kikwembe na Mheshimiwa Mwijage ajiandae.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi kijacho cha mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nitoe pole kwa ndugu zangu wana Katavi walioko Wilaya ya Mlele, Kata ya Kibaoni, kutokana na operesheni hii

inayoendelea ya upambanaji wa majangili; tumepoteza mwanakijiji mmoja ambaye amepigwa risasi na Mheshimiwa Diwani ambaye alikwenda kwenye msiba huo, yalimkuta masahibu na sasa hivi yuko hospitali anaumwa. Namwomba Mungu ampe afya, arudi kuendelea na majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda niishukuru Serikali kwa namna ambavyo imeweza kujitahidi kupanga mipango ambayo mara nyingi tumekuwa tunaiona na inatuletea mabadiliko katika nchi. Sisi wote ni mashahidi, tumeona namna ambavyo Tanzania yetu inabadilika, hasa sisi tunaotembea kwa barabara, tunashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia upande wa viwanja vya ndege tumejenga. Nashukuru Mkoa wetu wa Katavi tumepata kimoja. Japokuwa katika mpango huu vinaonekana kama vimekamilika, hapana. Niiombe Serikali katika kupanga mipangilio hii, sikatai kupanga ni kuchagua, lakini tupange mipango ambayo nafikiri tutaitekeleza kwa wakati unaofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa sana na huu utaratibu wa kusubiri, tukusanye kwanza, tunapanga, tunakusanya halafu ndiyo tunaanza kutekeleza. Kitu ambacho sidhani kama ni sahihi katika kupanga. Kwa hiyo, lazima Serikali ikubali sasa kubadilisha mfumo wa bajeti tutoke kwenye *cash budget* twende kwenye *capital budget*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ngumu sana kupanga kitu ambacho sinacho mkononi. Kwa mfano, nasema kwamba nikipata milioni 10 ndipo nitafanya moja, mbili, tatu. Je, nisipopata ama nikapata robo. Ina maana yale malengo mengine sitayatekeleza. Kwa hiyo, naishauri Serikali kupanga mipango kutokana na rasilimali tulizonazo ili hii miradi ambayo tunapanga kuitekeleza, tuitekeleze kwa wakati na tuweze kuimaliza na wakati ujao ndipo tuweze kupanga kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niungane na ndugu yangu Rage aliyeongelea suala la reli. Kwa kweli reli ndiyo mkombozi, tukubali tusikubali. Ukweli ubaki kuwa ukweli.

Hatuwezi kusema tutaendelea bila reli. Kwa hiyo, reli ya kati lazima tuipe kipaumbele. Tukubali tusikubali, Serikali ifanye juu chini kuhakikisha kama tulivyoongea kwenye bajeti iliyopita, basi mpango wetu unakwenda vile vile na tujipime katika kutekeleza hii miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hata Mwalimu darasani, ukiwa darasani huwezi kusema leo nitafundisha hapa kidogo hapa kidogo, hapa kidogo, hapana. Utakuwa na malengo ya jumla *and then* utakuwa na malengo mahususi kwamba, lengo langu la jumla ni hili, sasa ndani ya dakika hizi nitatimiza hiki. Siyo ndani ya dakika hizi nitatimiza moja, mbili, tatu, nne, tano, haiwezekani! Kwa hiyo, lazima tufike mahali, tuangalie namna gani tunapanga mipangiliio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye elimu. Natoa mapendekezo katika mpango huu, tuwekeze vya kutosha kwenye elimu. Tumeongelea suala la rasilimali watu kuwaendeleza, tunawaendeleza vipi? Tunawaendeleza vipi, kwamba tutaendelea kuwaongezea mafunzo, ama semina, watumishi au wafanyakazi katika Sekta labda ya *Uranium* au kwenye makaa ya mawe, kivipi, kama kwenye elimu ya msingi na sekondari hatujatengeneza. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kama kweli tuna nia ya kuikomboa nchi yetu lazima tuwekeze kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekeza zifanyike jitihada za makusudi katika kuhakikisha elimu ya sekondari au ikiwezekana tufanye basi kutoka elimu ya darasa la kwanza mpaka kidato cha nne iwe elimu bure na iwe ni ya lazima. Sasa tuwekeze kwenye maabara tuwekeze kwa Walimu, tuwekeze kwenye nyumba za Walimu, maana yake mwanafunzi atapataje elimu bora na tutaendeleaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwaje na rasilimali ya watu ambao tunasema wanakwenda kwenye gesi, ambao, jamani, si tunataka haya makampuni yaje na wataalam

wao? Ndio maana yake? Sasa sisi tutaendelea kuwa vibarua kwenye yale makampuni mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba katika hilo, Serikali iliangalie sana, namna ya utekelezaji wa miradi. Sheria zipo, wazembe wachukuliwe hatua, kwa nini tunaonekana aibu? Ni kwa nini tunaoneana aibu? Wanaozembea kutekeleza wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tunaweza tukawa tunalaumu wasimamizi, kumbe ndio haya haya tunayosema, kwamba, tunapanga kabla ya kuwa na pesa. Pesa inachelewa kufika, tunalipa mishahara watu wa kusimamia miradi kabla ya pesa za miradi hazijatoka, maana yake ni nini? Maana yake ni hela ya mishahara inaendelea kwenda, lakini hela ya miradi haipo. Tunalipa watu wasiofanya kazi; kwa hiyo, tunazidi kupata hasara, badala ya kusonga mbele tutazidi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hilo naomba sana. Pia, naomba Kitengo cha Usimamizi na Ufuatiliaji kiimarishwe, hii biashara ya kuwa mnatoa hela mnaacha, haiwezekani hata kidogo. Narudia tena, hapa majibu yamejibiwa kwa mfano, swali la Mheshimiwa Kandege lilivyojibiwa, kwa kweli, hatuwatendei haki wananchi wanaosikiliza; naomba Serikali ijaribu kutoa maelezo ya kina, pia kwenye masuala ya msingi ambayo wananchi wanauliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, tusisubiri kuja humu ndani na kuuliza miradi imefikia wapi? Niliwahi kuuliza kwenye kikao, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Niliwahi kuwauliza watu wa *TANROAD* Makao Makuu; nikauliza, hizi taarifa mnazileta, mnakwenda kwenye eneo ama mnaletewa tu makaratasi Wizarani *and then* mnakuja kutusomea hapa? Wakaelezaeleza pale, kwa sababu mimi sio *engineer* ilibidi nikubaliane nao tu. Sasa ndio haya tunayosema kwamba, ni lazima sasa tuone namna gani tunawekeza kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirudi niipongeze

*[MHE. DKT. P. W. KIKWEMBE]*

Serikali kwa kuanzisha mkongo huu wa Taifa wa Mawasiliano ambao unahusisha pia mambo ya *TEHAMA* ambao kwa wakati mwingine itaenda moja kwa moja kuunganisha kwenye mashule. Niiombe Serikali, vile vifaa ambavyo ni wezeshi kwa hii *TEHAMA,* kwa mfano labda, mambo ya *internet, package* za *data* na nini, nafikiri vile viwezeshi vya hii teknolojia, viweze kupunguziwa kodi ili kurahisisha au kupanua wigo wa watu wengi kutumia huduma hiyo na wewe ili uweze kukusanya kwa wingi kuliko ukiweka kodi kubwa. Ina maana watumiaji watakuwa ni wachache na mapato yako yatakuwa ni machache, kwa hiyo, hatutaweza kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la ukusanyaji wa mapato, kama tunayumba hapa naomba paangaliwe upya. Eneo la ukusanyaji wa mapato na lenyewe lichunguzwe upya, inawezekana kuna uzembe mahali ambao unasababisha haya yote kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kuongelea hizi riba za benki. Kwa kweli, zimekuwa juu sana kiasi cha kumfanya mwananchi wa kima cha kati ama kima cha chini kuogopa kwenda kukopa benki na hivyo kuwa ngumu kwake kujikwamua kutoka kwenye umaskini na sisi lengo letu ni maisha bora kwa kila Mtanzania, kwa kila mwananchi. Kwa hiyo, basi waangalie upya ni namna gani mtumishi wa kati ama mwananchi wa kima cha chini anavyoweza kuwezeshwa, ili aweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee hili la Benki ya Wanawake. Katika bajeti iliyopita, tuliongelea angalau basi ziwafikie wanawake vijijini; tukajaribu kueleza na namna ambazo zinaweza kuwafikia, lakini bado inaonekana kama hata kiwango chake bado ni kidogo kinachotolewa na Serikali. Kwa hiyo, tunaomba pia Serikali iangalie namna gani kwa sababu, vijijini hakuna mabenki. Mpaka utoke kule Kijijini kwenda benki kutafuta ni ngumu, basi tunaomba waangalie namna ambavyo Serikali itaongeza hela katika hii Benki ya Wanawake ili wanawake wa vijijini hasa wanaotoka Mkoa wa Katavi na Rukwa, Kigoma, Songea, Mtwara, waweze

kupata huduma hizi. Sio tu wanawake wa mjini, fursa nyingi zinakuwa kwa watu wa mjini. Kwa hiyo, hili naomba katika mipango hii mzingatie sana hilo, lakini la msingi kabisa la kuzingatia naomba uwekezaji mkubwa ufanywe na Serikali katika sekta ya elimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Kikwembe. Sasa namwita Mheshimiwa Mwijage, nadhani ndiye atakayekuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/ 2015, labda nina mambo matatu ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni lazima niliseme; wakati ilipoanzishwa *operation* Kimbunga, nilipokutana na tajiri mwenye nchi, baadaye akatangaza *operation,* rafiki yangu mmoja Mtendaji wa Serikali, aliniambia nyie Wanasiasa msituingilie tufanye Kimbunga. Wakafanya Kimbunga huko, sikuwaingilia; juzi uzalendo umenishinda, nimekwenda kwa Waziri wa Ulinzi leo asubuhi nikaenda kwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Rutoro, *Operation* Kimbunga haikufanyika, ng'ombe wote walifichwa pale na watu wa kutoka nchi fulani wakajificha pale, leo wameamua kuvamia migomba ya wananchi, basi wananchi wanalia. Sasa rafiki yangu nimeamua kuingilia na bila kukuuliza wewe nimeshamwambia Waziri na Serikali nimeiambia. Kwa hiyo, Kimbunga ilipofika pale Rutoro iliruka juu, haikufanya kazi. Sasa mkuu wa *operation* kaeleze kwa wakubwa zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu huu mpango. Niishukuru Kamati ya Mheshimiwa Chenge, mmefanya tafakuri nzuri; maelezo yenu kama kweli tutatenda haki tuyazingatie. Kamati ile ya Mipango unaweza kuwa na jambo nao, lakini kazi iliyofanyika ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nizungumze kuhusu hawa Watendaji wa Serikali. Watendaji wa Serikali watatushangaa, na nadhani ndio maana leo wameamua wasije, sio Mawaziri tu hata Watendaji kule wanakokaa hawapo, wameamua wasije. Watendaji wa Serikali mnafanya kazi, lakini kwa sababu na sisi kazi mnazofanya tunazijua, mnapaswa kufanya kazi zaidi ya mnavyofanya sasa; mna mgomo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine la nishati, niende kwenye Mpango, Mpango unasema utapeleka watu kujifunza gesi na nini. Hoja na suala sio kujifunza gesi, tulivyokubaliana tangu tufike Bungeni 2010, tulisema Watanzania waajiriwe katika sekta ya gesi na mafuta, waanze ku-*understudy* makampuni yanayoendesha shughuli, ili hawa Wazungu au wageni wanapokuwa wanamaliza, wana-*graduate,* watu wetu waweze. Waheshimiwa Wabunge, ngoja niwachongee hawa watu wa Serikali; najua ule mpango wa ku-*train* Watanzania wamekataa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia tajiri mwenye nchi, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, anasema Watanzania waajiriwe, Mheshimiwa Muhongo anasema waajiriwe, Waziri wa Utumishi anasema waajiriwe; ndani ya Wizara ya Utumishi kuna watu wanakataa. Kama ningeulizwa nje, ningesema wanalipwa, na nikiambiwa wanalipwa na nani, naweza nikamsema. Wanalipwa na mbaya wetu kwa sababu si kila mtu anatutakia mema. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali imekataa kuchukua vijana wa Kitanzania kwenda kuwa-*understudy* Wachina wanaochomea bomba? Mimi ni *Pipeline Operator,* kazi yangu niliyoanza kufanya ni *Pipeline Operator* niki-*prime* matenki na kusukuma mafuta. Nikatoka hapo nikaenda mpaka nikafikia hapa nilipo, nimesoma shule nyingi kweli, lakini *core job* niliyojifunzia ni *Pipeline Operator;* kwa nini mnakataa kuwaruhusu watoto waanze kujifunza?

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia Mchina ameanza kufanya kazi. Waziri wa Utumishi nina habari zako, umesema waajiriwe, kuna watu wamekataa kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi zile pesa nilipokuwa naiongoza ile Kamati, tulipoibiwa Dola milioni 100, hamjui kesi tulishindwa vipi. Katika Mkataba walikuwa wanasema ni wajibu wenu kufanya *auditing.* Kumbe sisi tulipigwa changa la macho kwa sababu, hatukufanya *auditing,* tukaamua waajiriwe watu kwenda kufanya *auditing;* Utumishi wamekataa, Waziri umekubali nasikia, Mheshimiwa Muhongo amekubali, tajiri mwenye nchi amekataa, Utumishi kuna watu wamekataa. *You don't need restructuring,* huhitaji kufanya *restructuring* ya *TPDC* kusudi kuajiri *Auditor;* umwajiri *Auditor,* utakapotaka wa kumpeleka wakati huo utampeleka popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina wanalaza bomba kilometa tano kwa siku. *By the time* unapeleka watoto wetu Wasukuma, Wanyamwezi wa Tanzania kwenda kujifunza Mchina atakuwa amenyanyua virago ameondoka. Watu wanasema mtaani kuna kampuni mnaiandaa kuipa hilo bomba. Ndugu zangu niwaambie, mkiipa kazi wataandamana na sitakubali kuwa Mwenyekiti wa Kamati wakati huo, eeh. Watanzania hawataridhika, *you are not doing fair to the country.* Nimependa niliseme hilo ili roho yangu iridhike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusudi mazima kuna genge la Watanzania limekataa kutekeleza maelekezo ya Bunge, kuwaajiri wale vijana tuliosema wakawa-*understudy* Wachina, *nothing has been done,* nimeamua kulisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye viwanja vya ndege, Mpango unazungumzia Viwanja vya Ndege. Nawapongeza, lakini Mpango ubadilike, kujenga mazingira wezeshi ya wawekezaji kuja kutengeneza *Airline,* aaa, tumeshindwa, tumesubiri muda mrefu; *The Government should take the lead law* kuhakikisha tunayo *National Airline,* hatuwezi kuendelea kuwa nchi ambayo haina *National*

*Airline.* Kuna nchi zimefanya hivyo na sisi twende kule; mazingira wezeshi hamwezi kuyatengeneza, tunakaa kwenye vikao mno, vikao vinakuwa vingi mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nimeunga mkono kazi ya Kamati ya Bwana Chenge, imefanya kazi nzuri. Niongezee kidogo kwenye suala la chakula. Ninachowaomba, pamoja na kujenga *Silos,* mtueleze kwamba, mtajenga maghala ya chakula angalau ya kuhifadhi chakukula cha miaka kama minne, kujenga *Silos* si hoja ni *silo* za kutunza chakula cha miaka mingapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *Silo* moja Shinyanga kwa ajili ya Kanda ya Ziwa, hamtutendei haki. *Economics* hazikubali kutoa chakula Peramiho, hata kama wangekuwa wanatupenda namna gani, kutoa chakula Peramiho kukipeleka Kagera; tunataka jitihada za Serikali zifanyike kusudi na sisi Kanda ya Ziwa tuzalishe *big time.* Tunayo mabonde ya maji mengi, tunayo maeneo mazuri, muwawezeshe watu kulekule, pamoja na kuzalisha chakula, lakini mnatusaidia ku-*retain* nguvukazi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza mambo mengi kwenye elimu. Mimi nina moja tu kwenye elimu, mnifanyie hilo nitaridhika. Nenda katafute pesa popote, kopa mahali popote, walipe Walimu madai yao; mmeyahakiki, hamkuyahakiki, umekuwa wimbo wa kila siku, *what is 57 billion?* Walipe waende wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watu wanahisi kwamba, watoto wanashindwa kwa sababu, Walimu hawajalipwa madeni, sasa muwalipe muwaachie ngoma wao. Nyie malizeni kazi tuwahukumu wao wenyewe, mtufanyie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika rasilimali watu mmeainisha maeneo ya kufundisha watu zaidi; mfundishe watu zaidi kwenye tiba, hiyo hamkuisema. Watu wengi wakifundishwa mambo ya tiba itatusaidia nini? Tunajenga zahanati kila Kijiji, sasa atafanya kazi nani mle? Sisi

tunaendelea kujenga kule, mtengeneze Wataalam wengi wa ku-*man* zile zahanati na hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninapomalizia, nimweke sawa rafiki yangu mmoja aliyesema mpango huu sio shirikishi. Mpango huu ni shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetoka Jimboni siku 30, nimetembea Kijiji kwa Kijiji, vijiji 62, nikizungumza na wananchi kuhusu Mpango na vipaumbele. Ni wajibu wa kila Diwani, bahati mbaya kwa wale Wabunge ambao sio Madiwani, lakini Mbunge yeyote ambaye ni Diwani, una wajibu wa kwenda kukaa na watu wako kuwauliza je ikija Serikali inauliza hapa, utachagua nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu nimefanya hivyo siku 30, Vijiji 62 matawi ya Chama cha Mapinduzi 75. Nilikuwa naanzia kwenye Chama najenga hoja, naingia ndani ya umma nasukuma mambo. Kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge, mpango huu ni shirikishi na ni jukumu letu sisi kama Madiwani kuwaongoza wananchi. Kwa sababu, kuna mtu mwingine unaweza kumuuliza unachagua nini, akamwambia mimi nachagua gari; unalo gari la kumpa na gari lenyewe anachagua *Vogue?* Kwa hiyo, ndugu zangu tukubaliane ni jukumu letu sisi kuwaongoza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ndugu zangu Watendaji, nimemwona rafiki yangu kwenye Wizara fulani, nimseme; watu wa Bandari mnatuangusha, *Port Community* haijafanya kazi vizuri. Nilimwona Waziri mmoja rafiki yangu analalamika nikasikitika kweli, unajua katika vitu sitaki kusikia nchi hii ni kuona Waziri analalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ushirikiano mzuri wa *Port Community* kati ya watu wa *TRA,* watu wa Madawa, watu wa *Container* sijui nini na nini, hamfanyi kazi pamoja, ongezeni kasi. Niwambie, Afrika Mashariki haitakufa kwa sababu, mimi kwangu Gosba napakana na Kenya napakana

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



na Uganda, sasa itakufa waondoke waende wapi? Kwa hiyo, tutaendelea kuwa nao, lakini ili tuwe nao ni ufanisi na siasa ni uchumi. Watu wa Kenya wako kwenye uchumi.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Kaimu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwandosya.

**KAIMU WAZIRI MKUU - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nitumie nafasi ya kuwa karibu na hiki Kiti muhimu sana ili niweze kutoa mchango katika haya yanayoendelea. Mchango wangu, najielekeza kwenye mawazo na michango ya Waheshimiwa Wabunge, iliyoelekezwa kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa Mawaziri wakati wa majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa niaba ya Serikali, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tuwepo tusipokuwepo, tunathamini sana sana yale ambayo yanazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Nasema hivi kwa uhakika kabisa kwamba, macho na masikio ya Serikali wakati wa Mikutano ya Bunge yanakuwa Dodoma kwa njia mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumeulizwa mbona Makatibu Wakuu hawapo? Napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hivi mnavyozungumza kila Ofisi ya Serikali katika ngazi za Katibu Mkuu au Naibu Katibu Mkuu hata Wakurugenzi, kuna runinga na macho yao na masikio yao yameelekezwa Dodoma. Mnaweza msimwone, kwa mfano hapa Gavana wa Benki Kuu, nina uhakika Gavana wa Benki Kuu sasa hivi, Makamu wa Gavana, wote wanasikiliza yanayoendelea katika majadiliano muhimu kama haya, ndivyo Serikali inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuwaona nyuma

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


yetu kule Maafisa wawili au watatu, lakini wanachukua kila kitu. Kile kinachowahusu wao, kinachowahusu vile vile Mawaziri wengine, tutakipata leo hii hii na Mawaziri watajua ni nini kimezungumzwa na watatakiwa, kwa taratibu zetu za Serikali, kuandaa majibu ili kuweza kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali hufanya kazi kwa taarifa. Taarifa muhimu katika kipindi hiki ni zile zinazotoka Dodoma na yale ambayo wanazungumza Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, tunaheshimu sana michango, tunasikiliza, hata wale ambao hawapo, sisi tuliopo tunasikiliza kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haimaanishi kwamba, tusiwepo, lakini kwa kweli naamini, jana imezungumzwa, leo imezungumzwa vilevile na pale ambapo hakuna sababu ya muhimu ya kutokuwepo Waheshimiwa Mawaziri watakuwepo, lakini pale ambapo kuna sababu za msingi, naamini kabisa kwamba, wanakuwa na sababu ambazo zinawafanya wasiwepo, lakini sisi tuliokuwepo tunachukua kila kitu kwa niaba yao. Ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba, hilo ndilo linalofanyika. Serikali, inafanya kazi kwa...

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM – KAIMU WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, jioni tunaendelea na michango. Tutaanza na Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa *Captain* Komba, Mheshimiwa Yussuf Salim, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa Lwanji.

Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Nasitisha Bunge, mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana, Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilitangaza majina ya watu watakaochangia jioni hii, sasa nitaanza na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa nafasi jioni hii kuwa wa kwanza kuchangia Mpango wetu wa Maendeleo wa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitisha Mpango Mkuu ule wa Miaka Mitano, tulisema tutakuwa tunatumia 8.5 trilioni kila mwaka kwa ajili ya shughuli za miradi mikubwa ya maendeleo. Ningependa labda watu wa Serikali watuambie, tunakwenda mwaka wa tatu sasa, naamini mwaka jana hatukutumia 8.5; mwaka wa kwanza walisema ndiyo tunaanza na ukiangalia hata huu mwaka huioni 8.5 trilioni kwenye mipango ya maendeleo, sasa tunajiuliza tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kilimo; kwa miaka hamsini iliyopita, tumeendesha kilimo chetu kama wanasiasa. Kila kitu tulikuwa tunafanya siasa kwenye kilimo, nadhani umefika wakati sasa kama nchi, kilimo tukifanye kuwa ni biashara. *This is the moment* lazima kama Taifa, miaka hamsini ijayo sasa, tufanye kilimo ni biashara ili kichangie kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tufanye hivyo? Tuamue kwanza tuzalishe chakula cha kutosha hapa nchini, lakini tukishafanya ni kilimo cha biashara kila mtu atakwenda kulima kwa sababu anajua mwisho wa siku ukishakifanya

kibiashara maana yake hata bei utakazopata za mazao yako ni bei ambazo ziko kwenye soko la biashara. Baada ya hapo tuanze kulima mazao ambayo ni *demand driven* duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ili tuweze kufanya haya yote, lazima tuweke sasa *legal framework* yenye *clarity,* tuwe na *commodity stock marketing* in Tanzania. Tukishakuwa na *commodity stock market,* kila mtu anajua atakuwa analima kulingana na bei anazoweza kuzipata hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalofanya sisi siyo wa kwanza, wenzetu wamefanya, Vietnam wamefanya, Thailand wamefanya, South Afrika wamefanya na Kenya wamefanya. Wamegeuza kilimo ni biashara ndiyo maana leo mpunga wa Thailand na mpunga wa Vietnam unaliwa dunia nzima na sisi tukiamua tiumnaweza kwa sababu tumepewa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini umefika wakati tumeongea sana, Wazungu wanasema; *we have been talking miles, we are doing centimeters.* Tumekuwa tunaongelea ma-*mile* na ma-*mile* lakini kwenye kutenda tunakwenda sentimita kwa sentimita. Nadhani wakati umefika tuache maneno, maneno tumesema sana yanatosha, kwa miaka hamsini ijayo tugeuze kilimo ni biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sasa hivi tunaambiwa tumepata muarobaini wa matatizo yetu, ni mtu anaiwa *BRN (Big Result Now),* sasa hivi kila mtu wa Serikali anakwambia sasa tuna *BRN,* matatizo ya nchi hii yataondoka, mimi nasema hapana. Nataka tuambiwe *clearly, source* ya *revenue* ya hii *BRN* iko wapi? Iletwe hapa tuione *source of envelope* ambayo tunasema *BRN* na miradi yake yote fedha ni hizi hapa, zitapatikanaje na Wabunge waweze kuziona na kuzipitisha, *otherwise* itakuwa ni *talk show.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana kwenye *BRN* kwamba, baada ya *BRN* kumaliza tu, tuondoe vizingiti

barabarani kwenda Rwanda, kwenda Tunduma, vizingiti havijaondoka na havihitaji bajeti. Sasa tunasema *BRN* hii inakuja kufanya nini kama hatuwezi kuamua sasa, *BRN* haiwezi kutuelewa tunachotaka kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu, ni reli ya kati, jamani reli ya kati tumefanya siasa, inatosha. Tumeongea kuhusu reli ya kati, siasa imefanyaje, imetosha. Tukiamua leo tunaanza kujenga *standard gauge* tunaweza na tunawezaje; tufanye kwa miaka mitano, unasema naanzia Dar es Salaam mpaka Morogoro nitang'oa reli, wakati unafanya Dar es Salaam mpaka Morogoro hii reli ya zamani inafanya mpaka Morogoro; wakati huo unafanya *study* kutoka Morogoro mpaka Dodoma, unamaliza huku unakuja huku. Unatoka Dodoma unakwenda Tabora, toka Tabora unakwenda Kigoma, unatoka Tabora unakwenda Mwanza ndani ya miaka mitano tutakuwa na *standard gauge.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hatuwezi kuamua na kutenda, kila siku tunasema, hapa watakuja watatuambia kuna Wachina, kuna Wajapan, kuna Wamarekani, tunafanya *study*, tunafanya *study* kwa miaka mingapi? Wenzetu wanafanya, leo Wakenya wanajenga *standard gauge,* tunapiga kelele hapa Wakenya, Wakenya, wenzetu wanaamua wanakwenda mbele. Wakati umefika tupunguze kusema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msongamano wa Dar es Salaam. Msongamano wa Dar es Salaam tusihangaike kuvunja nyumba, wako watu wanaweza wakafanya, unaweza ukaamua kutokea hapo Serena *Hotel* ukaweka *highway,* ukapanda juu, ukasema barabara ya juu huku ni ya watu wenye haraka watalipia, barabara ya chini ni ya Watanzania ambao wanakwenda bure, *people will do it.* Unaweza ukatoka pale ukajenga juu ukaenda mpaka Ubungo, ukajenga juu ukaenda mpaka *Airport*, ukajenga juu ukaenda mpaka Mwenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wale wenye haraka watapanda juu watalipa, watakwenda; wale

wanaosema hapana, lazima Serikali itujengee barabara, watapita kwenye barabara yetu ya chini. Hujambomolea mtu, lakini bado utakuwa umemaliza tatizo la Dar es Salaam. Kwa nini hatufanyi, mimi sijui Mungu ndiye anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la madeni; ukisoma kwenye vitabu deni letu la Taifa limepanda kutoka dola bilioni 12 mpaka dola bilioni 16 maana yake kwa mwaka huu mmoja tu, kuna dola bilioni nne za deni la Taifa zimeongezeka. Nataka Serikali ituambie tumefanya miradi gani kwa dola bilioni nne kwa sababu dola bilioni nne *by any standard* hizo ni trilioni karibu sita, basi tungeziona kwenye miradi ya maendeleo, *otherwise* tunakopa kwenda kula, kitu ambacho sidhani kama ni sahihi. Kwa hiyo, naomba wakati tunaambiwa, u*nl*ess tunakopa tunakwenda kulipia mafuta ya umeme ambayo nayo ni hatari kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Waziri atakapokuwa anajieleza atuambie *four billion dollars* zilizoongezeka kwa mwaka huu za deni la Taifa zimefanya miradi gani, *otherwise* Wabunge tutakuwa tunakaa hapa, tunapiga maneno, lakini hatuoni kinachokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, madeni ya ndani. Kama tunataka kuendelea lazima tulipe madeni ya ndani. Madeni ya ndani ndiyo wafanyabiashara hawa walioajiri watu wetu ambao hawajaajiriwa na tukiwalipa hawa inashamihisha kwenye uchumi wetu. Kwa hiyo, naomba sana, nenda kwenye Halmashauri watu wanadai, nenda kwenye Mawizara watu wanadai, nenda Jeshini watu wanadai, *everywhere* watu wanadai. Sasa tunafanyaje kulipa madeni ya ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, lazima sasa tuondoke kwenye *cash budget,* tutoke kwenye *cash budget* twende sasa kwenye *accrual basis* na twende kwenye *International Standard* katika kuripoti kwenye Mawizara yetu ili hao Maafisa Masuuli wasiwe wanafanya vitu, halafu kwenye bajeti hawajaziweka zile fedha za madeni, ile fedha ya bajeti ya

mwaka unaofuata wanalipia madeni ya mwaka uliopita ambao hawayakuya-*provide*. Nadhani umefika wakati tuanze kutenda badala ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Hamad Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Salim na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ajiandae.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi jioni hii ya kutoa mawazo yangu katika mada iliyopo mbele yetu katika Mpango huu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwanza sote tuliomo humu ndani kila mmoja ajiulize kwa nini tupo hapa, kwa nini tumechaguliwa na wananchi kuja kuwawakilisha hapa, kwa nini tumeteuliwa na vyama kuja hapa na kwa nini tumeteuliwa kuwa Mawaziri au Manaibu Mawaziri. Tukishajiuliza hili neno kwa nini tupo hapa, basi tutapata majibu ya haya matatizo ambayo wenzangu wengi wamekuwa wakiyapigia kelele hapa kwamba utendaji au utawala bora unakuwa ni tatizo katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nadhani ubinafsi ndiyo umetawala zaidi na ndiyo unaochangia kuonekana kwamba nchi yetu haiendi mbele. Kila siku Watanzania tunaimba wimbo kwamba tuna rasilimali nyingi kuliko wenzetu wa Afrika; tuna vivutio vingi vya utalii, tuna bahari, tuna mito, tuna mabonde, tuna maziwa, lakini bado nchi hii ni maskini kupindukia, kwa nini? Ni kwa sababu ya ubinafsi na hatujakuwa *committed* katika ile nafasi ambayo mtu ameiomba au amepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi ni kwamba, tunakula kiapo hapa na badala ya kiapo unamwomba Mungu nisaidie. Sasa Mungu atusaidie nini kama ametupa

neema zote hizi alizotupa, akatupa na elimu, akatupa na uzima, lakini bado leo tunakuwa maskini na tunasema tu, tuna hivi, tuna hivi, lakini bado ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa imekuwa kama ni pambo la jeneza, nje utaiona ni nzuri, lakini ndani kuna uozo kama huu; kila Mbunge anayesimama hapa, anapiga kelele tuna rasilimali lakini ni maskini sana. Kwa hiyo, nadhani kila mmoja ajiulize na ni wakati sasa wa kubadilika, ni wakati sasa wa kuamua kuwa *committed,* kila mtu kwa nafasi yake aliyopewa kuona kwamba, nchi yetu inakwenda mbele na hizi hadithi za kwamba uchumi, uchumi, tuko maskini, ziishie kwa sababu nani atakuja kutufanyia na wafanyaji ni sisi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili naiomba Serikali basi ichague miradi michache katika utitiri huu wa miradi ambao umeelezwa hapa. Ichague miradi michache ambayo tunaweza kuitekeleza, tuitekeleze imalizike, haya mambo ya kuwa na miradi mingi halafu hatuwezi kuitekeleza, hili ni tatizo ambalo baadaye litatugharimu; mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutayataka mambo haya yatatushinda, halafu 2015 yatatugharimu lakini hatuishii 2015 kwamba labda utakosa Ubunge tu na nini, lakini umekula kiapo, umechukua ahadi kwamba utayatekeleza haya, kwa Mungu tutajibu nini na tumeshindwa kuyatekeleza na tumeandika wenyewe kwamba tutatekeleza haya. Kwa hiyo, lazima tujielewe, ni lazima sasa tujitambue, kwamba tumeji-*commit* na lazima tuwe *committed* katika yale ambayo tumeji-*commit* wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hatuwezi kuyafikia kwa sababu ni mambo mengi yanahitaji fedha nyingi na uwezo wetu wa kulipa kodi au wa kukusanya kodi ni mdogo. Sasa nataka watu wa Wizara ya Fedha wanisikilize vizuri hapa, nataka nitoe rai katika suala la kodi, vipi tunaweza tukakusanya kodi nyingi na tukaweza kufanikisha miradi mingi tuwezavyo. Tunajitahidi sasa hivi kukusanya kodi kwa kiwango

kizuri, lakini pia tukubali kwamba, ni fedha nyingi vile vile tunaipoteza katika kukusanya kodi, kivipi? Bado kuna mianya ambayo walipa kodi au walipisha kodi, fedha nyingine zinaingia katika njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, Tanzania leo mtu kama anaingiza gari la mwaka 2001, akienda Mheshimiwa Barwany gari hilo hilo la 2001, aina hiyo hiyo, *cc* hizo hizo ataambiwa lipa *tax* milioni tatu. Akienda mwingine gari hilo hilo la mwaka huo huo lipa milioni mbili na nusu, sasa kwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Wizara ya Fedha kwa sababu tunajua bidhaa zote ambazo zinaingia nchini na kwa sababu tunajua bidhaa zote ambazo tunatoa kupeleka kuuza nje, kwa nini hatuweki bei moja, ikawa mfanyabiashara wetu akiwa kule nje, anajua nanunua *khanga* hii kwa bei hii, nitaisafirisha kwa bei hii, nitalipa ushuru huu na nitauza kwa bei hii, nitapata faida hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza itawasaidia wafanyabiashara wetu kuweza kujua kwamba biashara hii ninayoifanya nitapata faida ama nitapata hasara. Hilo la kwanza, lakini tujifunze mazuri kwa wenzetu. Katika nchi za *Scandinavian, Sweden* wameweka utaratibu huu, kila kitu kinaeleweka, kwa hiyo, wako *very transparent* katika biashara na wao kwa sababu wameweka hilo katika biashara, kila kitu kinajulikana hamna ukifika pale unafanya *negotiation* na mtu wa *TRA,* hakuna! Unajua nimechukua kiasi hiki cha mzigo, *tax* yangu ninayopaswa kulipa ni hii, hakuna urasimu, hakuna kupoteza muda, unalipa, unachukua mzigo wako, unaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wamefanya hilo wamefanikiwa na wafanyabiashara wa *Sweden*, baada ya kuona Serikali yao kweli imekuwa *committed*, imekuwa *very transparent,* wameamua wanaisaidia Serikali yao 20% ya faida anayopata mtu. Kwa hiyo, kiwango kile kinatosheleza bajeti ya *Sweden* na *surplus* na ndiyo maana utakuta sasa yale makusanyo yao ya kodi na njia nyingine ndiyo wanapata

fedha kutusaidia sisi. Tanzania tunashindwa nini kuiga hili, hadi leo tunaacha mianya ya rushwa, mianya ambayo ina mifereji mingi ya kuingia fedha za kodi, tunashindwa nini kuliweka hili. Nadhani mambo mazuri tuige ili na sisi twende mbele. Hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la uvuvi; katika maelezo yote yaliyotajwa katika vitabu hivi, suala la uvuvi halijazungumzwa vya kutosha pamoja na kwamba tuna eneo kubwa la bahari kuanzia Mtwara mpaka Dar es Salam, Zanzibar, Pemba, Tanga, wapi haijazungumzwa, tuna Maziwa Tanganyika, *Lake* Victoria, tuna mito na mabwawa lakini suala la uvuvi halijazungumzwa, halijapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatujaweza kuzitumia bandari zetu kama Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar kwa ajili ya uchumi wetu, wenzetu Dubai bandari tu, Malaysia bandari tu, lakini wako mbele, sisi Mwenyezi Mungu ametupa rasilimali hizo tunazitumia vipi? Ubinafsi umetawala ndani ya nafsi zetu, kila anayepewa nafasi basi anaona yeye tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kila Mtanzania amelewa na gesi na mafuta ya Mtwara. Kwa hiyo, sote tumegeukia huko, tunaacha mambo yetu mengine yote haya kuona kwamba haba na haba hujaza kibaba, hayo tumeyaacha, tunakuja kuiangalia gesi tu, jamani tunaunga kimo kwa kinu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tungeziangalia bandari zetu tukazitumia bahari tulizonazo na mabwawa na mito tukaimarisha uvuvi, nchi kama Malaysia uvuvi unaingiza asilimia kubwa sana katika pato lao la Taifa, sisi hatuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kuishauri Wizara inayohusika na mambo ya Uvuvi suala linaloendelea hili la uchimbaji wa gesi na mafuta kuna mazingira yanaharibika, lakini pia kuna vyanzo ambavyo tunaweza tukatengeneza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf, nakushukuru sana.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Dokta Kigwangalla, wajiandae Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Kidawa na Mheshimiwa Zambi.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ili nami nitoe mchango wangu kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi kwa kutujalia afya njema siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze Waziri angalau kwa kuweka vipaumbele vichache kwenye Mpango huu wa *Big Result Now*. Tulizoea kuona taarifa ama mipango mikakati ya Serikali ikiwa na vipaumbele vingi sana. Nakumbuka mwaka wa kwanza nilipokuwa Mbunge, kwa mara ya kwanza kulikuwa na vipaumbele 13, mwaka huu angalau viko sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwamba hata sita nafikiri ni vingi sana. Kweli tunashindwa tuache kipi, tushike kipi, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba, ukiwa na vipaumbe vingi sana unashindwa ku-*focus* na katika mambo haya ya maendeleo *the power of focus is very important,* unahitaji ku-*concentrate efforts* zako, japokuwa ni chache, u-*concentrate,* uzi-*focus* kwenye eneo moja maalum ili uweze kuona matokeo katika muda fulani, lakini pia ili uweze kuwa na *excellence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la kuwa *excellence* lina tafsiri katika sura ya kuwa na utamaduni wa *excellence*. Kwa mfano, nafahamu pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hii *culture* ya *excellence* inapatikana sana kwenye uwezo wa ku-*generate graduates* ambao wana

*independent thinking,* ambao wako *opened minded*, wana uwezo mkubwa wa kufikiria na kuchambua mambo, ambao wanaweza kuwa tayari kwa *open debate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo hicho toka kinaanza mpaka leo hii huo ni utamaduni wa chuo kile, ni utamaduni wa *excellence* kwenye kuzalisha *graduates* ambao wana uwezo mkubwa wa kupambanua mambo, wana uwezo mkubwa wa kuhoji na ndiyo maana wale viongozi wa zamani walikuwa wako huru sana walikuwa na uwezo wa kufikiri, wa ku-*debate* bila kukorofishana, bila kukasirikiana, kumbe ni utamaduni ambao waliupata kwenye Chuo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napata swali kwamba, hivi taasisi kwa mfano kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ama kama Baraza la Mawaziri lina *excellence* kwenye nini hasa. Hili ni jambo ambalo pia tunatakiwa tulitazame, maana yake tunaweza tukawa tunaongelea maendeleo tu, lakini kumbe tunasahau *ingredients* ndogo ndogo ambazo zingeweza kutupelekea kupata maendeleo, mojawapo ni kama hiyo tu ya kuwa na *culture* ya *excellence,* kuwa na *mindset* ambayo inawafanya watu wanapenda kuendelea, wanapenda kuwa *progressive.* Hiyo tu ni mojawapo ambayo ingeweza kutusaidia kupiga hatua, kuliko kila siku tunaongea mikakati, lakini haitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza kwa makini sana ndugu yangu Mheshimiwa Peter Serukamba, anaelezea mikakati kwa uchungu kweli kwamba, tunasema zaidi kuliko kutenda, lakini ukweli utabaki pale pale kama hatutaki ku-*focus*, kama hatutaki ku-*concentrate efforts* zetu kwenye mambo machache, tuka-*develop excellence*, tukayafanya mpaka tukayakamilisha, hatuwezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa kila siku tunapanga mambo mengi, lakini mwisho wa siku hatuoni matokeo ya mipango yetu. Huo sasa mekuwa kama ni wimbo kwa Watanzania, kiasi kwamba hata kama tunajaribu kuweka mipango mizuri hapa, Watanzania wanakuwa wameshatuzoea kwamba aah! *The same business*, kama

kawaida wanavyofanya Bungeni pale, wanaongea mikakati mizuri, lakini hatuoni matokeo. Kwa hiyo, nilipenda nisemee kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo hii sisi tuna *excellence* kama Taifa kwenye mipango, kwenye kuandika *documents,* kwenye kuleta mikakati, kwenye kuja na *slogans* nzuri nzuri, lakini hatuna *excellence* hata kidogo kwenye kuchukua hatua na kwenye kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya wako shapu kwenye ku-*grasp opportunities* kuzitafsiri kwenda kwenye matokeo mazuri kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa watu wao, sisi huko hatuko kabisa. Ndiyo maana leo hii tuna kilio, wenzetu wanakimbilia wanaona *opportunity* ya kuchukua soko la South Sudan na Ethiopia, sisi bado tunahangaika na mambo yale yale ya kila siku, wakati sisi tungeweza kuwa *gate* ya kuingilia Afrika Mashariki na Afrika ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tujifunze ku-*focus,* tu-*develop culture* ya *excellence* ili tuweze kujulikana kwamba Watanzania, kwa mfano, Bunge hili ni makini kwenye kitu gani, ni makini kwenye nini? Kama tungekuwa makini kwenye usimamizi, basi tungeonekana tunawawajibisha watu hapa. Kwa mfano, kama *excellence* yetu ni *oversight*, mtu akikosea anakuwa *responsible*, lakini hilo pia hatuliwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo hii, mambo haya tunayoyaongelea hapa, kwa mfano, hoja ya kukuza ajira kwa vijana, mambo ya kilimo ambayo yapo kwenye kipaumbele namba moja, tulipitisha hoja, tukasema kila mkoa utaandaa ardhi, tukasema Serikali itatenga fedha, itaanzisha Mfuko Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana, pesa zitawekwa mle, graduates wetu watakwenda kulima, lakini hakuna pesa iliyopelekwa mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bunge lingetakiwa lije liwa-task Serikali hapa kwamba, kwa nini hawajatekeleza Azimio, lakini tupo kimya, kwa hiyo hatuna *excellence* kwenye

kuwahoji watu *responsible* na kuwahoji watu *accountable*, tunanyamaza, mambo yanakwenda kama kawaida na hilo ndiyo tatizo kubwa ambalo tunalo kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja yangu ya pili na ya mwisho kwamba, tunapozungumzia Tanzania ya kesho, wengi tuna-*focus* kwenye mambo ambayo yanapatikana leo, kwa mfano, tunazungumzia sana kuwekeza kwenye nishati na madini, tunazungumzia zaidi mambo ya gesi sasa hivi, utafiti kwenye mafuta na tayari Wizara ya Nishati na Madini inagawa vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba iingie kwenye rekodi leo hii kwamba, siungi mkono jitihada zote zinazofanywa na Serikali za kwenda kugawa vitalu vyetu wakati hatuna Sera ya Gesi inayoeleweka, hatuna Sera ya *Local Content Initiatives*, hatuna Sera ya Uwekezaji inayoeleweka, hatuna Sera ya Kutajirisha Makampuni yetu kama *TPDC* na *STAMICO* kwenye madini, tunakwenda tunagawa tu vitalu, watu wanachukua, sisi hatujajipanga hata kama tuna sera gani na mle ndani tunafaidika vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tungekuwa kama tuna *excellence* kwenye kupanga mipango yetu, tungeweza kusema kwamba kila kampuni itakayokuja *free carried interest* kwenye kampuni hiyo inayowekeza pale lazima *TPDC* ichukue 40 *percent* na ingekuwa kwenye sera na ingekuwa kwenye sheria na kila Mtanzania angekuwa anajua hivyo lakini leo haiko hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba iingie kwenye rekodi kwamba, siungi mkono jitihada hizo na naomba kama kweli Serikali hii inasikia isikie kilio changu na kilio cha Watanzania walio wengi zaidi, tusimamishe utaratibu wa kugawa vitalu vya gesi mpaka pale tutakapokuwa tayari kuliwezesha Shirika letu wenyewe la Kitanzania kama walivyofanya Norway kwenye ile kampuni yao ya *Start Oil*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Start Oil* leo hii inakuja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


kuwekeza Tanzania. Lakini miaka 20 au 30 iliyopita *Start Oil* ilikuwa maskini lakini wakawekeza wao wenyewe mtaji wao, wakaweka mikakati mizuri, wakajijengea uwezo, leo hii *Start Oil* ni matajiri na nchi yao imetajirika kutokana na gesi. Lakini sisi tunakwenda kuwekeza hatujui *TPDC* ama kampuni yoyote ile ya Kitanzania, itakuwa inapata hisa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hivyo *Local Content Policy* hatuna, kwa mfano, wale watu Mtwara watafaidika vipi na uwepo wa uwekezaji huu mkubwa wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa tuna Sera tungeijadili Sera kama Watanzania, tukakubaliana kwamba, kwenye kila uwekezaji unaofanyika, *may be* asilimia 60 ya kila kitakachouzwa kama *raw materials and supplies* kwenye hii migodi ya gesi, kitoke maeneo ya pembezoni ya migodi hiyo, labda Mtwara na Lindi. Tungekuwa tuna sera ya namna hiyo ambayo inawa-*task* wale, tayari Serikali yetu ingekwenda kuwekeza kwa wananchi ili wazalishe bidhaa ambazo zinakidhi viwango vya ku-*supply* kwenye haya makampuni makubwa ya Kimataifa, lakini sisi hatujajipanga na hatuna sera yoyote, lakini tunaendelea kugawa vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema na iingie kwenye kumbukumbu kwamba, Hamis Kigwangalla, mtoto wa Nzega anapinga uwekezaji wa kuendelea kugawa vitalu kwenye gesi na ieleweke hivyo na wajukuu zangu watakuja kulikuta hilo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mambo mengine yanasikitisha, kwa mfano, leo tunapata kauli ya Serikali kwamba, Watanzania hawawezi kuwekeza kwenye gesi, wanaweza biashara ndogo ndogo za kuuza *juice* na maji. Hizi ni kauli za aibu, akizitoa *statesman,* mtu ambaye amepewa majukumu ya kuwa *Minister* inakuwa ni aibu kubwa zaidi, kwamba sisi hatuwezi kweli kuwekeza kwenye gesi, kwa nini tunashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Wazungu

wanachokifanya ni nini? Wanakuja hapa wanafanya utafiti, wakishapata wanakwenda kutafuta mitaji kwenye masoko ya hisa huko duniani. Wakipata ile mitaji wanakuja kuwekeza, wanazalisha, wanatajirika, kwani Watanzania wetu hawana elimu ya kuweza kufanya hivyo, naaamini wanaweza, lakini katika hali ya kusikitisha hatuwaungi mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba haya mambo tuyaweke sawa, tutengeneze sera vizuri, tuandae wasomi wetu watakaokuja kutusaidia ku-*exploit* hizi *resources* kabla hatujaendelea kuzigawa, maana yake tutakuja tutengeneze sasa hiyo Sera ya Gesi wakati gesi yenyewe ilishakwisha. Kwa hiyo, sheria inakuwa iko lakini haina maslahi yoyote wala haina faida yoyote kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na nashukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Namwita Mheshimiwa Maige, wajiandae Mheshimiwa Kidawa na Mheshimiwa Zambi.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango huu, Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2014/2015. Kwanza niseme tu kwamba, sina uhakika sana kama uandaaji wa mpango huu unajaribu kufanya *slice* ya mwaka mmoja ya ilani yetu ya CCM ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi kama *focus* ni hiyo kwa sababu ukiangalia sasa miaka mitatu imekwisha, imebaki miaka miwili kufikia hatua ya mwisho ya kufanyiwa tathmini ya kazi tulizofanya. Nitoe mfano tu wa maeneo ambayo naona kama vile utekelezaji wake na taarifa iliyotolewa, hauendi kwenye *focus* ambayo tunaitarajia kwenye ilani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye suala la maji, ukiangalia taarifa kwenye ukurasa ule wa 25, kifungu cha (E), kinaeleza upanuzi wa Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria

hadi Miji ya Igunga, Nzega na kadhalika. Niseme kwanza sina uhakika kwamba aliyeandika kifungu hicho sidhani kama anatoka Mkoa wa Shinyanga! Kwa sababu ukiangalia *genesis* ya wazo lenyewe lilianza mwaka 2008, Mheshimiwa Rais alipokuja kuzindua mradi ule, wananchi wa Kahama wakamwomba na Mheshimiwa Profesa Mwandosya bahati nzuri yuko hapa, wakati ule akiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya mradi ule ulikusudiwa ufike Isaka, kwa maana ya kupata maji Kagongwa na Isaka. Baada ya hapo mradi umeendelea kupanuliwa bila kutekeleza chochote. Sasa hivi tunazungumzia kupeleka maji Nzega, Igunga hadi Tabora na hatuna hata hatua moja iliyofanyika. Wako waliozungumzia kwamba tunazungumza *miles* na tunatekeleza *inches* na hili ndiyo linalojitokeza kwenye suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itafika mwaka 2015, tunazungumzia kwamba mradi tupeleke hadi Shelui, kwa sababu tunachokifanya ni kuendelea kuongeza maeneo bila kutekeleza angalau kidogo. Kwa hiyo, naomba sana katika utekelezaji tuwe *focused* angalau mwaka huu au mwaka uliopita tungekuwa tumefikisha maji Isaka, ili tunapokuja kuzungumzia mwaka huu kwamba, sasa leo hii maji yamefika Isaka mwakani tunayapeleka Tinde, ingeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kuiomba sana Serikali katika utekelezaji wa mpango, ikumbukwe sana kwamba tuna suala la Ilani na muda unakwenda na tathmini itakuja kufanyika kwa kuangalia utekelezaji ambao tutakuwa tumefanya kwenye yale tuliyoyaahidi. Mfano huo mmoja kwenye maji niutumie tu ku-*emphasize* kwamba, tatizo la maji Isaka na Kagongwa ni kubwa. Tathmini na uamuzi utakaokuja kufanyika, wananchi wataangalia ni kwa kiasi gani tumetatua eneo hilo na si kwa kiasi gani tumetaja maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo nataka kulizungumzia ni suala la madini, kwenye Ilani tumekusudia kupunguza matatizo ya wananchi na kunufaisha wananchi

[MHE. E. M. MAIGE]

wanaozunguka maeneo ya migodi. Mwaka 2010 tulitengeneza Sheria ya Madini ambayo ililenga kupunguza migogoro baini ya wananchi wanaoishi jirani na migodi pamoja na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana vifungu au utekelezaji wa eneo hili nalo hauridhishi. Nimeangalia taarifa kwa kweli nikashangaa, nikajiuliza hivi mwaka mzima kilichofanyika, ukiangalia ule ukurasa wa 39 kwenye suala madini, taarifa ya utekelezaji hasa kwenye suala hilo maeneo yanayozunguka mgodi, wanasema kazi iliyofanyika ni kukamilisha uchambuzi na udhihirishaji wa mipango wa ufungaji wa migodi ya Tulawaka, Bulyankulu, North Mara, Buzwagi na kadhalika. Nikasema hivi ahadi tuliyotoa ilikuwa ni kufanya tathmini ya ufungaji migodi au kunufaisha wananchi wanaozunguka migodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Sheria ya Madini ya mwaka 2010, kifungu cha 52(f) kinazungumzia migodi kuajiri na ku-*train* Watanzania. Kwenye eneo hili tulitegemea mpaka sasa hivi angalau kungekuwa na hatua kubwa imefanyika angalau Chuo kimoja cha *VETA* kimejengwa Kahama, Geita au eneo fulani ili kuwajengea uwezo wananchi wa maeneo hayo waweze kuajiriwa migodini, hili halijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika kwa mwaka mzima kwa mujibu wa taarifa hii niliyonukuu, ni kwenda kuangalia na kukaa na wale jamaa wakatufanyia *presentation* wakiangalia namna gani wanajiandaa kufunga migodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *approach* hii sidhani kama wananchi wale watatuelewa na sidhani kama wataendelea kutupa ridhaa ya kuendelea kuwatumikia. Nikutaadharishe sana Mheshimiwa Waziri kwamba, kwenye eneo hili jambo hilo ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la wachimbaji wadogo wadogo. Kifungu cha 16 cha Sheria ya Madini, kinampa nafasi Waziri kufanya uamuzi ili eneo fulani

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



liwe *designated* kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Kasi ya utekelezaji wa eneo hili ni ndogo sana na matatizo bado ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea kwenye taarifa tungeambiwa kitu gani kimefanyika na kwenye Mpango tungeambiwa sasa tumetekeleza angalau asilimia 30 ya lengo hili. Tuna wachimbaji wadogo wadogo zaidi ya milioni nne kwenye nchi, angalau sasa wachimbaji wadogo milioni 2.5 wamepata maeneo, angalau ingeeleweka. Kwa hivyo, *focus* iwe ni kutekeleza ahadi zetu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mwisho kwa mujibu wa vipaumbele vyangu; suala la migogoro ya wafugaji na jamii zingine za watumiaji wa ardhi. Naamini Serikali yetu ipo kwa ajili ya kutatua matizo ya wananchi, tatizo ya migogoro ya wafugaji na wakulima, migogoro ya wafugaji pamoja na wahifadhi kwa upande mwingine imekuwa ya muda mrefu. Tatizo kubwa lililoko ni ukosefu wa ardhi, lakini mbaya zaidi kwa sasa hivi ni hujuma ambazo zinafanyika kwa makusudi kabisa kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2011 tulianza mpango kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ya kuyaangalia upya maeneo ya hifadhi na tuliunda Tume kwa ajili ya kupunguza migogoro baina ya wananchi na wahifadhi. Tukaanza kukagua maeneo ili tuangalie maeneo ambayo ama yamebaki hifadhi kwenye makaratasi ili maamuzi yafanyike ili ya ku-*degazette* ili yaweze kutumika kwa shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka katika kazi hiyo yako maeneo ambayo naamini yalikwisha kuwasilishwa Serikalini na ukweli upo wazi kwamba, kwa mfano, misitu kama ya Geita *Forest Reserve*, Nyantakala *Forest Reserve*, maeneo ya *Game Reserve* kama Uwanda, maeneo mengi ambayo ukisoma kwenye karatasi yanaonekana ni hifadhi, hivi sasa ni makazi ya watu. Kinachoonekana hapa sasa hivi ni biashara na hujuma inayofanyika kwa makusudi kabisa kwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



wafugaji, kwa sababu kwa upande mmoja Serikali au Wizara haichukui hatua ya ku-*legalize* makazi ambayo *already* wananchi wako pale kwa zaidi ya miaka kumi, badala yake inaendelea kung'ang'ania kwamba yaendelee kubaki hifadhi wakati kimsingi yalishabadilika kuwa makazi, lakini mbaya zaidi sasa kinachofanyika ni wizi wa ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Sheria ya Wanyamapori, kifungu cha 18 kinaelezea au kuzuia vitu ambavyo haviruhusiwi kufanyika kwenye *Game Reserve*, mojawapo kifungu cha 18(2) ni kuzuia kuchunga mifugo hifadhini na kifungu kidogo cha (4) kwenye hicho kifungu kinasema: "Mtu akikutwa na mifugo hifadhini anatozwa faini kati ya sh. 300,000 hadi milioni tano, *has a maximum* bila kujali idadi ya mifugo aliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, ukiangalia taarifa ambazo zipo kwa sasa hivi, mifugo inatozwa kwa mfugo mmoja mmoja na kuna taarifa zinaonesha mtu anatozwa mpaka milioni 30 na kitu ambacho ni kinyume kabisa cha sheria. Matatizo haya yameanza kutokea toka miaka miwili mitatu iliyopita na kwa bahati mbaya sana ukiangalia mwaka jana tulipozungumza kuhusu suala hili, hakuna hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi sasa hivi imeongezwa sheria nyingine au adhabu nyingine ambayo haiko kwenye sheria ya kupiga risasi mifugo. Ni kinyume kabisa cha haki za mifugo, ni kinyume cha haki kwa kweli za kistaarabu cha jamii yoyote ambayo imeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana katika mipango yetu, tuwe na mpango maalum kwenye Wizara ya Mifugo, Wizara ya Maliasili pamoja na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la wafugaji, ambalo kwa sasa hivi ni tatizo kubwa na naamini kwa taarifa iliyowasilishwa jana itabidi yafanyike maamuzi magumu ya kuweza kukabiliana na hali iliyoko hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda kuwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



umekwenda sana, niombe tu kwamba pia katika utekelezaji wa Mpango wa MMAM wa kujenga zahanati na vituo vya afya kwenye maeneo mbalimbali, utekelezaji wake nao sidhani kama unaendana na Ilani, kwa sababu mpaka sasa hivi miaka minne inakaribia kwisha, bajeti zinazoletwa kwenye Wilaya kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hazifiki zahanati tano kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati malengo unakuta kwenye maeneo mengine ni zahanati karibia 70 au 80 kwa hesabu ya zahanati tano kwa mwaka, maana yake itafika mwaka 2015 kuna zahanati 15 au 25 na hatutakuwa tumefikia lengo. Wananchi bahati nzuri sasa hivi ni wasomi, wanatunza kumbukumbu, wanaturekodi kwenye mikutano yetu na utakapofika wakati tutasema jamani tulikuwa tunasema ya kwenye Ilani. Kwa hiyo, tunaomba tuelewe kwamba, *is a total failure of all of us* na siyo ya mtu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, Serikali ndiyo inayotekeleza yale tuliyoyaahidi, na Serikali ndiyo inayokusanya kodi itekeleze kama tulivyokubaliana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Kidawa, ajiandae Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa Kapteni Komba.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja iliyokuwa mezani sasa hivi. Nchi yoyote makini ni lazima iwe na mipango makini kwa sababu mipango ndiyo inayoonesha tunataka kuiondoa nchi wapi na tunataka kuipeleka wapi. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwa kuleta Mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mipango ya nchi iko

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



ya muda mrefu, miaka 20 na kwenda mbele; muda wa kati ya miaka mitano, na muda wa mwaka mmoja ambayo inatafsiri au inafanyia kazi yale malengo yaliyowekwa ya miaka mitano. Baada ya miaka mitano tunajipima kuona je, tumefikia malengo au hatukufikia malengo na kama hatukufikia kuna changamoto zipi zilizotukwaza ili kutoweza kufikia hayo malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina utaalam mzuri wa kuandaa mipango mizuri, lakini kuna changamoto nyingi sana zinazozuia utekelezaji wa mipango hiyo. Mipango imepangwa mizuri, lakini utekelezaji wake unakuwa mgumu na hasa hasa linalosababisha hivyo ni uhaba wa rasilimali fedha. Mipango inapangwa lakini hakuna mpango mzuri wa kuona ni vyanzo gani vya mapato vya uhakika ambavyo vinaweza kusaidia kutekeleza mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mipango ya kifedha ambayo iko juu juu tu. Labda tunategemea fedha zaidi kutoka kwa wafadhili, kutoka sekta binafsi na mchango ya mapato ya ndani unakuwa ni mdogo sana. Kwa mfano, katika Mpango wa Mwaka, imeanishwa pale, trilioni 8.6 zitahitajika kutumika kwa mwaka kutekeleza mpango huo uliowekwa; lakini kwa bahati mbaya sana ni trilioni 2.9 ndiyo mapato ya ndani. Mapato yenyewe ambayo hayapatikani kwa uhakika vilevile, lakini ni trilioni sita zimepangwa zitokane na sekta binafsi na Wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza sekta binafsi ni hii hii ya Tanzania au sekta binafsi ipi? Kwa sababu uelewa wetu, sekta binafsi ya Tanzania bado haijawa pevu, haijawa imara kusaidia kutoa fedha trilioni sita. Je, Serikali ilikaa na sekta binafsi wakaongea, wakakubaliana kama uwezo huu upo? Au Serikali imekaa ikawapangia watu wengine bila ya wao wenyewe kushiriki katika huu mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wafadhili sasa hivi, yaonekana nao wanaendelea kutuchoka. Kwa sababu ukichukua trilioni sita kwa mwaka, ukigawa kwa *quarter*, inategemewa zipatikane angalau trilioni 1.5, kwa robo

mwaka. Katika robo mwaka hii, mwaka huu tulionao takwimu zinasema kilichopatikana ni bilioni 50.7 tu. Kati ya zile zote zilizopangwa za misaada na mikopo za bilioni 291, ambapo kilichopatikana ni 94.1 kwa ujumla wake sawa na asilimia 32. Ni kitu ambacho hakina uhakika. Kwa hiyo, mipango itaendelea kuwa mizuri, wenzetu wa nchi nyingine wataichukua waifanyie kazi, lakini sisi katu haitatekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tujaribu kuleta miradi michache ya kipaumbele na vilevile iletwe pamoja na vyanzo vyake vya mapato. Kwa mfano, kama tunaamua kipaumbele namba moja baada ya kufanyiwa tathmini na utafiti, ambacho kitakuza uchumi haraka haraka, ni reli ya kati. Kwa hiyo, iangaliwe reli ya kati, itagharamiwa na chanzo gani cha mapato. Kwa hiyo, Serikali ije na vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; reli ya Kati itagharamiwa na chanzo *X*, mfano uvuvi wa bahari kuu au mapato ya bahari kuu. Kwa hiyo, chanzo kile kisitumike kwa mambo mengine yoyote, kitumike kwa kugharamia mradi ule tu, wanaita *merging principle.* Chanzo hiki cha mapato kinaambatanishwa na mradi huu fulani na hii inakuwa *ring-fanced*, kuliko sasa kila kitu kinatua kwenye *pool*, hatimaye fedha zinatumika katika matumizi ya kawaida zaidi, kuliko matumizi ya maendeleo na hatimaye miradi ile hakuna hata mmoja unaokwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ni baya sana linafanyika, ni kwamba, Serikali hawakubaliani, zinakusanywa pesa chache katika robo mwaka, lakini kila Waziri katika kila Wizara anataka na yeye apate kidogo kidogo. Kwa hiyo, zile fedha zinakuwa zinagawiwa kidogo kidogo, hazileti *impact*, haziwezi zikatumika kufadhili mradi wowote ule wa maana ambao unaleta athari ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ikubaliane, kwa hiki kidogo kinachokusanywa sasa, basi mradi namba

moja huu, upatiwe fedha za kutosha u-*take off*; uendelee na ile miradi mingine isubiri kipindi kingine kuliko kugawiwa kidogo kidogo na hakuna lolote linalokwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana hapa kwamba, mgawanyo wa fedha za maendeleo na fedha za matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida; yawe kwa asilimia sitini na tano kwa matumizi ya kawaida na asilimia thelathini na tano ni matumizi ya maendeleo. Hilo limesahauliwa kabisa, fedha zikipatikana moja kwa moja asilimia kubwa inakwenda kwenye matumizi ya kawaida, huku matumizi ya maendeleo yanasahauliwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipobadilika hatutayapata maendeleo ambayo tunategemea kuyapata, ya kuhamisha nchi yetu kutoka hali ya umaskini kwenda katika hadhi ya kipato cha kati, haitawezekana, tutakuwa tuna *mark time* hapo hapo hatuendi mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine limezungumziwa ni la aibu kulisema, kwamba, wafadhili wanashindwa kuchangia wakati mwingine, kutokana na kuwa wataalam wetu wanashindwa kuandika maandiko ya miradi yanayokidhi matakwa ya wafadhili hao. Huu mwaka wa 50 tangu tupate uhuru, wataalam kila siku wanasomeshwa, kuambiwa hilo bado ni tatizo sugu, wengine hatuelewi. Hivyo, Serikali iweke nia safi, ifundishe wataalam wetu, tusikose fedha kwa sababu ya maandiko. Karne hii ni ya sayansi na teknolojia na watu wetu wana akili, wakifunzwa, miradi itapatikana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani bado watu hawajaweka msisitizo huo, pengine ni jambo lililokuja juu juu tu, tuanzisheni miradi, lakini hatukujipanga vizuri katika mambo madogo madogo kama hayo; kwa sababu hilo naliona ni jambo dogo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kurudia utaratibu wetu wa *capital* bajeti na tukaachana na *cash* bajeti, limezungumzwa na wengi sana. Tulifanyie utafiti wa kina na

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kuona ipo haja sasa ya kubadilika. Tusibakie pale pale, tumeshaona panatutia matatizoni, kwa nini tusirudie kule kwenye utaratibu wa *cash* bajeti? Zikatafutwa fedha mwaka huu, ambazo zitatumika kwa mwaka ujao, kwa utaratibu wowote ule utakaoonekana ni muafaka; tunaweza kukopa au tunaweza kufanya utaratibu wowote; Serikali ipo, fanyeni utafiti tuone, hili kila mmoja analiona kuwa linaweza likatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ukomo wa kukopa. Ukomo wa kukopa tumewekewa na taasisi za *IMF*, *World Bank*, kwamba tusizidi, lakini na Wizara ya Fedha inaweka vikomo hata kwa taasisi ambazo zinajitegemea, waondoe huo ukomo kwa hizo taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Kapteni Komba na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Mpango huu ambao tumeletewa hapa, lakini ninavyoona hapa, watu wengine wakisimama ni kubeza tu, kubeza tu! Inafika mahali mpaka mtu anamlinganisha Rais wetu anayeongoza karibu watu milioni 50 na mtu ambaye ana watu milioni tisa au milioni kumi na nchi yake inaingia kwenye nchi yetu zaidi ya mara kumi na tano, kwamba huyu ndiye kaweza ila wa kwetu hakuweza. Kwa kweli hapa hatutendi haki, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukubwa wa Tanzania jumlisha nchi tano inazozizunguka, jumlisha Kenya, Uganda, Burudi, Burundi, Rwanda na Malawi. Hizo zote zinaunda asilimia 48% tu, lakini bado tumeweza kufanya vitu ambavyo hata wengine hawawezi kufanya. Leo ukichukua umeme ulioko Tanzania, ukausambaze Rwanda, haki ya Mungu utakwenda mpaka vyooni, mpaka makaburini watatembea

kwa lami. Peleka mashule yaliyopo Tanzania, uyapeleke Burundi, mengine yatakaa angani. Peleka chochote unachokifikiri wewe, tumefanya, watu wanasahau!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nasoma Sekondari, nilikuwa nasoma Songea *Boys*, miaka kama 40 iliyopita. Unatoka Songea unakwenda Tabora likizo unatumia siku saba. Siku nne mpaka Dodoma, siku tatu mpaka Tabora. Leo ukifiwa Mwanza unatoka Songea unatumia siku moja na nusu, unafika kuzika kama ndugu yako amekufa Mwanza. Haya siyo maendeleo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuyaseme, tumefanya lakini kuna upungufu, moja, mbili, tatu, hiyo ni sawa, hakuna mkamilifu bwana. Mkamilifu ni yule aliyezikwa futi sita chini, hafufuki mpaka Yesu Kristo atakapokuja tena, huyo ndiyo kakamilika, *otherwise* hakuna mkamilifu hapa. Sasa upo upungufu, kwa mfano, huu Mpango ambao tumeletewa hapa, ningefikiri kwamba, ungetueleza katika vipaumbele vya mwaka jana, katika miundombinu tumekamilisha asilimia kadhaa, katika elimu asilimia kadhaa, katika afya asilimia kadhaa, katika hiki asilimia kadhaa. Sasa mpango huu tunauleta kwa ajili ya kuboresha haya ya mwanzo na kuleta mengine mapya. Hii sijaiona, kwa hiyo, hapa kuna upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisi wanasiasa tunasimamia sera, lakini tatizo linapokwenda kwa watumishi wa Serikali kule, ni yule yule aliyekuwa tangu mwaka 60, huyo huyo anaendelea mwaka 70, 80, 90, mpaka 2000na uzoefu wake ni huo huo wa mwaka huo. Kwa hiyo, tunaangushwa na watumishi wa Serikali, hawa walioko Serikalini. Tunapanga mambo vizuri, lakini yakifika anatumia uzoefu tu, tunafanya mipango mizuri, lakini ukifika kwake anafanya uzoefu, hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo sikuliona kwenye mpango ni kuhusu Mtwara *Corridor*. Mtwara *Corridor* ni kama sasa umekufa, hauzunguzwi chochote, yaani hauzungumzwi kwamba kuna mradi mkubwa ambao utatukomboa sisi Watanzania na wenzetu wa Kusini mwa

Afrika. Kidogo kuna barabara zinatengenezwa, ndiyo, lakini Bandari ya Mtwara imezungumzwa tu lakini kwa kweli sioni juhudi kubwa ya kuitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Mbaba Bay imezungumzwa tu lakini ukifika Mbaba Bay ni kichekesho kitupu. Kwa hiyo, Mbamba Bay haiwezi kuwa kiungo kati ya Tanzania na Malawi na nchi nyingine za Kusini mwa Afrika. Kwa hiyo, kwa kweli naomba katika mambo ya bandari, jambo hilo lingetiliwa mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maziwa, naona bahari imezungumzwa, lakini kwenye maziwa hakuna kilichozungumzwa hasa katika mambo ya usafiri. Mpaka leo Ziwa Nyasa linatumia usafiri wa Malawi, mpaka leo usafiri wa Malawi, lakini mpango wa kunusuru Watanzania wale ili wajione kwamba wako Tanzania, mpango huo tumeusoma mwaka jana na nimeusoma mwaka huu, haupo. Sasa sisi ni wa Malawi au Watanzania bado?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Waziri atakaposimama atueleze mpango huu wa kutunusu sisi wengine kuitwa Wamalawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo; nilipongeze sana Shirika la SUMA ambalo mwaka jana lilipoleta matrekta angalau kilimo chetu kiliinuka kidogo, kutoka pale tulipokuwa mpaka hapa tulipofika. Hata hivyo katika Mpango nimeangalia hapa kuinua Shirika la SUMA liendelee kuleta matrekta ili kilimo chetu kipande juu, sijaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokijua ni kwamba, SUMA wanalalamika sana, viongozi wetu wanakwenda pale, ndiyo wamehamasisha kilimo, lakini wanakopa matrekta, fedha hazirudi, wanasema aah, sisi tulikuwa tunahamasisha na matrekta haya ni kwa ajili ya kuhamasisha, SUMA

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



wanaomba zile fedha mlizokopa mrudishe ili SUMA ipate uhai. Rudisheni zile fedha za matrekta ambazo viongozi mmekopa, wanalalamika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie uvuvi; nimeangalia katika Mpango kuna uvuvi wa Bahari Kuu tu, uvuvi wa Maziwa na Mito hakuna. Sasa samaki wengi wanaovuliwa na kupelekwa nje, wanatoka kwenye maziwa na hasa Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa kwa upande wa Malawi, lakini halizungumzwi katika mipango yetu, tunafanyaje uvuvi katika maziwa haya makubwa? Mpango huo hauko kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye Mpango wenyewe hakuna, nimesoma kwenye hotuba ya Waziri mhusika hakuna. Sasa naomba sana, tukitaka kukuza uvuvi ndiyo bahari ipo, lakini pia mito na maziwa yamesaidia sana katika kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kivuko. Vimetajwa vivuko vingi mle ndani, kuongeza na kufanikisha vivuko, lakini kipo kivuko kimoja ambacho kipo kwenye Ilani ya Uchaguzi, kivuko cha Mto Ruhuhu ambacho kinaunganisha mikoa mitatu; watu hawawezi kwenda Iringa, Njombe wala sehemu yoyote wakitokea Ruvuma. Kwa hiyo, sehemu ile imekuwa kama vile imefungwa, ni *land locked*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana katika vivuko vile na kwa kuwa Ruhuhu ilikuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi na bado tuna miaka miwili tu au mmoja na nusu, naomba sana jambo hili litekelezwe tuliweke katika mpango wa mwaka huu ili mikoa ile ambayo inazalisha mahindi na chakula kwa wingi waweze kutumia daraja hilo la Mto Ruhuhu kuvusha vyakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nipongeze Mpango huu na niwaombe watumishi wa Serikali waupokee vizuri, wakifanya vizuri nina hakika kabisa tutaondoka hapa tulipo. *Wasalaam allaykum*, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Komba. Sasa ni Mheshimiwa Riziki Lulida, ajiandae Mheshimiwa Meshack Opulukwa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa katika afya njema, hivyo kuweza kuchangia katika hoja iliyopo mezani. Sera tunazo nzuri, lakini tunapaswa kuzisimamia ili tupate mafanikio katika hizi sera ambazo tunaziweka mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la kilimo. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ilisema, mikoa iliyoko pembezoni itapewa kipaumbele cha maendeleo. Nilitarajia katika mikoa hiyo yote ya pembezoni mmojawapo ukiwa ni Lindi, Mtwara na mikoa ya Rukwa wakati ule na Kigoma, ndiyo mikoa ambayo ilikuwa nyuma kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoona sasa hivi, mikoa mingine angalau inaonesha kufuatiliwa na kusimamiwa wanaendelea. Mikoa mingine imegawanywa na katika kufanya hivyo maendeleo yamezidi kuboreshwa na wenzetu wanaendelea, lakini Mkoa wa Lindi bado uko nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuunge mkono Mbunge aliyemaliza kuchangia sasa hivi kuhusu Mtwara *Corridor*. Tulitegemea Mtwara *Corridor* ingetusaidia wananchi wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, lakini Mtwara *Corridor* haipo. Kwa vile haipo tukategemea *SAGCOT* itasimamia Mikoa ya Kusini ambayo imeingia katika mradi ule; Lindi, Mtwara haipo. Sasa je, tunataka tulete maendeleo ya kilimo, mikoa hiyo hatupo popote, tunayumbayumba tu, tunategemea sera hii ya maendeleo ya kilimo mtausaidia vipi Mkoa wa Lindi?

*[MHE. RIZIKI S. LULIDA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho katika Mkoa wa Lindi lilikuwa la kwanza kuingiza fedha za kigeni katika miaka ya sitini na mpaka sasa hivi korosho inaingiza fedha za kigeni, lakini Viwanda vyote vya Korosho viliingia katika uwekezaji na mpaka leo hatujajibiwa na Serikali uwekezaji wa viwanda vile unafanya nini hata kiwanda kimoja hakifanyi kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa Lindi hawana kazi, wanakimbilia Dar es Salaam, huko wanakimbizwa kimbizwa hawana pa kwenda. Waziri mwenye dhamana, awe ni wa Kilimo, Viwanda na Biashara aseme vijana wale tuwapeleke wapi ili na wao waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Lindi wanalima ufuta, lakini soko la ufuta hatuna. Usimamizi wa soko la ufuta haupo, korosho ndiyo zimekaa majumbani, hawajui watazipeleka wapi, lakini ukiangalia nje, soko la korosho ni kubwa na hata ukiingia ndani ya ndege unakula korosho kwa bei ya juu. Hii ina maana usimamizi wa sera zetu za maendeleo ya masoko umekuwa mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa ardhi, nyumba na makazi. Tunakuja katika miji mipya *new cities, programs* zake ziko wapi? Mipango miji ya miji mipya iko wapi? Nitoe mfano ambao nataka nione pengine tukipiga hesabu hizo Serikali italiona, kuna Kigoma nauona kama unawekwa katika miji mipya una uwezekano wa kufika katika maendeleo ya miji mipya, kwa vile uta-*link* na Burundi, Rwanda na Kongo, pale pakitengenezwa mji mpya pataweza ku-*link* katika masuala mengi ya maendeleo.

*[MHE. R. S. LULIDA]*

Kilwa, katika historia ya miaka ya 1690 ilikuwa Makao Makuu ya *East Africa* na sasa hivi kuna madini, kuna Mbuga ya Selous, mbili ya tatu ipo Kilwa; lakini je, Mpango wa Kilwa uko wapi?

Tuna kiwanda cha Songosongo. Ukienda pale Kilwa ukaambiwa inatolewa gesi huwezi kukubali kama pametolewa gesi; watu ni maskini. Je, tumejipanga katika mipango bora ya maendeleo ya Wananchi wa Kilwa?

Tunafika mahali tunajiuliza, kama Mipango hii itakuwa ni ya *work and see attitude* hatuendi; tutakuwa tunapiga porojo za kuongea hapa lakini maendeleo yatakayotoa tafsiri hayapo. Leo najiuliza, Sera ya Madini, inabidi ije hapa ili ikishafika hapa Wananchi ambao wataondolewa katika maeneo yao watapata nafasi ya kufaidika na maendeleo ya madini, lakini Sera hakuna!

Kama Sera hakuna watu hawa watafanya nini, wataondolewa kwa shilingi 400,000 halafu watafanya nini na shilingi 400,000, akiondolewa kwa milioni mbili atafanya nini na miloni mbili! Tunataka yule mtu anayekutana na madini katika eneo lake afaidike. Nataka nitoe mfano, Wachina kwao wanatetea uchumi wao, lakini wakija kwetu wanaongoza katika kuvuruga uchumi wa Tanzania. Sisemi wote, lakini *majority* ya Wachina na Waasia wamekuja Tanzania hapa siyo kutusaidia katika maendeleo, wengi wao wamekuja hapa kutuvurugia maendeleo. Ndiyo maana tunajikuta wamepewa nafasi kila eneo wamejaa; ukienda Vijijini kila maeneo wamejaa, lakini hawajakuja na mazingira ya kutusaidia, wamekuja katika mazingira ya kupora uchumi wetu kwa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninawataja Watu wa Asia? Ninataka nichuke sehemu ndogo sana ya Utalii wa Tanzania; Utalii wa Tanzania upo katika asilimia 18.7, lakini leo hii wao wanakuja kumaliza Tembo kwa faida yao. Ukienda kule Asia, Tembo anatunzwa, inakuwa kama ni kivutio kikubwa. Sasa je, kwa nini tunaendelea kuwaacha

*[MHE. R. S. LULIDA]*
hawa watu wakitufanyia fujo na sisi hatuna *action* ya aina yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa ambayo ni sahihi na baadhi ya Wabunge nilikwenda nao Katavi, Mchina alikutwa na lori limejaa pembe. Alipopelekwa Mahakamani wakasema huyu hajui Kiingereza na Kiswahili, anashindwa kuchukuliwa *action* yoyote! Leo tumefikia utalii wa Tanzania ni wa *Wildlife*, ni wa Mifugo ya Wanyamapori na wanafanya fujo sasa hivi kupeleka sumu katika Mabwawa, bwawa lile Simba na Nyati wanakufa na wanyama wote wanaokwenda kunywa maji. Sasa je, *survival* ya utalii Tanzania itafikia wapi?

*Are we serious? Are we committed? Are we monitoring* wanavyofanyiwa wanyama wetu au tuko hapa tunaangalia tu? Tunahitaji sasa hivi juhudi ya pamoja na Wabunge wenzangu naomba tuunge mkono suala hili la fujo ya wanyamapori limekuwa *critical*, ni janga la Taifa.

Napenda ku-*declare interest,* kwanza, mimi ni Mwenyekiti wa Kusimamia Mauaji ya Tembo na Vifaru ndani ya Bunge la Jamhuri. Pili, bado ninaupenda utalii wangu wa Tanzania ukue, lakini kama haukui ina maana watalii watakuja kufanya nini Tanzania! Kama Tembo hamna, kama Kifaru hamna, kama Nyati hamna, pana utalii hapo? Hamna utalii, usimamizi bora wa utalii wetu uwe mazingira bora kwa kila Mtanzania, asimamie utalii. Kwa nini ninasema hivyo? Kuna Vijiji vinazunguka Mbuga zetu za Wanyama, lakini maeneo yale wamepewa vitalu, watu wanawinda kipindi cha *corridor* ya wanyama wanatembea. *(Makofi)*

Natoa mfano wa Miasa, Mozambique, pale pana vitalu karibu sita karibu na eneo la Tunduru, wanapewa watu kuwinda kipindi kile wanyama wanapita kwa fujo. Kipindi cha neema zao, wao wanawindwa, wanauawa na bado tunaiona Asia kama ni sehemu ya kuisaidia. Naomba Wabunge, tujumuike kwa pamoja, tuone janga la Taifa letu la Utalii linauawa na Asia. Wamekuwa ni watu waharibifu katika nchi yetu, kwao wanatangaza utalii. Tumefikia mahali

tunajiuliza, kama utalii unaingiza pato kubwa namna ile, bado wao wanaamua kutuhangaisha tunawachukulia *action* gani ya kina?

Mnasema, tutafute siku tuandae maandamano ya mshikamano wa kupinga Asia kuharibu utalii wetu Tanzania. Tupeleke malalamiko yetu *UN*, hili suala la *hunting* life tusiendelee nalo tena.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Riziki!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Opulukwa, ajiandae Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa Leticia Nyerere pia ajiandae!

**MHE. MESHACK J. OPOLUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Mpango wa Maendelo wa Taifa. Ningependa nianze na barabara za kupunguza msongamano wa watu na magari kwenye Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu imeelezwa kwamba, kutakuwa na *flyover* moja kwenye eneo la *TAZARA*. Kwa bahati mbaya sana, aliyekuwa anaandaa Mpango, *either* alipitiwa au hakuona umuhimu; anaweka *flyover* eneo la *TAZARA*, lakini kuna barabara inayojengwa ya mabasi yaendayo kasi kutoka Kimara mpaka *City Centre*, hakuna *flyover* iliyoandaliwa kwa ajili ya Ubungo, hakuna *flyover* iliyoandalia au iliyoko kwenye Mpango kwa ajili ya Magomeni na kwa ajili ya Fire. Sasa haya mabasi yatakayokuwa yanakwenda kwa kasi, yatakwenda kwa kasi ipi wakati yakifika kwenye *junction* nayo yana-*stack?*

Kwa hiyo, naomba sambamba na *flyover* ambayo itakuwa inajengwa pale *TAZARA* au ule Mpango ambao umeandaliwa kwa ajili ya *flyover* ya *TAZARA*, basi hizi *flyover* nyingine tatu ambazo nimezitaja, ziingizwe kwenye Mpango huu ili kuweza kuufanya Mradi wa Mabasi Yanayokwenda Kasi uweze kuwa na mafanikio na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea suala la Mji wa Kingamboni. Mpango unasema maandalizi ya ujenzi wa Mji wa Kigamboni yanaendelea, lakini kwa mstari mmoja tu na nusu, hakuna maelezo ya kujitosheleza kabisa katika Mpango huu ambao tunauongelea hapa ili kuweza kuupitisha. Wananchi wa Kigamboni, zaidi ya miaka minne sasa wamekuwa wakiishi kwa matumaini, wamekuwa wakiishi wakiwa *ICU*, hawajui wafanye nini, hawajui waishi vipi. Wameanza kuzaliana tangu wakiwa wanakaa chumba kimoja, mwaka au miaka minne iliyopita mpaka leo bado chumba ni kile kile, hawaruhusiwi kuendeleza lakini Serikali imekaa kimya!

Sasa kumeanza minong'ono mingine ambayo inaendelea kuhusu Mji wa Kigamboni inasema na ningependa Waziri mwenye dhamana, alitolee ufafanuzi kwamba; itakapofikia muda wa fidia, Serikali imepanga kulipa shilingi 35,000 kwa *square metre* moja kama fidia kwa wale ambao watahamishwa, lakini shilingi 700,000 kwa *square metre* moja kwenye eneo ambalo ni *built up area*. Kwa maana hii hakuna nyumba ambayo italipwa chini ya shilingi milioni 70 na kuendelea.

Wananchi walikuwa wanataka kujua; bahati mbaya sana hata Mbunge wao, Mheshimiwa Ndungulile, hayupo hapa, inabidi niwasemee kwa sababu hawana mtu wa kuwasemea. Serikali itafute fedha kwa ajili ya kulimaliza tatizo la Kigamboni, kwa sababu Wananchi wamekuwa wakiishi kwa matumaini kwa muda mrefu, hawajui hatima yao, hawajui kama ni fidia italipwa lini na ni shilingi ngapi kwa *square metre* moja. Naomba wakati Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana anahitimisha, basi awaambie Wananchi

*[MHE. M. J. OPOLUKWA]*
wa Kigamboni waweze kujua hatima yao na mambo yatakwisha lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la utalii, kuna maeneo mawili ambayo nimeona leo ni bora niyazungumzie. Tunasema utalii unaingiza fedha nyingi sana kwenye Serikali yetu, lakini kuna maeneo ambayo yamesahaulika ambayo napenda Serikali iweze kuyafanyia kazi. Kuna eneo moja ambalo liko pale Mkarama, pale kulikuwa na Wajerumani walioishi miaka ya zamani, kuna magofu ambayo yako pale, ambayo Serikali ingeweza kuyawekea mkakati wa kuyatengeneza na kuyalinda, nadhani yatakuwa kivutio kikubwa sana kama malikale kwa ajili ya watu ambao wangependa kwenda maeneo yale kuangalia jinsi ambavyo Wajerumani waliweza kuishi na kufanya kazi zao. Kuna magofu ambayo yanavutia kuzidi hata yale ambayo nimeyaona kule Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha eneo la Mkarama, kuna eneo lingine ambapo aliwahi kuishi Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, eneo la Gezaulole Kigamboni. Eneo hili lilikuwa ni *root* ya Watumwa waliokuwa wakitoka *interior*, wanafikia maeneo ya Kigamboni halafu wanasafirishwa wanakwenda maeneo ya Bagamoyo kabla ya kupelekwa maeneo mengine. Ukifika kwenye eneo hili, maji yanapokuwa yameondoka katika eneo lile utakuta kuna magofu yako pale ndani ya maji.

Ninadhani ingekuwa ni wakati mwafaka sana kwa watu wa *archaeology* kufika pale ku-*study* magofu yaliyoko pale. Wangeweza kupata mambo mengine mazuri, ambayo yangeweza kuwa hazina kubwa kwa ajili ya watu wanaojifunza historia, kwa wanaikolojia pamoja na watu wengine wanaokuja kufanya utafiti kuhusu maisha ya Watanzania hapo zamani wakati wa biashara ya watumwa**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *issue* ya *TASAF*; *TASAF* wamekuwa wakilalamika muda mrefu kwamba, hawapati fedha za kutosha, lakini maeneo ambayo wamekuwa

*[MHE. M. J. OPOLUKWA]*

wakipata fedha za kutosha, zile fedha zimekuwa *misused*, au zinakuwa *mismanaged*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 7 Julai, pale Meatu, *TASAF* walikuwa wanagawa vyerehani kwa ajili ya vikundi vya wajasiriamali. Kwa bahati mbaya sana *TASAF* Meatu wanatumika kama chombo cha Chama cha Mapinduzi. Alikuja Mwenyekiti wa Mkoa wa Simiyu, ambaye pia ni Mbunge katika Bunge lako Tukufu, wakachukua vyerehani vilivyokuwa vinagawiwa na *TASAF*, vikapigwa rangi ya kijani vikaandikwa CCM, halafu kwenye mkutano wa hadhara, wakaenda kuzigawa kwamba hii ni mali ya Chama cha Mapinduzi. Hii ni aibu na suala hili halikubaliki. Ninaomba Viongozi wenzangu ambao pia ni Wabunge pamoja na Viongozi wa Serikali kama *DCs* na watu wengine, tuiache *TASAF* ifanye kazi yake kama ambavyo inaelekezwa katika miongozo ya utendaji wa kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea ukurasa wa 26 kuhusu ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti. Hauwezi kuongelea ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti bila kuongelea barabara ambazo zinaelekea ambako daraja linajengwa. Daraja hili ni kiungo kikubwa sana kwa Mkoa wa Singida, Shinyanga, Simiyu mpaka wanaotokea Mara na nchi za jirani.

Ninaomba katika Mpango unaokuja, pamoja na kwamba, barabara ipo kwenye upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuwekwa lami, lakini sasa yale madaraja ambayo ni ya chini, madaja yote ambayo yamewekwa kalvati yajengwe yawe ya juu ili daraja lile litakapokamilika hata kama itakuwa bado haijawekwa, basi magari yaweze kupita juu na Mkoa wa Simiyu, Shinyanga, Singida, pamoja na Mara, waweze kufaidika na ujenzi wa daraja hili pamoja na barabara zake zinazoingia katika Daraja hili la Mto Sibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea suala la Pamba. Kipindi hiki ni cha msimu wa kuanza kilimo cha pamba, lakini nimepata taarifa kwamba, Wananchi wameanza kulazimishwa kujiunga kwenye vikundi ili waweze kuuziwa mbegu za pamba. Yule ambaye hatajiunga

kwenye kikundi hatapata mbegu na kwa hiyo hataweza kulima Pamba katika msimu huu unaoanza sasa. Ninaomba Serikali itoe tamko kwa watu wote ambao wanalima pamba Tanzania, kama ni kweli ili mtu aweze kupata mbegu ya pamba ni lazima awe amejiunga kwenye kikundi, kwa sababu Wananchi tayari wameshaanza kukwazika.

Ninaamini Serikali ikishirikiana na wadau, kwa kuandaa mbegu bora ya pamba ambayo ni *UK 91* iliyotolewa manyoya, ni kwamba inaweza ikazalisha ile *productivity* ikawa kubwa sana. Wananchi wameshaanza kukwazika kwamba kama *productivity* inakwenda kuwa kubwa kiasi hiki; kwa nini kuanze kuwa na vikwazo vingine ambavyo Wananchi wanaona kwamba hili ni tatizo!

Kwa hiyo, naomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja hii, awaambie Wananchi wa maeneo yanayolima pamba kwamba, siyo lazima au kama ni lazima mtu ajiunge kwenye kikundi ili aweze kupata hiyo mbegu ya pamba ambayo ni pamba bora ya *UK 91.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilishangaa sana aliposimama aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Maige, akiwa analalamika na anashangaa, anasema Wananchi wanaonewa, wafugaji wanaonewa, wanatozwa shilingi 500,000 mpaka milioni 32 wakati yeye ndiyo alikuwa Waziri mwenye dhamana na haya yote yametokea kwenye kipindi chake! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mkuki kwa Nguruwe, kwa binadamu mchungu. Leo yuko *back bencher* huku, sasa ameanza kuona machungu ya Wananchi wake wanavyoteseka. Mambo yanayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, aliyokuwa anayafanya yeye mwenyewe, tayari ameshaanza kuona limekuwa tatizo. Hili nadhani ni mfano mzuri kwa Waheshimiwa Mawaziri mlioko hapa; mnapokuwa mbele hapo, hebu fanyeni yale ambayo Wananchi wanawategemea.

Mheshimiwa Mweyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2014/2015, kama ulivyowasilishwa na Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niseme kwamba, Watanzania tumekuwa wazuri sana kwenye Mipango, tunaandika Mipango mizuri, lakini tunafeli katika utekelezaji kwa sehemu kubwa sana. Sasa naiomba sana Serikali, wakati imetuletea Mpango na maeneo tunayoshauri ihakikishe yanakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kilimo. Kwa vyovyote vile ili nchi yetu iweze kuendelea ni lazima tuhakikishe Mipango yetu ya Kilimo inawekwa vizuri, lakini pia inatekelezeka. Vinginevyo, tutaendelea kuzungumza hapa lakini hatutaweza kupiga hatua au kuondoa umaskini wa Watanzania tunaotegemea hasa tukizingatia kwamba, zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima au wafugaji. Kwa hiyo, naomba Serikali ielekeze nguvu huko.

Ninasema hili, sijaona Mpango unaozungumzia. Kwa mfano, tunazungumza hapa suala la uanzishwaji wa benki hususan Benki ya Wananchi, suala hili lilishaingia kwenye Mipango muda mrefu sasa, lakini utekelezaji wake hauonekani. Maana yake, tunazungumza kwenye Mpango ukisoma amesema kwamba, tunaendelea na tijihada za kuanzisha Benki ya Wananchi ya Kilimo, mpaka leo tuko kwenye Dirisha la Kilimo ndani ya Benki ya *TIB*; lakini tijihada zenyewe za kuanza kujenga benki yenyewe ziko wapi? Tunazungumza Serikali imetenga fedha, lakini bado tunaendelea kutoa huduma ndani ya Benki ya *TIB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo haitoshi, suala la riba kwa mikopo hiyo ambayo inatolewa ndani ya Benki ya Rasilimali ya Taifa lakini Dirisha la Kilimo, bado mikopo ile haiwanufaishi Wananchi walio wengi, ambao ndiyo wanaweza pia wakasaidia sana kuchangia uchumi wa Taifa. Leo ukiangalia hata waliokopa kwenye Benki ile, bado

ni watu wakubwa wenye uwezo wao, lakini angalia Watanzania wa kawaida ambao wamekopa. Ninachosema hapa, hata masharti ya mikopo, hayako *favorable* hata kidogo kwa wakulima wadogo.

Kwa hiyo, tunataka wanapotuandikia waje na Mpango ni kiasi gani wakulima wadogo wadogo watafaidika na bajeti hii tunayoitegemea ya mwaka 2014/ 2015; vinginevyo, sioni namna.

La pili, tumezungumzia pia suala la kuwa na matumizi sahihi ya mbolea, sioni tunapozungumzia ujenzi hasa. Ninajua Serikali inasema hatufanyi biashara, lakini kuna maeneo ambayo lazima ije na Mpango sawa sawa wa kujenga viwanda vya mbolea. Leo tuna Kiwanda cha Minjingu, tumeambiwa na imendikwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ujenzi wa kiwanda kingine cha mbolea kule Mtwara. Sioni kuna mpango gani ambao wanatuambia Kiwanda cha mbolea kinachotarajiwa kujengwa kule Mtwara kinakamilika lini ili Wananchi wa Tanzania wawe na matumaini kwamba wanaweza kupata mbolea hivi karibuni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie na hilo; hivi tunakuwa na Mipango gani; sisi Mbeya tulishazungumza, jamani mbolea ya Minjingu haiwafai Wananchi wale kwa ajili ya uzalishaji wa mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza na hili nitaomba Serikali ilijibu, kwenye Mipango tena kuanzia mwaka 2008, tulishazungumza Mkoa wa Mbeya maeneo mengi mbolea ya Minjingu haifai na kwa kweli hata katika maeneo mengine katika nchi hii, mbolea ya Minjingu haifai. Serikali ikasema haina virutubisho vya kutosha tutairutubisha, tumetengeneza Minjingu Mazao, Minjingu Mazao imetumika mwaka jana, lakini matokeo bado yamekuwa mabaya.

Ninashangaa na nitaishangaa Serikali ya Chama changu kama itaendelea kuwalazimisha Wananchi waendelee kutumia mbolea ya Minjingu ambayo haina tija.

*[MHE. G. W. ZAMBI]*

Aliyekuwa wakala wa mbolea ile kule Mbozi mwaka jana, mwaka huu amekataa kwamba hataisambaza tena kwa sababu mpaka leo Wananchi hawajaitumia ipo kwenye ghala, amepata hasara. Mwaka huu Serikali inatuletea mbolea hiyo hiyo Wananchi waendelee kuitumia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Mbozi, Ileje, Momba na Wananchi wa Mbeya Vijijini, wamesema hiyo mbolea hawatakuwa tayari kuitumia; na kwa maana hiyo, tutegemee ruzuku ya Serikali, kama tutaendelea kuwang'ang'aniza mbolea ya Minjingu hawatakuwa tayari kuitumia. Bahati nzuri nimeongea na Mheshimiwa Waziri Chiza, kama ananisikia popote alipo, basi wahakikishe kwamba, ili kuendeleza Mipango mizuri ya kilimo na kuhakikisha Wananchi wale wanaweza kulima vizuri tena kwa tija, basi watuletee mbolea ya kupandia ya *DAP* ambayo Wananchi walishaizoea. Serikali ikifanya hivyo, nadhani Mipango yote tunayoipanga kwenye Sekta ya Kilimo na ustawi wa Wananchi basi unaweza ukapatikana kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa nilizungumze ni la Kiwira. Inasikitisha tunavyopanga Mipango ya nchi hii; kwenye mipango ya nchi tuna maeneo mengi, lakini nizungumzie hili la makaa ya mawe, mengine Waziri ameyazungumza Mipango inaonekana. Suala linalosikitisha ni la Makaa ya mawe Kiwira. Makaa ya Mawe Kiwira, alipokuwa Waziri Mheshimiwa Ngeleja alituambia kwamba, mipango yote imekamilika, tumeshamaliza na tunasubiri mwekezaji pale. Amekuja Waziri wa sasa Mheshimiwa Profesa Muhongo, akatuambia tumeshamaliza tunachosubiri ni utekelezaji. Juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara ya Uchina ndiyo nimefahamu kwamba kumbe Mpango ule bado haujakamilika na Serikali inaendelea kufanya mazungumzo; na kwenye Mpango ndivyo wanavyozungumza Serikali inaendelea kufanya mazungumzo. Tunawadanganya Watanzania, tunawapa matumaini na mambo ambayo hayajakamilika.

*[MHE. G. W. ZAMBI]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hebu tunapokuja na Mipango tuweke na *time frame*; Mpango huu tunaouleta utekelezaji wake unachukua muda gani. Ukiweka Mipango ambayo ni *open-ended*, hatuwezi kufika hata kidogo. Wenzetu waliofanikiwa wanapokuja na Mpango wanaweka na *time frame*, kila jambo linakuwa na *time frame* yake; lakini ukiacha hivi hivi hatutaweza kujua tunatekeleza lipi na tunaacha lipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni la elimu. Kwanza, hili limenichanganya kidogo na ukisoma kwenye Mpango wenyewe, inaonekana elimu kama vile haipewi kipaumbele kinachotakiwa. Kwenye yale maeneo sita ya mwanzo yanayozungumzwa, elimu haizungumzwi kwa ujumla wake. Nataka nijue tuna mipango gani inayotekelezeka hasa katika suala la ujenzi wa maabara, kumaliza madeni ya walimu na pia kuhakikisha madawati yanakuwepo shuleni na kuhakikisha walimu wanakuwepo wa kutosha?

Mipango hii iweke wazi ni lini hasa tunamaliza matatizo ya walimu katika shule za msingi na shule za sekondari. Tunajua Serikali inafanya jitihada, lakini tuwe na *time frame*, tusiseme tu kwamba tunajua *by 2014/2015* inawezekana tukamaliza. Tuwe na *time frame* inayoeleweka kwamba, tutamaliza matatizo haya ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Mipango ya Maji. Kama kuna maeneo ambayo tutafeli ni pamoja na suala la maji. Leo ukifuatilia bajeti iliyopitishwa ya maji ya zaidi ya shilingi bilioni 500, haijaanza kutekelezeka mpaka ninavyozungumza. Tulikuwa na Mpango tunasema lazima tuhakikishe Watanzania walio wengi wanapata maji, sasa kama leo ndiyo tunaanza *quarter* ya pili pesa za maji hazijaanza kutoka tunategemea nini? Nilikuwa nasoma *documents* za Serikali, kwamba Serikali au Idara mbalimbali ndiyo zimeanza kupata pesa sasa hivi, lakini *quarter* nzima ya kwanza hazikupata. Sasa hii Mipango tunayoipanga utaitekeleza namna gani kama pesa hazitoki?

Serikali tujaribu kuangalia, kama kuna tatizo kwenye ukusanyaji wa pesa Serikali iweke Mpango unaoeleweka kwenye ukusanyaji wa pesa. Vinginevyo, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Tunaweka Mipango pesa hazipo za kuitekeleza.

Wizara karibu zote, hakuna Mradi wowote wa mwaka wa fedha ambao umeanza kutekelezwa kwa sababu pesa hazitolewi. Kama tatizo liko Wizara ya Fedha, Serikali mje na tujue kabisa kwamba, tunahangaika namna gani katika kuhakikisha pesa zinapatikana za kutosha. Mimi nafikiri liko tatizo la matumizi au la ukusanyaji wa pesa, linalotokana na Wizara ya Fedha kwa ujumla. Nadhani Wizara ya Fedha bado kuna matatizo, panapaswa kutafuta utaratibu tuhakikishe pesa zinakusanywa mapema na ziende.

Pia ni vizuri Serikali ikatueleza kwa nini *quarter* ya kwanza yote imepita Wizara hazijaanza kupewa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo katika maeneo yao?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Leticia Nyerere, ajiandae Mheshimiwa Masoud Salim na Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika Mpango huu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Pato la Taifa. Kwa uelewa wangu, unapotafuta pato la wastani

*[MHE. L. M. NYERERE]*
la kila Mtanzania ni lazima ujue idadi ya watu Tanzania nzima. Cha kushangaza kwenye hiki kitabu wameonesha idadi ya watu kwa Tanzania Bara bila kuonesha idadi ya watu kwa Zanzibar. Sasa nashindwa kuelewa pengine labda nitahitaji ufafanuzi; tunapozungumzia Taifa, Zanzibar haiingii kwenye Taifa au inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie masuala ya uchumi. Inaonekana uchumi umepanda kwa asilimia 0.1, jambo ambalo ni la kusikitisha lakini kuna baadhi ya watu wanafikiri *it's a progress*, lakini ni jambo la aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya 60, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alisema yafuatayo: "Maendeleo si ya vitu bali ya watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa sasa kuzingatia hilo, kwa sababu tumejikita kwenye maendeleo ya vitu na wala si maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu tunajadili Mpango wa Maendeleo wakati Wananchi wa Kwimba hawana maji. Ni jambo la aibu tunajadili Mpango wa Maendeleo wakati wafugaji wananyanyasika nchi nzima. Ni jambo la kutia aibu tunajadili Mpango wa Maendeleo wakati wanafunzi wa Wilaya ya Kwimba na kwingineko Tanzania wanakalia mawe. Ni jambo la kusikitisha kujadili Mpango wa Maendeleo wakati akina mama wajawazito wanapoteza maisha yao kila kukicha kwa kukosa huduma ambazo ni *basic*. Ni aibu kujadili Mpango wa Maendeleo wakati hatuna barabara. Nasema ni aibu kujadili Mpango wa Maendeleo wakati Wamachinga wanazagaa mijini hawana maeneo ya kufanyia biashara.

Vilevile ni aibu kujadili Mpango huu ambao hauna tija kwa Taifa na Wananchi wake wakati wakulima wa pamba wananyimwa bei ya pamba yao. Nasema ni aibu kujadili Mpango huu wakati wakulima hawana pembejeo. Ni jambo la aibu na la kusikitisha, kukaa tunajadili Mipango isiyokuwa na ukomo wakati kwenye hospitali zetu hakuna

vifaa vya kutendea kazi ikiwemo Hospitali ya Ngudu Mjini, Kwimba. Ni aibu tunajadili Mpango usiowanufaisha Wananchi wa Tanzania wakiwemo akina mama wauza mboga wa Ngudu ambao wanatozwa ushuru usiolingana na kufanana na kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko makubwa, tumejikuta tuko hapa tunajadili Mpango unaosemekana wa maendeleo, ambao umewaacha nyuma Watanzania. Ni aibu kubwa kujadili Mpango wakati tukienda mijini kwetu watoto wa mitaani wamezagaa kila kona. Nasema ni aibu kujadili Mpango usiokuwa na tija, Mpango usiowajali wanafunzi wa Taifa hili ambao unawanyima mikopo yao ya shule ambayo wanastahili kuipata ili wajiendeleze na hatimaye wajenge Taifa letu. Ni aibu kubwa; narudia tena ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usemi unaosema kwamba, sasa hivi tuanze kuchukulia matatizo kama yalivyo na siyo kuyachukulia kama tulivyo. Ni aibu sana kuona tumeshindwa kujirekebisha, tumeshindwa kuwa *serious.* Ni aibu mifugo ya wafugaji inauawa; hatuoni aibu kukaa humu ndani tunajadili Mpango wa Maendeleo? Tunajadili Mpango wa Maendeleo ya nani? Tunajadili Mpango wa kitu gani kama siyo Watanzania wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa masikitiko na ninawaomba wenye dhamana ya kuongoza nchi hii, tubadilishe utaratibu wa kuendesha nchi. Ni jambo la kusikitisha, ni jambo la aibu kubwa, Wananchi wa Kwimba wanachangia maji na ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi, leo nimeletewa ujumbe hapa, Wananchi wa Ngudu Mjini hawajapata maji kwa siku saba na wanachota maji yenye tope kwenye Bwawa la Mwamasululu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kujadili Mpango ambao unawadidimiza Watanzania. Ni aibu kujadili Mpango wakati Wananchi wa Jimbo la Kwimba, wakiwemo

wale wa Hungumalwa, Mwamashimba, Jojiro, Hunge na Ngudu Mjini, hawana barabara na hata njia tu za kupitia hazijapaliliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unadhani hawa watapelekaje mazao yao? Hawa Wananchi wa Kwimba ambao wananyanyasika wana-*future* gani katika Taifa hili? Ni aibu, ni aibu, ni aibu, kujadili huu Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kaa chini Mheshimiwa!

Nakushukuru Mheshimiwa Leticia.

Waheshimiwa Wabunge, lengo la mjadala huu lipo katika Kanuni ya 94. Naomba mfungue Kanuni ya 94 mtapata mwongozo wa namna gani Serikali inahitaji msaada wa Bunge hili. Sehemu kubwa ambayo Serikali inahitaji msaada au ushauri ni vitu vitatu; kupokea kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali. Sasa tutoe maoni kuhusu vyanzo vya mapato ili Serikali iweze kutoa hiyo aibu.

Mheshimiwa Masoud, ajiandae Mheshimiwa Mhagama!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhanahu Wataala,* aliyenijalia uzima na afya njema na kuweza kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mpango, tuna maneno yasiyoonesha dira wala mwelekeo utakaoweza kuwanusuru Watanzania kuondokana na umaskini. Sifikirii

kwa utaalamu na Wataalamu wa Serikali mkatuandikia maandishi haya mkasema huu ni Mpango! Ni kweli tutaendelea kuangalia mikakati ya Serikali au tupendekeze mapendekezo ambayo yataweza kusaidia kuboresha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pendekezo langu katika Mpango wa Kilimo cha Mwani Ukanda wa Pwani. Wakulima wa Mwani wanahangaika; hawana masoko ya uhakika, bei ya mwani imekuwa ndogo, wanatangatanga, hawajaandaliwa mazingira mazuri katika Ukanda wa Pwani. Hii ni aibu nyingine ya Taifa hili. Hatutaacha kusema aibu hii kwa sababu mlipowasahau Wananchi wa Mtwara na Lindi, Dar es Salaam, Tanga, Visiwa vya Unguja na Pemba na Visiwa vingine vidogo vidogo, mkasahau mikakati ya Serikali ya kuboresha kilimo cha mwani ni aibu nyingine. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali iandae mikakati madhubuti ya kuhakikisha Zao la Mwani linaboreshwa katika dhana nzima ya MKUKUTA kama kweli Serikali ina nia hiyo ya MKUKUTA. Kama ni maneno tu yaliyoandikwa kwenye kitabu hiki ambacho kinasema kimetolewa na wataalamu; funika kombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Mtambile, kuna eneo la Kangani, Shehia hiyo na Kuu Kuu wanalima mwani. Bei yao wanayouza kule ni shilingi 400; ni ndogo sana. Ukiuliza maeneo ya Bagamoyo nao ni hivyo hivyo. Mimi ninaiomba Serikali iandae mazingira yaliyo mazuri juu ya kilimo hiki cha mwani. Masoko yatafutwe, ukitafuta masoko na masoko ni sehemu ya Mpango, Serikali ilielewe hilo, masoko ni sehemu ya Mpango. Kwa hiyo, kama hutafuti masoko ina maana Mpango huo ni Mpango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni uvuvi. Sekta ya Uvuvi tunajua inaingiza Pato la Taifa kwa asilimia mbili. Uvuvi unaajiri watu wengi; iwe wa baharini, kwenye maziwa na mito, watu karibu milioni nne tulionao Tanzania wanajiajiri katika sekta hii ya uvuvi. Mpango huu tulioletewa hauoneshi

*[MHE. M. A. SALUM]*

namna ya kuboresha maisha ya wavuvi hasa wavuvi wadogo wadogo wa kwenye bahari na kwenye maziwa. Hakuna kitu humu, Mpango huu ni fedheha nyingine. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi katika maeneo ya Pwani, ningetegemea katika Mpango huu basi wangelikopeshwa zana za kisasa, wakapewa mitaji na siyo Serikali ikawa mabingwa wa kuchoma nyavu zao moto; ni aibu nyingine. Mpango hauoneshi hapa. Ninadhani Serikali ikae iandae mazingira yaliyo mazuri, kama kweli kuna dhana ya kweli ya kuboresha wavuvi wetu, tuandae mazingira yaliyo bora waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu nyingine, tunaagiza samaki tunaletewa samaki wabovu hapa kutoka Japani, kutoka China, Afrika Kusini, wakati wavuvi wetu tumewaacha wanahangaika, hatuwakopeshi mitaji, tumekuwa mabingwa wa kuchoma nyavu moto tu; ni aibu nyingine. Ninaishangaa Serikali, nadhani tuwe makini sana; ni vyema tujipange katika mazao ya bahari, mazao ya kwenye maeneo ya maziwa ambapo sasa hivi magugu maji yanaendelea, mito hii au maziwa haya siku za mbele yanaweza kutoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la bahari linatupatia mapato mengi. Kwenye maziwa kama tunavyojua, asilimia kubwa ya uchumi wetu, sasa mikakati ya uchumi iangalie jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu tulioletewa na Wataalam hawa, dhana ya diplomasia ya kiuchumi, Mpango hauoneshi kabisa namna Serikali itakavyoongeza kipato na kutoa ajira kwa vijana wetu katika dhana nzima ya diplomasia ya kiuchumi. Hili linasikitisha sana kwamba, mpaka sasa sisi kama Tanzania tumekuwa na Mabalozi wetu na tunajipanga kuinua uchumi wetu, lakini hadi tunatoa maeneo au Serikali imekuwa na Ubalozi wake, hatujazifikia baadhi ya nchi. Hati za Uwakilishi, *to present credentials;* mfano, pale Abuja, sisi eneo letu la uwakilishi

*[MHE. M. A. SALUM]*
ni Nigeria, Benin, Togo, Cote d'Ivoire, Ghana, Guinea, Senegal, Burkina Fasso, Mali, Sierra Leone, Liberia, Guinea Bissau, Mauritania na maeneo mengine; lakini mpaka kufika hivi sasa hati ambazo ziliwasilishwa ku-*present credential* hakuna.

Maeneo ambayo hatujayafikia ili watu wetu waweze kutangaza vivutio vya utalii, kwenda kutoa maelezo kujitambulisha, ni maeneo mengi; Benin hatujafika, Togo hatujafika, Cote d'Ivoire hatujafika, Ghana hatuna, Guinea hatuna, Senegal hakuna kitu, Mali hakuna, Sierra Leone, Liberia, Buinea Bissau na Mauritania. Hii ni aibu nyingine. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya *Economic Diplomacy* ni kubwa, watu hujawafikia unataka utangaze vivutio vyako vya utalii. Tunazo fukwe zilizo nzuri na vivutio vingi vya utalii kama vile Ngorongoro na maeneo mengine mengi; hii kama siyo aibu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Berlin pale Ujerumani, hatujafikia kutangaza au kuwasilisha Hati zetu za Utambulisho kwa Jamhuri ya Czech, Slovakia, Holland, Hungary, Bulgaria na Romania; hii ni aibu nyingine. Miaka na miaka, maana mlituahidi hapa mtakwenda huko mpeleke mpaka leo; hii ni aibu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Rome pale Italia hatujafika Croatia, Marcedonia, Slovenia, Albania, Bosnia, Hesgovina na Serbia hatujafika. Kule Stockholm Sweden nako hatujafika Finland, Iceland, Latavia na Lithuania. Tumekuwa mabingwa wa kutembea na mikasi tu ya kukata utepe na makelele, amekata utepe; tutafika wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, dhana ya *economic diplomacy* ni kubwa, tusiwe mabingwa, tuna maboksi ya mikasi, anakuja Mheshimiwa anakata utepe makofi. Tunatafuta kura mwaka 2015 wembe ni ule ule, hatufiki ni aibu. *(Kicheko)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kusema kwamba, katika jambo ambalo silikubali hata kidogo katika Mpango huu, ukurasa wa 41 unazungumzia usafiri wa majini. Serikali haioneshi Mpango wa kuwanusuru Wananchi walioko katika visiwa vidogo vidogo. Katika Bonde la Mto Rufiji kuna visiwa vidogo vidogo kila siku watu wanakufa kule. Kila wakifa ninyi mnakwenda kutoa ubani na salamu za rambirambi huku mkitoa machozi kumbe muwaongo. Hii ni aibu, mngeliandaa boti za uhakika ambazo mtawanusuru wanafunzi wanaokufa kila wakati kule. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu hakuna chochote kinachoonekana; sijui tatizo ni wataalam au ni nani! Hii ni aibu nyingine kama siyo fedheha. Kama katika visiwa vile wanafunzi wale wataendelea kufa na hatutaki kuwanusuru; hili ni tatizo lingine. Serikali iandae Mpango wa kweli hasa usio huu wa maneno haya kwa hawa tunaowaita wataalam, ili kuwanusuru wanafunzi ambao wako katika visiwa vidogo vidogo wasipoteze maisha. Ubani wenu watu hawautaki tena, risala zenu za kufuta machozi, machozi siyo ya kweli ni ya uongo; hii ni aibu nyingine na fedheha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhagama, wajiandae Mheshimiwa Chombo na Mheshimiwa Malocha!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati watu wengine wakisema ni aibu, lakini mimi ninaomba niseme ni faraja kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Wananchi wa Tanzania, kwa kushuhudia hata Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni akiishukuru Serikali kwa mtandao mzuri wa barabara za lami hapa nchini na ambazo nyingi zimejengwa

hata kule kwenye Jimbo lake; kwa kweli ni faraja kubwa sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Vilevile ni faraja kubwa sana kwa Serikali ya Chama hiki cha Mapinduzi kwa kuona kwamba, kwa takribani muda mrefu sana katika nchi yetu ya Tanzania. Nchi hii haikuwa na Vyuo Vikuu, lakini Serikali hii kwa mfano mzuri sana mwingine imejenga Chuo Kikuu kikubwa sana hata hapa Dodoma; hiyo ni faraja kubwa sana kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi na ni faraja sana kwa Wananchi wa Tanzania. Watoto wanaosoma pale ni wa Watanzania wote bila kujali wa Chama gani wala wa Serikali gani. Hii ni faraja kubwa sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na ni faraja sana kwa Watanzania wa nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wengine wakilalamika ni aibu lakini mimi ninaendelea kusema kwamba ni faraja kubwa sana kwa Wananchi wa Tanzania; kwa sababu unaona kwa takribani miaka yote hii ya Uhuru, sasa hivi Serikali imeweka nguvu kupeleka umeme vijijini na mifano ipo mingi. Mifano iko mizuri katika nchi hii ya Tanzania mpaka Pemba kuna Mradi mkubwa sana wa Umeme. Kwa hiyo, nchi hii mimi ninasema mkitulia, Serikali ya Chama cha Mapinduzi Mipango hii tukitulia nayo ni faraja kubwa na ni heshima kubwa kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikutaarifu; juzi tarehe 29 Oktoba, nilikuwa nina mkutano mkubwa sana Peramiho, umeme unasambazwa pale Peramiho pote. Katika Kijiji cha Maposeni kote unapatikana umeme. Umeme unataka kwenda mpaka Mpitimbi, kule vijijini kote. Nilikuwa Wizarani tu hapa kwenye Wizara ya Nishati na Madini. Umeme huu wa Gridi ya Taifa njia ya Makambako, unapita Igawisenga, Wino, Maweso, Mkongotema, yaani mimi ninasema kule ni faraja tu. Mbunge Jenista na Serikali hii, ninajisikia faraja sana kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, wakati watu wengine wakisema ni aibu mimi ninasema ni faraja kubwa sana, kwa sababu

*[MHE. J. J. MHAGAMA]*

haya maendeleo, hata huo umeme ninaousema unakuja kwenye Vijiji vya Jimbo la Peramiho, unaenda hata kwenye vijiji vingi vya Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani, wa Chama Tawala, katika nchi nzima ya Tanzania. Kwa hiyo, ninasema hii ni faraja kwa Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipoanza Ubunge, watumiaji wa simu katika nchi hii ya Tanzania walikuwa wachache sana, lakini leo hii wanafika Wananchi karibu milioni 28. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba yapo maendeleo.

Ninachotaka kusema, ipo haja ya kutazama mambo haya sasa kwa ukubwa wake. Ninaomba kumshauri sana Waziri wetu anayesimamia Mipango, kupitia Kiti chako, shida kubwa hapa ipo kwenye rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye rasilimali fedha lazima tufanye kazi ya ziada. Tumejenga hivi Vyuo Vikuu vingi lakini, watoto wetu hawana mikopo. Mheshimiwa Wasira sasa hapo ndiyo tuseme kwamba pana kazi ya kufanya. Ninasema hivyo na ninawashukuru sana Wabunge wote, kwa umoja wao wananipigia makofi, kwa sababu wanajua mafanikio yanahitaji kupewa changamoto nyingine ambazo zitakwenda kutatua haya mafanikio. Kwa sababu karibu katika kila mafanikio lazima panakuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri sasa tushughulikie rasilimali fedha. Tumejenga Vyuo Vikuu, watoto watasomaje, lazima tuwe na fedha za kuwasomesha. Tumesema kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu la Tanzania. Hapo sasa Mheshimiwa Wasira kwenye Mipango yako ninategemea wewe na vichwa vyako vya Mipango, mtuondoe kabisa kwenye kuendelea na migogoro ya Sekta hii ya Kilimo. Kwa mfano, tunasema uchumi wetu unakwenda mbele lakini hali ya kipato kwa Wananchi bado iko chini. Sasa hapo ndiyo mahali tunapotakiwa kutafuta tatizo kubwa ni nini. Hapo lazima tujue; kwa mfano na mimi nillikuwa ninafikiri Mheshimiwa Wasira utakapokuwa

*[MHE. J. J. MHAGAMA]*

unajibu hoja yangu, umshirikishe sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, angalau mtuambie kwenye Mpango wa mwaka huu, tulikubaliana kwamba tunaanza kupunguza matumizi ya pembejeo kupitia kwa mawakala, kwa sababu tuligundua mawakala wametuangusha sana. Tukakubaliana tunaunda vikundi, nina mfano mimi wa kikundi kimoja kutoka kwenye Kata ya Muukulu kinachoitwa Usenga, kimeshafungua akaunti, kimeishaweka hisa karibu shilingi 900,000 na vikundi vingine. Tunavyo vikundi kama mia tatu thelathini na kitu kwenye Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivyo ndivyo mtuambie, rasilimali fedha, Wananchi wale wapate zile pesa kupitia kwenye vikundi tuondokane na mfumo wa pembejeo kupitia kwa mawakala. Katika hilo lazima tuseme vizuri na mfumo huo utawakomboa sana Wananchi wetu wa Tanzania na hasa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikwambie kitu; unajua sisi tunafikiri sana haya mambo ya kilimo kwa kuwa na Miradi mikubwa mikubwa, lakini ukiisoma Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2012, unaona kilimo kilisonga mbele kwa sababu ya kupeleka pembejeo, kupeleka mbegu bora na kwa sababu ya kutafuta namna na mbinu za kuwasaidia wakulima kuuza mazao yao. Haya ndiyo matatizo ya kimsingi ambayo nadhani rasilimali fedha itafutwe; kilimo kiwe cha kutumia zana bora za kilimo, mbegu ziende kwa wakati, mbolea ipatikane kwa wakati. Hilo likifanyika, sasa nitaona kabisa kwamba, yale tuliyoyafanya na ambayo yametupa heshima bado tukiongeza na hayo ninayoyasema, tutakuwa tumekwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kufanya nini? Tunachoweza kufanya bado niishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi; hivi ni kwa nini inaendelea kupata kigugumizi kupunguza misamaha ya kodi kwenye madini? Hapo pana matatizo. Katika Mpango huu namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie, sasa hivi tunazo rasilimali nyingi katika nchi yetu, tuna tatizo la rasilimali fedha, tunaendelea kutoa

misamaha na hasa kwenye eneo la madini; je, hali hii itaendelea mpaka lini?

Ninaomba hali hiyo iondoke, ikiondoka hiyo tutapata fedha na tukishapata fedha haya mafanikio niliyoyasema ambayo ni faraja kwa Watanzania, jumlisha na hiyo fedha nyingine, tutafika mbali sana. Tutatatua matatizo ya maji ambayo tumeshaanza kuyawekea mikakati mizuri; Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajua. Tutaendelea kusambaza umeme vijijini ambacho ni kipaumbele kikubwa. Tufanye Miradi ambayo inawagusa Wananchi moja kwa moja na Miradi inayowagusa Wananchi moja kwa moja ni ya kihuduma zaidi.

Miradi ya kihuduma zaidi ni kama hiyo ya kuwasaidia wapate pembejeo kwa wakati, wapate zana bora za kilimo, wapate masoko kwa ajili ya mazao yao, wapate maji ya kutosha na wapate umeme mpaka kule vijijini. Tukishafanya hayo, hiyo itakuwa inaendelea kuifanya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, ione kabisa kwamba inatekeleza Ilani yake kwa imani iliyopewa na Wananchi wa nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutengeneza vipaumbele, lakini utaratibu wa Bunge hili kujadili vipaumbele na Mpango wa Taifa ni kitu chema. Nami niseme, Mheshimiwa Waziri akae na atusikilize vizuri sana, hatutapenda kuona maneno haya ambayo Wabunge wamekuwa wakiyashauri, tena maneno ya msingi na maneno ya kwenda kuboresha kabisa Mipango ya Maendeleo katika nchi yetu, yafanyiwe kazi. Wakati mwingine inasikitisha kuona mambo tunayoshauri hayaendi kusimamiwa vizuri kiutekelezaji. Kwa hiyo, ninaomba sana hilo lizingatiwe na Serikali iwe makini na ione umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu ipo Miradi ambayo inaweza kutuokoa. Katika Mkoa wa Ruvuma sasa hivi tunayo machimbo ya makaa ya mawe kule Ngaka. Makaa mawe yale kama kweli yatafanyiwa kazi ya kutosha, hapa tunaambiwa bado

*[MHE. J. J. MHAGAMA]*

kuna majadiliano kati ya *TANESCO* na Wawekezaji *(TANCOM)*. Tunaomba hayo majadiliano yaishe, utekelezaji uanze, halafu basi tuone matokeo ya haraka. Hayo matokeo ya haraka tuweze kuyaona sasa. Tukiona hayo matokeo ya haraka yatatusaidia. Tuone matokeo ya haraka katika kuwasaidia wakulima, wakiwemo Wakulima wa Jimbo la Peramiho. Tuone matokeo ya haraka kama haya ya barabara yalivyotokea haraka, tuyaone na kwenye maeneo mengine. Maeneo ya elimu na afya, ndiyo sekta za huduma ambazo zitamwondoa Mtanzania kutoka katika janga hili la kuhangaika na umaskini wa kipato na kuweza kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya Ulaya, yalitokana na watekelezaji wa shughuli wadogo wadogo na wala siyo viwanda vikubwa vikubwa; vilikuwa ni viwanda vidogo vidogo na wakulima wadogo wadogo. Kwa hiyo, tukiendelea kufikiria sana Miradi mikubwa, tunapoteza muda. Turudi kwa wafanyabiashara wadogo, turudi kwa wakulima wadogo, tukiwafanyia hawa wote Mipango mizuri, watatusaidia sana kutuvusha katika maendeleo kwenye nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja hii na Mheshimiwa Waziri atusaidie kuyazingatia hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Chombo na Mheshimiwa Malocha ajiandae!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina matatizo na Mpango au Mipango ambayo Serikali imeleta kwa ajili ya kuijadili hapa. Hii siyo mara ya kwanza na wala haitakuwa mara ya mwisho kuleta Mipango mizuri namna hii. Tatizo letu Watanzania ni utekelezaji wa Mipango yetu tunayoipanga. Hii inatokana na kutosimamia vizuri sheria ambazo Bunge

*[MHE. M. A. CHOMBOH]*
hili Tukufu huwa linazipitisha katika utekelezaji wa mambo mbalimbali ambayo tumepanga kutekeleza na kuyasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tulilonalo katika utekelezaji wa Mipango yetu ni kwamba, sisi watu na ninafikiri nisiseme sisi watu niseme hivi; unakumbuka Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, alituambia kitu kimoja; alisema ili tuendelee tunahitaji vitu vine; Ardhi, Watu, Siasa Safi na Uongozi Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu katujalia tuna ardhi nzuri sana na kaipamba kwa kila kitu ambayo nchi nyingi sana hawana. Tatizo tulilonalo sasa hivi hasa wakati huu ni watu. Sensa iliyopita ilionesha tunao Watanzania karibu 44,000,000 au 45,000,000, lakini hao ni binadamu, tuna uchache wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchache wetu ni watu. Nikisema mtu au watu siyo Bodi. Utu ni kutofautisha baina ya mnyama, miti na viumbe vingine baina ya binadamu. Utu ni vitendo ambavyo binadamu mwenye umbo la binadamu anavitenda kwa masilahi ya binadamu wenzake, lakini pia kwa nchi yake, siyo kwa ubinafsi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna watu na kwa kuwa hatuna watu wa kutosha tunao wachache, watu wa kutosheleza hasa tukatimiza Mipango yetu hii ni wachache sana, waliokuwepo wameshaondoka na wanaendelea kuondoka, tukitaka kubadilika lazima turudi kwenye utu. Utu ule ambao aliusema Mwalimu Nyerere, kwamba; lazima tupate watu, uumwe na nchi, uumwe na wenzako. Ubinafsi umetuzidi, hatuwezi kuitekeleza Mipango hii. Mifano ipo mingi sana; tunazungumza vitu mdomoni tofauti na vitendo ambavyo tunatakiwa tuvifanye, hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna Sheria ya Mazingira imepitishwa hapa, anakuja mtu anavunja Sheria kwa makusudi halafu anakimbilia Mahakamani kuzuia Sheria ambayo ilipitishwa na Bunge hili na kusainiwa na

*[MHE. M. A. CHOMBOH]*

Mheshimiwa Rais isitekelezwe. Yeye kwa makusudi anaivunja halafu anakwenda kuweka kizingiti Mahakamani isitekelezwe na Mahakama inachukua hatua; huo ni utu kweli? Huo siyo utu ni ubinafsi. Huo ni mfano mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kingine; kwa mfano, juzi kuna mtu mmoja, huyo ni mtu, alitekeleza Sheria ya Usimamizi wa Magari makubwa ambayo yanaharibu barabara zetu, limekuwa zogo mji mzima, wakati anasimamia sheria ambayo yeye ni msimamizi mkubwa! Kuna mwingine alikwenda kusimamia Sheria kule Bandarini ili tupate masilahi ya nchi mambo yaende vizuri, kila mmoja anamwona yule ni mbaya. Tunataka watu kama hawa ambao wako *committed* ndiyo tunaweza kufanikisha kitu kama hiki kwa kila sehemu. Lazima tusimamie sheria ambazo tumezipanga wenyewe na tutekeleze ndiyo tutavuka katika kutekeleza Mpango huu. Serikali yetu imefika wakati sasa hivi inaajiri watu, inaajiri binadamu, maana wengine siyo watu ni binadamu, kwa kupata mshahara tu, lakini siyo kufanya kazi. Anaajiriwa mtu kwa kukusudia kupata mshahara siyo kufanya kazi.

Kuna vyama ambavyo vinasimamia masilahi ya wafanyakazi au haki za wafanyakazi, lakini hakuna Chama ambacho kinasimamia wajibu wa mfanyakazi. Wale wenye vyama vinavyosimamia masilahi ya mfanyakazi ni kweli wana-*trace* au wanakwenda kufuatilia kwamba hawa ninaowatetea haki zao wanatimiza wajibu wao? Wanatetea kweli hilo na kuna haki gani inayopatikana bila wajibu; lakini Tanzania tunakwenda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeajiri watu au imeajiri binadamu kwa ajili ya kupata mshahara siyo kufanya kazi. Saa nane au saa kumi za kufanya kazi, basi mtu anakwenda kufanya kazi kwa saa tatu au nne tu, muda mwingine wote yuko kwenye shughuli zake; hatuwezi kwenda. Nchi zinazoendelea zinafanya kazi zaidi. Tumeumbwa kufanya kazi, hatukuumbwa sisi kuja kustarehe tu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika saa 24 ujipangie wewe upumzike saa ngapi, lakini muda uliobakia wote unatakiwa ufanye kazi. Sisi tunaamini kwamba, kazi ni ibada. Mimi ni Mwislamu, lakini kazi ni ibada na ninafikiri vitabu vyote vya dini vinasema asiyefanya kazi huyo na asile. Sasa jamani ni watu sisi?

Tunakula bure bila kufanya kazi na bila kuwajibika; tukijipima sisi ni watu kweli? Tunataka tujirekebishe, tu-*change mind* zetu turudi kwenye utu ndiyo tutaweza kufika kwenye lengo ambalo tulisema ili tuendelee tunahitaji ardhi na ardhi tunayo na watu tuwepo, tukiwa na watu tutapata Siasa Safi na Uongozi Bora. Lazima tufanye hivyo ndiyo tutafika tunakotaka na ndiyo hapo tutakapoweza kutekeleza Mipango hii na mingine na mingine.

Inafika hadi sasa hivi watu wanatuambia ni aibu wanasahau angalau kidogo kidogo ndugu yangu pale alisema ni aibu, lakini sasa hivi kule Pemba kuna umeme mpaka chooni, barabara za lami kila kona, hakuna tatizo la maji sehemu zote Pemba maji ni safi na salama. Hiyo nafikiri siyo aibu isipokuwa alikuwa anasherehesha mambo, ni wajibu kila mmoja ana haki ya kusherehesha. Kwa upande huo ndugu zangu ninachokisema, ili tuweze kufanikiwa mambo haya na kuweza kutekeleza Mpango huu ni lazima turudi kwenye utu, utu ni vitendo, utu ni imani na utu ni moyo wa kuweza kufanya jambo hili likafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache mimi sina zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malocha!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa mambo mengi sana; imejaaliwa rasilimali nyingi ambazo

zinatosha kabisa kutuendeleza, kutusukuma na kutufikisha mbali katika suala zima la maendeleo. Nchi yetu ina rasilimali na rasilimali namba moja ni ardhi. Ardhi ambayo imesheheni mali nyingi; madini, maji yakiwemo maziwa, mito, mabwawa na kadhalika. Imesheheni ardhi nzuri ya kilimo, imesheheni mifugo mingi ambayo wengine wanaanza kuirarua baada ya kukosa maarifa ya kuitumia wanairarua kwa kuipiga risasi na pia imesheheni misitu mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo kila aina ya rasilimali zinazoweza kutuwezesha kuiendeleza nchi hii na Watanzania tukaishi maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida tuliyonayo katika nchi hii ni ukosefu wa wasimamizi wazuri, ambao wamekosa uadilifu, wamekosa uwajibikaji, wamekosa uzalendo na wamekosa ubunifu. Hata kama nchi ingekuwa na rasilimali kiasi gani, kama baadhi ya wasimamizi wake siyo waadilifu, siyo wachapakazi, siyo wabunifu na siyo wazalendo ni bure. Kwa hiyo, namba moja katika jambo lolote lile ni uadilifu, uwajibikaji, uzalendo na ubunifu na ndiyo maana utakuta Wizara ambazo zina watu wa namna hiyo ndiyo zinaonekana zinaipa sifa nchi hii.

Mimi nashangaa Wizara ambazo hazitaki kuiga mifano ya Wizara ambazo zinasemwa kila kona kwa mazuri; maana yake hiyo ni dalili ya kushindwa kazi na wanapaswa kujiuliza kwa nini Wizara fulani inasemwa kila mahali; je, mimi niliyepewa mamlaka kwa nini nisioneshe uwezo wangu? Mambo hayo yanapaswa kujiuliza kwa mtu yeyote aliyepewa dhamana; nafasi hii niliyopewa watu wanasemaje juu yangu? Ukiwa na mawazo haya utafanya kazi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu karibu asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo, lakini mimi nataka kuzungumzia wakulima wadogowadogo. Wakulima wadogowadogo kwa sehemu kubwa ndiyo wanaolibeba Taifa hili katika kulilisha japokuwa nchi haijawatazama. Wakulima wadogowadogo ndiyo wanaoibeba nchi hii

katika kuilisha pamoja na mitaji yao midogo na kutumia nguvukazi yao.

Ninachotaka kuzungumza na ambacho Serikali inapaswa kuliangalia ni kwamba, wapo wakulima wadogowadogo ambao wanakosa mahali pa kulima, hawana kabisa sehemu ya kulima na nchi yetu tunatakiwa kufanya utafiti kuangalia ni Watanzania wangapi ambao wanategemea kilimo hawana ardhi ya kulima wakati tukiwa na ardhi ambayo imekaa na mapori, imemilikiwa na watu ambao hawaiendelezi wamekaa nayo tu sanasana wanafanya kazi katika kuikodisha badala ya kuendeleza kile walichokusudia. Kwa hiyo, jambo hili tunapaswa kuliangalia kwa umakini sana vinginevyo litafutikisha pabaya.

Tunashuhudia migogoro ya wakulima na wafugaji, wakulima na wawekezaji na kadhalika. Jambo hili Serikali inapaswa kulitafutia majibu ya haraka kwa sababu kwa hivi sasa kila kona unakuta kuna migogoro kati ya wakulima na wafugaji na wakulima na wawekezaji. Sasa nani atatue migogoro hiyo kama siyo Mawaziri waliopewa dhamana ya kusimamia mambo hayo?

Utakuta kila kona ni matatizo ya ardhi na migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima na wawekezaji, ni migogoro na maeneo mengine yanaleta mauaji makubwa. Lazima Serikali iangalie ni namna gani inaweza kutatua matatizo hayo; bila kufanya hivyo tutashuhudia migogoro mikubwa sana huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninataka kutoa mfano mmoja; jambo la kusikitisha ni kwamba, hata pale ambapo Rais anatoa maagizo kwa Waziri kwamba nataka tatizo hili lishughulikiwe haraka, Waziri hashituki! Sasa watu wasipomheshimu Rais nani ataheshimiwa katika nchi hii? Rais akitoa agizo maana yake ni agizo la kuvalia njuga, watu wote mliopewa dhamana mnapaswa kulishughulikia.

*[MHE. I. A. MALOCHA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano; mwezi wa sita, Mheshimiwa Rais alitoa agizo namna ya Waziri kushughulikia mgogoro wa Shamba la Malonje na akasema kwa namna yoyote ile lazima ardhi ile irudishwe kwa Wananchi! Nami sheria inaniruhusu kama msimamizi wa ardhi, kama kuna tatizo lolote naomba Waziri aniletee, akiniletea saa moja basi saa tatu nitakuwa nimetatua. Cha ajabu mpaka sasa hivi suala hili halina majibu wala halishughulikiwi, pamoja na jitihada za Mkoa kukumbusha mara kwa mara. Kwa hiyo, mnachotaka kuona, Serikali inataka kushughulikia mauaji huko baadaye, maana mmezowea kuendesha kwa dharura za kuvamia matatizo.

Matatizo yanapoibuka ndiyo Serikali inaonekana kupeleka utatuzi, jambo ambalo siyo jema. Naishauri Serikali jambo hili lishughulikiwe haraka; vinginevyo, hali ninayoiona inaweza ikatuletea matatizo huko mbele. Naomba Waziri mwenye dhamana, arudie agizo la Mheshimiwa Rais kushughulikia jambo hili haraka.  Mimi naliona ni la hatari na ninazungumza ili Wananchi wasikie kwamba, wajibu wangu nimeutimiza, sasa kama tatizo linatokea ni suala la Serikali.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia Miradi ya Umwagiliaji. Sisi sote tumekubali kwamba, ili nchi hii iweze kuleta tija katika suala la kilimo ni lazima tuboreshe Miradi ya Umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji ni kilimo cha uhakika, lakini inashangaza toka mwaka 2005 ipo Miradi ambayo imeanza lakini mpaka sasa haijakamilika. Kama kuna Miradi mitano au minne unakuta hata mmoja ulioanza haujakamilika. Sasa tunakwenda wapi?

Nataka tujiulize kama tunaona uwezo wetu ni mdogo kwa nini tuna-*prolong* Miradi mingi ambayo tunashindwa kuitekeleza halafu baadaye tunaaza kupimwa kwa Mipango ambayo tuliisema sisi wenyewe halafu utekelezaji wake umekwama? Kwa hiyo, lazima turudi tujisahihishe tuhakikishe Miradi ile tuliyoipanga tunaisimamia barabara.

*[MHE. I. A. MALOCHA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano; katika Jimbo langu tuna Miradi kama mine; Mradi wa Sakalilo, Maleza, Ng'ongo na Zia, lakini hakuna hata Mradi mmoja ambao umekamilika, hata ule ulioanza Sakalilo mwaka 2006 mpaka sasa hivi haujakamilika; tunategemea nini? Mipango hii tunayoipanga mbona naona kama tunairudia ileile tuliyoipanga utekelezaji wake haujakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinapotolewa nusunusu ni lini Miradi hiyo itamalizika? Na hata ikimalizika basi itamalizika kwa kiwango ambacho siyo kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la miundombinu ya barabara. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kazi nzuri na kubwa ambayo imejitahidi kuunganisha Mikoa katika suala la barabara za lami mipakani. Nitoe rai, yapo maeneo ambayo yanahitaji kuwa na barabara nzuri ili kuweza kuharakisha kukuza uchumi. Zipo kanda mbalimbali ambazo zinatakiwa Serikali iangalie kuboresha barabara katika Kanda zile na hasa Kanda za Maziwa. Kanda za Maziwa zinabeba idadi kubwa sana ya watu; watu wanatoka mikoa mbalimbali wanakimbilia maeneo yale kwa sababu ya uvuvi, rutuba nzuri na maeneo mazuri ya kushughulika na Miradi mbalimbali. Kwa hiyo, Kanda kama hizo inatakiwa Serikali iboreshe barabara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano; ipo barabara ya kutoka Kilimetundu – Muze – Stalike – Kibaoni mpaka Mpanda, Ukanda ule wa Ziwa Rukwa rasilimali yake ni kubwa sana kwa upande wa ardhi, ni ardhi nzuri na yenye rutuba nyingi, hakuna zao linalokataa na yanakomaa kwa haraka. Vilevile ni eneo ambalo lina mito mingi sana ambayo ingeweza kutumika katika suala zima la umwagiliaji, ina mito zaidi ya 40 ambayo haikauki. Serikali inapaswa kuangalia njia ya kuwekeza katika kuitumia ile mito ili kuweza kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni umeme. Umeme ni ajira na ni uchumi. Tunapozungumzia suala la uchumi, kwanza, niipongeze

Serikali kwamba imeanza vizuri katika suala hili, lakini lazima tuangalie ni maeneo gani ambayo tunapaswa kuwahisha umeme kulingana na utayari wa Wananchi katika kuutumia umeme ili kuweza kukuza uchumi na kusaidia maeneo mengine. Maeneo mengine unapeleka umeme lakini Wananchi hawako tayari wanauangalia tu na wanaangalia nguzo. Yapo maeneo ambayo Wananchi wako tayari na walishajiandaa kupokea umeme katika suala zima la kuendeleza uchumi wao. Kwa mfano, naweza kuuzungumzia Mkoa wa Rukwa; Wananchi wa Mkoa wa Rukwa ni wachapakazi, wanazalisha kwa kiasi kikubwa sana na wanasaidia nchi hii katika suala la kilimo, lakini umeme umeishia mjini tu, vijijini hakuna. Mpango wa kupeleka umeme vijijini naona kama unasuasua, unaanza kuelekezwa maeneo ambayo ukiangalia hayana tija hata ya uzalishaji. Hakuna kitu utakacho-*gain* kwa muda mfupi ili kuleta maendeleo katika suala zima la uchumi. Kwa hiyo, pamoja na kupeleka umeme ni lazima tuangalie maeneo ambayo yanaweza kutoa majibu ya haraka katika kukuza uchumi na siyo suala tu la kupeleka, maana umeme ni gharama, tunategemea ukienda kwenye maeneo uweze kuleta *impact* ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nami ningeweza kuishauri Serikali kuwa, kwa Mkoa wa Rukwa harakisheni kupeleka umeme vijijini kwani Wananchi wanahitaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Mbowe, ajiandae Mheshimiwa Vullu, tutamalizia na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mmojawapo ya wachangiaji wa mwisho kwa jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisikiliza mazungumzo ya Waheshimiwa Wabunge, kinachogombaniwa hapa ni

namna ya ugawaji wa Keki ya Taifa. Cha msingi zaidi ni kwamba, hii Keki ya Taifa kama hakuna uzalishaji wa kutosha, kugawa kwake kunakuwa ni matatizo siku zote. Hilo la kwanza.

La pili, Mpango huu haujaweka mkakati wowote wa namna ya kupunguza matumizi makubwa ya Serikali. Hata tukirumbana na tukapanga Mipango mizuri, kama kile cha kugawa kwenye Mipango ya Maendeleo tumeshakitumia katika uendeshaji wa Serikali, ni dhahiri tutaendelea kurumbana kila siku na haitatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mpango wa Miaka Mitano, *ratio* ya matumizi ya kawaida ya Serikali na matumizi ya maendeleo, ilikuwa imekusudiwa iwe asilimia 65 kwa 35. Kwa mtazamo wetu nafikiri ingeweza ikabanwa vilevile zaidi ikawa *ratio* ya matumizi ya kawaida ya Serikali ikawa asilimia 60 na asilimia 40 ikapelekwa kwenye maendeleo. Tungeweza kufanya hivyo kwa kujibana katika matumizi ya Serikali, tungekuwa tuna *resources* nyingi za kupeleka kwenye shughuli za maendeleo. Nina hakika marumbano na ugomvi unaoelekea kujitokeza mahali hapa usingekuwa na sababu yoyote ya kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Serikali yameendelea kuwa makubwa sana. Ukiangalia historia, kwa miaka 15 iliyopita, mimi niliingia Bunge hili kwa mara ya kwanza kabisa mwaka 2000; mwaka 2000 *Government Budget* ilikuta shilingi trilioni 1.6, lakini leo tunakimbilia trilioni 30. Tunazidi kupanua wigo na ukubwa wa Serikali, tunapanua Wilaya, Mikoa, Kata na Vijiji. Pamoja na nia njema ya kupeleka utawala karibu na Wananchi, lakini maana yake ni kwamba, tunaongeza ukubwa wa matumizi katika masuala ya *administration* na tunapunguza fungu ambalo lingeweza kwenda kwenye maendeleo ya kuwasaidia Wananchi moja kwa moja. Kwa hiyo, napenda kuzungumza kwamba, kuna umuhimu sana wa kuliangalia hili.

*[MHE. F. A. MBOWE]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mtazamo wa muda mrefu na mitazamo ya kiuchumi, lazima tuangalie tunagawaje hii Keki ya Taifa, tunatawala vipi rasilimali za Taifa hili. Bado tunaendelea kupanga kila kitu Dar es Salaam, kila kitu kinapangwa na Baraza la Mawaziri Dar es Salaam, ndiyo wenye maamuzi makubwa ya mwisho. Watanzania wote sasa hivi wanaiangalia Dar es Salaam, wanamwangalia Mheshimiwa Rais, wanamwangalia Waziri Mkuu na wanaiangalia Serikali kuomba.

Hebu tufikirie tunapokwenda kuandika Katiba mpya, umuhimu wa sisi kama Taifa kufikiria upya suala la *decentralization*. Tuna uwezo mkubwa sana kama Taifa ku-*manage resources* zetu kama tutaacha utaratibu wa kutegemea *centre* moja ndiyo ikae na kapu lenye mayai yote ya Taifa hili. Tufikirie upya mfumo wa utawala wa uchumi wetu ili kuwasaidia Watanzania kuwa *beggars* katika nchi yao. Hilo lilikuwa jambo la kwanza ambalo nimeona nilizungumze siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kulizungumza, nimeangalia Mpango wa Maendeleo wa mwaka huu ambao tunakwenda nao sasa; yamefanyika mambo mengi, lakini nisikitike tu kusema kwamba, nimejaribu kuangalia kuna Mpango gani wa Maendeleo mkubwa ambao umefanyika katika Mkoa wangu wa Kilimanjaro, kwa bahati mbaya sikuuona.

Kuna jambo moja ambalo ninapenda nilizungumze; nimezungumza kwenye bajeti ya mwaka jana, nimezungumza kwenye bajeti ya mwaka juzi na ninaona bado haijaingia kwenye akili ya wenzetu, pengine naomba hili mlitafakari kwa kina sana. Hili liko vipi?

Mlima Kilimanjaro ni chanzo kikubwa sana cha mapato ya utalii na mapato ya Taifa letu. Mlima Kilimanjaro unaliingizia Taifa hili mapato ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 50 kila mwaka na dhahiri unatoa ajira kwa watu wengine wengi sana. Kwa hiyo, kunakuwa na *multiplier*

*effect* kubwa sana kwa upande wa utalii katika *Northern Circuit.*

Nikiangalia Serikali inauangaliaje Mlima huu, inautunzaje na mazingira yanayouzunguka, ile *Kilimanjaro Ecosystem* yote inaendelezwa vipi ili kuhakikisha unaendelea kuwa na barafu ambayo itaendelea kuwavutia wawekezaji na kuwavutia watalii kwenda kuupanda. Ni kama vile tunachuma kwenye Mlima Kilimanjaro, hatujali mazingira ya Kilimanjaro, hatujali theluji ya Kilimanjaro, ni kama tunataka kumchinja bata anayetaga mayai ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wetu wa Taifa kwa mwaka ujao ninaomba sana wanaohusika wakaangalie uwezekano wa kufikiria kuhusu kitu kinachoitwa *Kilimanjaro Ecosystem.* Nimelizungumza hili mwaka jana, nimelizungumza na Waziri wa Utalii, tumeunda na Kamati ambayo haikufanya lolote mpaka leo; matokeo yake theluji inazidi kupotea, mazingira yanazidi kukauka na maji yanapotea Kilimanjaro.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, maji yanayoteremka katika Mlima Kilimanjaro yako katika *Management* ya *Pangani Water Basin*. Sasa hivi tunashuhudia vita kati ya wakulima na wafugaji, katika miaka michache iyajo tutakuwa na vita ya maji. Katika Mikoa ya Kanda ya Kaskazini na kipekee Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha na Manyara, tunakwenda kuwa na vita ya maji kwa watu walioko milimani *(upstream)* na watu walioko mabondeni *(downstream)*.

Leo tunapozungumza watu waliopo *upstream* hawaruhusiwi kutumia maji kwa sababu maji yale yanatakiwa yaende *downstream* yakawasaidie watu wanaoishi *downstream* na watu hawa hawana kilimo kwa sababu hakuna ardhi, watu hawa hawana *mining* kwa sababu hakuna madini, watu hawa hawana uvuvi kwa sababu hakuna mahali pa kuvua na hawana mifugo kwa sababu hakuna ardhi ya kufugia.

*[MHE. F. A. MBOWE]*

Sasa, kama hatukufanya utaratibu maalum wa *water management* katika mabonde kama ya *Pangani, Arusha* na *Meru Basins,* tunakwenda kusababisha vitu ambavyo ninahisi vitakuwa na hatari sana kwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo lingine; ni kwamba, maeneo haya ninayoyazungumza yana udongo ambao ni mzuri mno, kuna *infrastructure* ambayo ingeendelezwa kidogo ingeweza kuwa eneo zuri sana la uzalishaji na kutengeneza kilimo ambacho ni *high yield,* yaani kilimo ambacho kinazalisha mazao yenye bei kubwa kwa ajili ya kuuza kwenye masoko ya nchi za nje.

Tuna *Kilimanjaro International Airport,* Uwanja ambao haujatumika *effectively* kusafirisha *horticulture,* kwa sababu hakuna maji ya kuwezesha kufanya *horticulture* Kilimanjaro na Arusha. Ninachoomba kifanyike; iwepo mikakati ya makusudi ya kuvuna maji ya mvua ili kutoa ugomvi wa maji na kuvuna maji ya mvua; ni *infrastructure* rahisi sana wala hatuhitaji *rocket science*. Sijui ni kwa sababu gani wakati wa masika maji yanakimbilia baharini, tunalia mafuriko, kikija kiangazi tunaomba chakula.

Serikali inaweza kujenga miundombinu rahisi sana katika mabonde ya Mlima Kilimanjaro. Imezungumzwa mara nyingi, kuna mabonde makubwa mno, ni kujenga *dykes* tu *upstream* halafu tunafanya *gravity irrigation*. Tunaweza tukanywesha chini Wananchi wale wakazalisha mwaka mzima bila kungojea mahindi ya msaada au misaada mingine yoyote. Hii ni *Economic Management*, naomba watu wa *Planning* walisikie suala hili na waone watasaidia vipi kwa sababu *Zone* ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara mpaka Tanga, ina uwezo mkubwa sana wa kufanya *production* kwa sababu ya *export* na *Kilimanjaro International Airport* tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza na hili ninaomba Waheshimiwa Wabunge mnielewe vizuri sana, ni kauli zetu wanasiasa. Ni

jambo la kusikitisha sana kwamba, tunataka kuua kitu ambacho tumekilea wenyewe, tumekijenga wenyewe, kimefikia hatua tunataka kukiachia kidondoke bila sababu za msingi kwa sababu ya kauli. Siyo tabia nzuri za kidiplomasia kubeza nchi za wenzetu, w*hether* ni nchi ndogo ama ni nchi kubwa. *Impact* ya kuvunjika kwa Afrika Mashariki itaathiri Uchumi wa Tanzania kuanzia Mwanza, Mara, Kilimanjaro, Manyara, Arusha na maeneo mengine mbalimbali. Tunahitaji kutafuta suluhu na majirani zetu, hatuhitaji kutafuta ugomvi na majirani zetu, wala hatuna sababu ya kubeza. Tanzania tuna heshima, tuna mazoea ya kuwa wanadiplomasia. Huu utamaduni wa kuanza kuwadharau na kuwadhalilisha wenzetu tunaupata wapi? Siyo utamaduni wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, hili jambo lifikiriwe kwa makini sana, tunahitaji kutafakari mahusiano yetu badala ya kuyaangamiza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbowe, muda wako umeisha.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Zaynab Vullu, tutamalizia na Mheshimiwa Murtaza Mangungu!

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie Mpango huu wa Maendeleo. Kabla sijaanza kuchangia, nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Mbowe, kwa kauli yake aliyoibaini kwamba, kauli zetu wanasiasa za kudharauliana na kubezana si za kujenga. Hilo kwa kweli nampongeza ameliona na nishauri tu kwamba, tusione kwa nchi za jirani, tuanze kuona kwetu wenyewe Watanzania ili tuweze kujenga nchi yenye amani na upendo. *(Makofi)*

*[MHE. Z. M. VULLU]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijikite katika hoja ya msingi iliyotuweka humu ndani. Niipongeze Serikali kwa kufanya kazi zake kama ilivyokuwa imepanga, kwa kuhakikisha maendeleo yanawafikia Wananchi. Hakuna Mbunge yeyote humu ndani atakayesema kwenye Jimbo lake au Wilaya yake hakuna maendeleo ambayo yamefika. Hatuwezi kuijenga nchi nzima kwa siku moja, tunajenga kwa awamu. Sote tumeona barabara, maji, umeme na tumetangaziwa humu ndani, majimbo karibu vijiji vyote kama siyo robo au robo ya tatu ya vijiji umeme utakwenda. Siyo mtu atoke hapa ajidai kwamba, yeye ndiye amepeleka umeme, umeme huu umeletwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haukuletwa na Mbunge, aseme mimi nimeenda kuleta umeme. Kwa hiyo, hili ni letu wote kwa ujumla na ni la kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wana msemo wao wanasema kwamba: "Ili jambo liwe zuri, lazima kuwe na mabaya au kuwe na upungufu ambao unahitaji kuboreshwa." Naomba yafuatayo; kwanza, kuna mgogoro wa wakulima na wafugaji. Tunazungumzia hali ya uchumi imeongezeka, lakini Wananchi wa kule vijijini sidhani kama hili wanalijua kwamba, hali ya uchumi imeongezeka kwa sababu mkulima analia na mazao yake, mfugaji analia na ng'ombe wake. Watu hawa tuliambiwa hapa na Serikali kwamba, tutapeleka maendeleo pale hawa ng'ombe wanapopelekwa kwenye Halmashauri zetu, lakini hadi hii leo Halmashauri zetu hazijawezeshwa hata senti tano; tunategemea nini?

Tunategemea wafugaji wale watatengenezewa vipi miundombinu? Sote tunafahamu jinsi gani Halmashauri zetu hazina kipato cha kutosha, hiyo miradi ya kawaida tu mingine inasuasua, sasa sikwambii wameongezewa na jukumu la kuandaa mahali pa kuweka mifugo. Ombi langu kwa Serikali; nimeona Mpango, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja atueleze Serikali ina mkakati gani wa kuziwezesha Halmashauri ili ziweze kujipanga kutengeneza miundombinu, malambo, majosho na maeneo

ambayo watalishia wale ng'ombe badala ya kuwafanya wafugaji wadhalilike na mifugo yao, halikadhalika wanawadhalilisha wakulima kwa sababu mkulima anategemea mazao yake na mfugaji anategemea ng'ombe wake, sasa watu hawa wanapigana.

Naomba nijibiwe, mwisho wa siku watu hawa watakuwa na kipato chochote? Mfugaji mwisho wa siku atakuwa hawezi kuuza ng'ombe kwani ng'ombe wake watakuwa wamepigwa na yeye mwenyewe kapigwa. Halikadhalika, mkulima mwisho wa siku mazao yake yameliwa na yeye mwenyewe amepigwa. Tunaomba Serikali itusaidie kutatua hii migogoro kwa kuziwezesha Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo na mgogoro wa wakulima linaweza likaharibu hata miundombinu ya maji. Sasa hivi Mto Rufiji tumepewa kivuko kule Utete, lakini hakifanyi kazi kwa sababu maji yamekauka. Mto Rufiji hauna asili ya kukauka, lakini sasa hivi Mto huu umekuwa wa msimu na tatizo kubwa ni wafugaji. Wakulima wakiona wafugaji wamewavamia wanahama kutoka eneo moja kwenda lingine. Wafugaji wakiona majani yameisha pale na hawana maji ya kunywesha mifugo yao, wanakwenda kule ambako wenzao wapo. Sasa hii migogoro mingine, Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha haitakuwepo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma hatukusikia mfugaji yeyote akilalamika wala ng'ombe wakidhalilika, kwa sababu wale nao ni viumbe, lakini bahati mbaya hawawezi kusema. Tumeshuhudia kwenye maeneo yetu wanapigana, zile Kamati zetu za Usalama za Wilaya na Mikoa zinaishiwa nguvu kwa sababu hazina nyenzo, ziwezeshwe ili linapotokea tatizo waende; lakini unakuta askari wana gari lakini petroli hakuna au gari lipo lakini matairi matatu ni mazima, moja ni bovu, wanakokwenda mitandao haifanyi kazi, hawana *radio call;* tunawasaidia nini hapo wakulima na wafanyakazi? Ningeomba sana hilo nalo tuliangalie. *(Makofi)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema maendeleo, maendeleo yanaletwa na maji na umeme. Nitoe kilio cha Wanakisarawe, Kisarawe hatuna viwanda, tumebahatika kupata kiwanda kimoja cha Saruji lakini nacho kinashindwa kufanya kazi. Naiomba Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Maliasili na Utalii, wakae pamoja na watusaidie lile eneo la Pugu mpaka Kazimzumbwi, wamekataa nguzo za umeme zisipite. Tunaomba Wizara hizi mbili zikae zijadiliane, wapitishe nguzo za umeme ili na Wanakisarawe waweze kupata umeme, kiwanda kile kifanye kazi na maeneo mengine yaweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hapo tu, na maeneo mengine ya Wilaya za Mkoa wa Pwani. Tunapozungumzia Mkoa wa Pwani ni lazima utaje Wilaya zote kwa masilahi ya Wilaya. Naomba hilo Wizara ilifuatilie ili tuweze kuona tunasaidiana vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitoe nafasi kwa wengine, lakini naomba mwisho wa siku nipate majibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Sasa Mheshimiwa Mangungu!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kustajabu kidogo. Nimestaajabu sana baadhi ya wachangiaji hapa wamekuwa wakilaumu, kushutumu na kuweka wimbo wa kusema kwamba ni aibu, lakini mtu yeyote mwenye fikra na akili timamu, kufagia unaanzia uliposimama. Wenzetu hawa ambao wamekuwa wakilalamika sana, wameshindwa hata kujenga kule nyumbani, maghorofa yanamiminwa Kariakoo na maeneo mengine ya Ilala. Sasa hili ni jambo ambalo inabidi ujiulize sana, mkataa kwao ni mtumwa. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aibu!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wapo wengine ambao wamekuwa wakisomesha watoto nje ya nchi kutokana na fursa na miundombinu iliyowekwa na Serikali hii inayowatia wao aibu, lakini katika kuudanganya umma, wanakuja hapa kusema ni aibu. Sasa inabidi tujiulize! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchangiaji wa Wabunge niliamini sana tusimame pia katika jambo linalohusu ukweli, kwa sababu sisi ni watu ambao tumepewa dhamana katika nchi hii na tunao wajibu wa kuwawakilisha waliotuchagua. Wakati wa uchangiaji, yuko Mbunge mmoja ambaye alisema mpaka leo *TPDC* inaingia mikataba bila kuangalia na hakuna masilahi yoyote ambayo Watanzania wanayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ya Nishati na Madini, na ni mtu ambaye ninamwamini sana Mungu, siwezi nikakubali niingie ndani ya Bunge hili nikatamka kitu ambacho hakina ukweli. Ukiangalia Sheria ya Uchimbaji na Utafutaji Mafuta na Gesi ya mwaka 1980 ambayo inafanya kazi hadi sasa, mapato na mgawanyo kutokana na ile *Production Sharing Agreement* (*PSA*), Serikali kupitia *TPDC* inapata asilimia kati ya 65 hadi 75. Sasa leo hii tunaposema *TPDC* ipate japo asilimia 40; mbona tunapata zaidi ya hapo? Huwezi ukamulika tochi unakotokea, lazima umulike unakoelekea ili uweze kupata mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Mawaziri wengine wote, lazima tukubaline; haiwezekani ikawa mimi ndiye ninaumwa homa halafu akatibiwa mtu mwingine ili nipone mimi. Hilo haliwezekani na ni jambo ambalo halina mantiki na haliingii akilini.

Tumekuwa na malalamiko katika Mipango yetu ambayo tunaiandaa. Wabunge wengi wamechangia

*[MHE. M. A. MANGUNGU]*

hapa kwamba, fedha nyingi zinapelekwa katika maeneo ya mijini, maeneo ya vijijini ambapo sisi wengine tunatoka hakuna fedha zinazopelekwa kutekeleza Miradi.

Tunasema kwamba, uchumi unakua kwa asilimia saba, ukisoma aya ya 1.2 ya kitabu hiki inasema, uchumi umekuwa ukikua kwa asilimia saba lakini Wananchi hawanufaiki kwa sababu uchumi huu umejengwa katika maeneo machache. Hatujakuza kilimo, Wananchi wanazalisha mazao hayafiki sokoni yanaharibika. Wananchi wanazalisha, lakini umeme wa kuweza kuzalisha kuongeza thamani ya mazao haya hakuna. Leo hii mpaka vijijini watu wanaishi kwa kutegemea kwenda dukani. Mapato yanatokana na nini? Kila siku asubuhi atoe fedha akanunue sukari, unga, mchele, hali ya kuwa ardhi na maeneo ya kuweza kuzalisha mazao haya yote tunayo lakini bado hatujafikia kuweza kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika Mipango ambayo imeandaliwa na Serikali, lakini niseme tu kwamba, hatuwezi kufanikiwa haya yote kama kuna urasimu. Leo hii Wizara na Wizara zinaweza zikawasiliana kwa muda wa miaka mitatu barua hazijajibiwa. Tumekaa hapa tunajadili vyanzo vipya vya mapato ya Serikali, bandari hatuitumii. Leo hii kuna ugonjwa ambao ni lazima upatiwe dawa na ufumbuzi wa kudumu, mitandao. Ukienda Halmashauri unaambiwa mtandao haufanyi kazi watu hawawezi kulipwa fedha *EPICAR* imekwama. Ukienda *TRA* unaambiwa leo mtandao uko *down* hatuwezi ku-*process,* mizigo ya watu inakwama bandarini. Bandari vilevile wanakwambia mtandao haufanyi kazi; sasa huyu mtandao ni nani?

Leo hii mnakuja hapa mnatuambia Mipango ya maendeleo Serikali iongeze mapato; unaongeza vipi mapato bila kuwa na *efficiency* kwenye utekelezaji wako? Haya hayawezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwa tatizo kubwa sana kukosa *consistence* kwenye Mipango ya Serikali. Tuna chuma na makaa ya mawe Liganga, tuna Nickel ambayo

imeshafanyiwa utafiti na imegundulika Nachingwea, Ruangwa na maeneo ya Nakiu kule Kilwa, tunaisafirishaje kuifikisha Bandarini? Bandari ya Mtwara unaambiwa mipango inaendelea, itafanyika itakuja pale; chuma kile tunakisafirishaje? Kitasafirishwa na barabara? Mipango ya reli haipo, aah! Hili tuliangalie kwa makini, lazima Mipango yetu iwiane na utekelezaji na mahitajio halisi kwa wakati tulio nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 54 ile aya ya 3.3.4 imesema, Misitu na Wanyamapori. Hawa wanyama kwa tafsiri niliyo nayo mimi sasa hivi wanayo haki ya kuishi kuliko binadamu. Wananchi wa maeneo ya Njinjo, Miguruwe, Kandawale, Mitole, Miteja, Nanjilinji na kwingineko Kilwa, wanapigwa bila sababu, bila kufikishwa mahakamani, hukumu zinatolewa na Wananchi hao wamekosa haki ya kuishi; hili ni tatizo kubwa sana. Nashukuru nimezungumza na Mheshimiwa Waziri, amenipa majibu ambayo yanawiana na kulipatia ufumbuzi wa kudumu, lakini hili ni tatizo kubwa na lazima tuliangalie. Hizi operesheni zisitumike kwa ajili ya kunyanyasa na kuwatesa Wananchi wasiokuwa na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa kutokana na muda ni madeni ya ndani. Kila mwaka tunapanga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni ya ndani, wafanyabiashara hawa wanakopa kwenye benki kwa mikopo ambayo ina riba ya hali ya juu kabisa. Wakishakopa Serikali baada ya kupewa huduma inachukua muda mrefu, watu wengine wana zaidi ya miaka minane, tisa, hawajalipwa, nyumba zinauzwa, mali zao zinanadiwa bila sababu.

*(Hapa kengele ililia kushiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu, nakushukuru, kaa chini. *(Kicheko)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi. *(Kicheko)*

*(Saa 1. 35 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 1 Novemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*